

3009=  
**MAIGIZO KAMA MBINU YA MAUDHUI  
KATIKA RIWAYA MBILI ZA  
KEN WALIBORA**

**NA**

**RAJAB OCHENJA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI  
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU  
CHA KENYATTA**

**2008**

Ochenja, Rajab  
*Maigizo kama mbinu  
ya maudhui katika*




08/330250

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine



RAJAB OCHENJA  
(MTAHINIWA)

25-4-08

TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya Chuo Kikuu cha Kenyatta



DKT. R. M. WAFULA

25-4-08

TAREHE



DKT. C. MOMANYI

25/04/08

TAREHE

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Suleiman Juma na Mansura Juma.

Natabaruku kazi hii pia kwa mke wangu Maridhia Lilian na kwa watoto wetu

Ahmed, Seif na Yasin Juma.

## YALIYOMO

Mada .....	i
Ungamo .....	ii
Tabaruku .....	iii
Yaliyomo .....	iv
Shukrani .....	vii
Ikisiri .....	ix
Ufafanuzi wa Istilahi .....	xii

<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Swala la Utafiti .....	3
1.2 Nadharia Tete .....	4
1.3 Malengo ya Utafiti .....	4
1.4 Sababu za Kuchagua mada .....	5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....	6
1.6 Msingi wa Nadharia .....	7
1.6.1 Uhalisia kama Nadharia ya Uhakiki .....	7
1.6.2 Mihimili ya Uhalisia .....	9
1.6.3 Nadharia ya Uigizaji .....	10
1.6.4 Mihimili ya Nadharia ya Uigizaji .....	14
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada .....	14
1.8 Mbinu za Utafiti .....	17
1.8.1 Kuchanganua Data .....	18
1.9 Kiishilio .....	18

<b>SURA YA PILI .....</b>	<b>19</b>
Historia, Usuli na Kazi za Ken Walibora .....	19
2.0 Utangulizi .....	19
2.1 Historia na Usuli wa Ken Walibora .....	21
2.2 Kazi za Ken Walibora .....	28
2.2.1 Riwaya ya <i>Siku Njema</i> .....	28
2.2.2 <i>Ndoto ya Almasi</i> .....	30
2.2.3 Vijiriwaya .....	31
2.2.4 Hadithi Fupi .....	34
2.3 Kiishilio .....	36
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>38</b>
Uigizaji na Uhalisi kama Nyenzo za Maudhui katika <i>Ndoto ya Amerika</i> .....	38
3.0 Utangulizi .....	38
3.1 Maelezo ya Jumla juu ya <i>Ndoto ya Amerika</i> .....	39
3.2 Uigizaji na Uhalisi kama Nyenzo za Maudhui katika <i>Ndoto ya Amerika</i> .....	40
3.2.1 Sifa za Wahusika .....	40
3.2.2 Maneno na Vitendo vya Wahusika .....	45
3.2.3 Lugha ya Wahusika .....	53
3.2.4 Mandhari .....	58
3.2.4.1 Akilini .....	58
3.2.4.2 Nyumbani .....	62
3.2.4.3 Kortini .....	63
3.2.4.4 Mada .....	64
3.3 Kiishilio .....	67

<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>69</b>
Maelezo ya Jumla juu ya Riwaya ya <i>Kufa Kuzikana</i> .....	69
4.0 Utangulizi .....	69
4.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Riwaya ya <i>Kufa Kuzikana</i> .....	69
4.2 Maigizo na Uhalisi kama Nyenzo za Maudhui katika Riwaya ya <i>Kufa Kuzikana</i> .....	71
4.2.1 Tabia za Wahusika .....	73
4.2.2 Maneno na Vitendo vya Wahusika .....	80
4.2.3 Lugha ya Wahusika .....	89
4.2.4 Mandhari .....	102
4.2.5 Mada .....	113
4.2.5.1 Ukabila .....	114
4.2.5.2 Ufisadi .....	115
4.2.5.3 Mila na Athari zake .....	116
4.3 Kiishilio .....	119
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>121</b>
Hitimisho la Utafiti .....	121
5.0 Utangulizi .....	121
5.1 Muhtasari wa Utafiti .....	121
5.2 Matokeo ya Utafiti kuhusu kazi za Walibora .....	123
5.3 Matatizo ya Utafiti .....	128
5.4 Mchango .....	129
5.5 Mapendekezo .....	130
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>131</b>

## SHUKRANI

Mwanzo kabisa natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na afya ya kusoma na kukamilisha utafiti huu. Hakuna jambo ambalo ningeweza kutekeleza kama si kwa majaliwa yake mwenyewe Allah, muumba wa mbingu na ardhi.

Pili, nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Dkt. Clara Momanyi kwa mwongozo na ushauri wao mwafaka katika kila hatua ya utafiti huu.

Nawashukuru wahadhiri wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika wa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa mawaidha yao yaliyonifaa sana nilipokuwa nikitafiti. Shukrani zangu za kipekee ziwaendee Bw. Peter Mugambi, Bi. Mudhune, Dkt. Pamela Mathooko na Dkt. Onyango kwa kunipa moyo wa kuendelea na utafiti hasa pale nilipohisi nimelemewa.

Namshukuru mke wangu, Bi. Lilian Maridhia kwa kunitia moyo na kujaza pale nilipopungukiwa kwa hali na mali wakati nilipokuwa nikisoma. Siwezi kuwasahau watoto wangu Ahmed, Seif na Yasin ambao walivumilia kutokuweco kwangu na shauku yao ya kutaka kuona hatima ya kazi hii.

Pia nawashukuru ndugu zangu, Harun, Shaaban, Fatuma na Zainabu kwa mchango wao wa hali na mali na kwa kunihimiza kuendelea na masomo yangu. Mbali na hawa, natoa shukrani kwa wanafunzi wenzangu tulioshiriki nao katika masomo ya shahada hii kwa michango yao iliyonifaa wakati wa

kusoma na kutafiti. Hasa siwezi kuwasahau James Wanyela, Bakari Mohamed, Simiyu Wanjala na Mary Malenya kwa kunihimiza kuendelea na safari hii ya usomi.

Namshukuru vile vile Maalim Iddi Harun Musa kwa mchango wake wa kipekee wakati wa masomo na utafiti wangu. Ninawashukuru walimu wenzangu wa shule ya Nangina, Denis Makokha, David Wakhanu na Susan Odonde kwa mema waliyonifanyia.

Mwisho, natoa shukrani zangu kwa Bi. Sheila Ozengo kwa kujitolea kuipiga chapa tasnifu hii licha ya vikwazo mbalimbali vilivyokuwa vikitokea. Shukrani pia ziwaendee wengine wote ambao walichangia kwa namna moja au nyingine katika ufanisi wa tasnifu hii.

## IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia maigizo kama mbinu ya maudhui katika riwaya mbili za Ken Walibora. Riwaya zilizoshughulikwa ni *Ndoto ya Amerika*, (2001) na *Kufa Kuzikana*, (2003). Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto za uhalisia na uigizaji. Nadharia hizi zilifaa katika utafiti huu hasa ikizingatiwa ya kwamba riwaya zilizotafitiwa zimesheheni matukio mengi ambayo yanaakisi mambo yanayotokea katika maisha ya kawaida.

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa riwaya za Walibora zilizotafitiwa zina sifa za kitamthilia. Mwandishi ametumia mbinu mahsusi za maigizo ambazo zimezifanya riwaya hizi kubainika kama tamthilia.

Kwanza, mwandishi amewashirikisha wahusika wake zaidi katika kutenda na kusema, kuliko kusema pekee. Vitendo vyao vimeandamana na mazungumzo. Haya yanaonekana kupitia wahusika kama Isaya, Madoa na 'Rock Mwamba' au Zablun Okutoyi katika *Ndoto ya Amerika* (2001); na Akida, Tim na Tamari katika *Kufa Kuzikana* (2003).

Utafiti pia umebainisha kuwa katika kuzifanya riwaya zake zibainike kama tamthilia, Walibora amewafanya wahusika wake wote kuwa binadamu halisi wanaowasiliana moja kwa moja. Jambo hili limeyapa masimulizi yake uhai na uhalisi zaidi kiasi cha kuonekana kama maigizo.

Katika matukio mengi, mwandishi amewafanya wahusika wake wawasiliane wakitumia wakati uliopo, jambo ambalo linatoa taswira ya uigizaji. Kupitia utafiti, imebainika pia kuwa riwaya za Walibora zilizotafitiwa zimebeba wahusika wa kila umri na jinsia; hili ni jambo la kawaida katika maisha halisi kwa sababu linaakisi hali inayopatikana katika maisha ya kila siku; na maisha ni maigizo.

Utafiti pia umebainisha kuwa mwandishi ametumia mabadiliko ya mandhari katika riwaya zilizohakikiwa ili kujenga taswira ya uigizaji. Mandhari yamebadilishwa ili kuafiki mada iliyohusishwa katika mazungumzo baina ya wahusika. Kupitia riwaya hizi, kuna mandhari ya shule, ofisi, mahakama, sokoni na hata kituo cha polisi. Hili ni sawa na jukwaa ambalo hupatikana katika maigizo. Kubadilika kwa mandhari kila mara kunaweza kukamithilishwa na mabadiliko yanayotokea jukwaani katika michezo ya kuigiza ili kuashiria kumalizika kwa onyesho moja na kuanza kwa onyesho lingine.

Utafiti umebainisha vile vile kuwa maudhui yanayoshughulikiwa katika kazi za Walibora yamechangia pakubwa kuzifanya zikaonekana kama maigizo. Maudhui ya uhalifu, ukabila, ubinafsi na ukatili yamewasilishwa kwa hadhira kupitia maigizo ya moja kwa moja ya wahusika mbalimbali.

Utafiti huu utakuwa na mchango ufuatao; kwanza, umetuonyesha kuwa inafaa tuwe na mtazamo tofauti na vigezo vingine vya kuzihakiki riwaya badala ya kuselelea katika mitazamo ya kijadi iliyokuwa ikichukulia riwaya kama

utanzu mahsusi unaojitosheleza. Kupitia utafiti huu, imebainika kuwa riwaya za Walibora zilizotafitiwa zina pia sifa za kitamthilia.

Mchango mwingine ni kuwa, baada ya utafiti, imebainika kuwa riwaya yoyote inaweza pia ikawa na sifa za kitamthilia kama ilivyobainika katika riwaya za Walibora zilizotafitiwa.

Utafiti huu pia ni miongoni mwa kazi chache ambazo zimewahi kuhakiki baadhi ya kazi za Walibora kwa mtazamo tofauti. Kazi hizo zimehakikiwa kama zinazobeba sifa mseto za tanzu mbalimbali na kutofautiana na mitazamo ya awali iliyochukulia tanzu tofauti za fasihi andishi kama zinazojitosheleza.

Kwa hivyo, utafiti huu utawapatia wasomi wengine wa kazi za fasihi ya Kiswahili barabara tofauti za kufuata wakiwa katika safari ya kusaka mengi zaidi katika taaluma hii.

## UFAFANUZI WA ISTILAHU

**Kijiriwaya:** Ni kazi ya sanaa ya kubuni. Ni maandishi ya nathari (ujazo) yanayosimulia hadithi ambayo kwa kawaida haina upana, uzito na urefu kama wa riwaya. Ina wahusika wachache na migogoro michache kuliko riwaya, (Fasiri yetu).

**Maigizo:** Ni ile hali ya kuiga mfuatizo wa maneno au matendo ya watu wengine. Kuigiza ni kule kufanya na kusema kama vile mtu mwingine alivyofanya. Katika maigizo, matendo hupewa umuhimu mkubwa, (King'ei, 2005). Katika utafiti huu, neno hili limetumiwa kumaanisha hali ya mhusika kueleza ujumbe wake kupitia maneno yanayoambatana na vitendo.

**Maudhui:** Ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Maudhui hujibu swali la nini kazi ya kifasihi inazungumzia (Msokile, 1993).

**Nadharia Mseto:** Hii ni nadharia inayohusisha sifa na mihimili ya nadharia tofauti ili ifanye kazi pamoja. Utafiti huu umeongozwa na nadharia hii kama dira ya kuhakiki vitabu teule vya Walibora.

**Riwaya:** Ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo ina visa na vitushi, migogoro na husimulia mambo yanayohusiana na jamii. Kwa kawaida huwa na uzito, upana na urefu wa kutosha. Huwa na wahusika mbalimbali wenye tabia za aina nyingi na huwa na migogoro mingi mikubwa na midogo ndani yake. (Msokile, 1993).

Uhakiki: Ni sanaa au sayansi ya uchambuzi wa kifasihi kwa nia ya kubainisha  
visehemu vyake, kufasiri, kutenganisha, kutathmini na kutolea hukumu kazi  
ya fasihi. (Wamitila, 2003).

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Maana pana ya Fasihi ni kitu kilichoandikwa. Fasihi pia ni kazi za kisanaa zinazotumia lugha kwa usanii na zinazowasilisha suala fulani pamoja kwa njia inayoathiri, kugusa na kuacha athari fulani na kuonyesha ubunilizi na ubunifu fulani na zinazomhusu binadamu. Kazi hizi huweza kuwasilishwa kwa mdomo au kimaandishi, (Wamitila, 2003).

Riwaya ni mojawapo ya tanzu tatu kuu za fasihi andishi, zingine zikiwa tamthilia na ushairi. Katika enzi zilizopita, kumekuwa na mtindo wa kuhakiki tanzu hizi tatu za Fasihi Andishi kama zilivyoandikwa na aghalabu huwa zinachukuliwa kama tanzu zenye sifa mahsusi tofauti zinazobainika na kutofautiana na tanzu zingine.

Utafiti huu ulinua kuhakiki utanzu wa riwaya kama unaoweza kumiliki sifa fulani za kimaigizo au kitamthilia na kubainisha namna maigizo hayo yanavyoweza kutumiwa na mwandishi wa riwaya katika kuelezea maudhui ya kazi zake.

Kazi za kinathari ambazo zimetafitiwa ni za Walibora, *Ndoto ya Amerika* (2001) na *Kufa Kuzikana* (2003). Utafiti umelenga kubainisha sifa za kimaigizo zilizomo na namna sifa hizo zinavyoweza kufanya maudhui ya mwandishi kueleweka kwa urahisi kupitia maneno na vitendo kuliko masimulizi pekee.

Okutoyi au 'Rock Mwamba' kwa jina la kupanga. Namasake anafungwa jela kwa miaka mitatu, Isaya anaachiliwa na Okutoyi anauliwa anapojaribu kumpokonya askari-jela bunduki.

*Kufa Kuzikana* (2003) ni riwaya inayoangazia athari za ukabila katika nchi ya Kiwachema. Katika eneo la Baraki wilayani Korosho, vita vinazuka kati ya Wakanju na Wakorosho kutokana na uchochezi wa viongozi. Watu wanauliwa na nyumba na mali kuteketezwa. Serikali inaunda tume ya kuchunguza chanzo cha vita hivyo, lakini ukweli halisi haubainiki.

Kazi hizi za Walibora na nyinginezo zimehakikiwa kama maandishi ya kinathari na miongoni mwa waliohakiki kazi kama riwaya au vijiriwaya ni Kairu (2005). Utafiti wa Kairu ulihakiki uhalisi na mtindo wa Walibora katika vijiriwaya vya watoto. Vijiriwaya alivyotafitia ni *Ndoto ya Amerika* (2001), *Mgomba Changaraweni* (2003), na *Mtu wa Mvua* (2003). Tanzu hizi hazikuangaliwa kama tanzu zinazoweza kushirikisha uigizaji. Utafiti huu unalenga kutoa mtazamo tofauti wa kuziangalia kazi za Walibora.

### **1.1 Swala la Utafiti**

Utafiti huu umekusudia kubainisha matumizi ya maigizo katika hadithi za Walibora na jinsi maigizo au mitindo mbalimbali ya tamthilia inavyotumiwa na mwandishi huyu kuyatolea maudhui yake na kwa njia hiyo kuyafanya yaeleweke vizuri zaidi.

Utafiti huu umenuia kuonyesha mbinu anazotumia Walibora katika kuwahusisha wahusika wake katika vitendo kwa kiasi cha kuvifanya vitendo vibainike zaidi kama maigizo kuliko masimulizi.

Vile vile Walibora ametumia mbinu mahsusi na kwa njia maalum ili anayesoma kazi zake aweze kung'amua kuwa kazi hizo zinabainika zaidi kama maigizo kuliko masimulizi. Inawezekana kuwa Walibora ametumia fani iliyofanya masimulizi yake yabainike zaidi kama maigizo kuliko masimulizi.

## **1.2 Nadharia Tete**

Nadharia tete zifuatazo zitaongoza utafiti huu. Ingawa riwaya za Walibora ni masimulizi, masimulizi hayo yamebainika zaidi kama tanzu za kuigizwa kuliko tanzu za kuelezwa moja kwa moja kinathari.

- (i) Walibora anatumia mbinu mahsusi za kisanii ili riwaya zake zidhihirike kama kazi zinazoweza kuigizwa zaidi kuliko kazi za kusimulia.
- (ii) Ubunifu wa riwaya za Walibora kama maigizo unatokana na maudhui anayozungumzia.

## **1.3 Malengo ya Utafiti**

- (i) Utafiti huu unanua kuainisha sifa zinazozifanya riwaya za Walibora kubainika zaidi kama maigizo kuliko kama masimulizi ya kinathari.
- (ii) Kuchunguza ikiwa maudhui ya riwaya za Walibora yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuyafanya masimulizi yake yawe kama maigizo.

(iii) Utafiti huu pia unalenga kuonyesha ya kwamba riwaya za Walibora ni mifano mahsusi ya mwingiliano kati ya sifa za riwaya na sifa za tamthilia.

#### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mshawasha wa kushughulikia mada hii umetokana na sababu kadha. Sababu ya kwanza ni kwamba licha ya kuwa na waandishi wengi katika fasihi ya Kiswahili, wengi wao wameshughulikia tanzu mbalimbali kama riwaya, tamthilia na ushairi kama zinazojitosheleza. Tanzu hizi tofauti pia zimepewa sifa mahsusi zinazozitofautisha na tanzu zingine.

Ukweli ni kwamba sifa hizi si za kudumu kwa sababu utanzu mmoja unaweza ukashirikisha mwingine kama inavyobainika katika riwaya nyingi duniani zilizotumika kutengeneza filamu. Mifano ya riwaya hizo ni kama *Shujaa Okonkwo* (Achebe, 1979) na *Carcase for Hounds* (Mwangi, 1974). Pia baadhi ya riwaya za Kimagharibi zilizowekwa katika sura ya filamu ni kama *Anna Karenina* (Tolstoy 1949); *Emma* (Austen, 1966) na *Far from the Madding Crowd* (Hardy, 1974). Mchezo wa kuigiza pia unaweza ukageuzwa na ukawa riwaya. Riwaya ya *Usiniharakishe* (Ngweno 2005) ilikuwa awali mchezo ulioigizwa kwenye runinga nchini Kenya. Kwa hivyo utafiti huu umeazimia kubainisha kuwa masimulizi yanaweza kuingiliana na maigizo. Tunaamini kuwa sifa za uigizaji zinapatikana katika riwaya za Walibora na zinahitaji kutafitiwa. Utafiti pia umelenga kuona iwapo riwaya za Kiswahili zinaweza kuwa na sifa za kuigizwa kama zilivyo riwaya za tamaduni zingine.

Sababu nyingine ni kuwa ingawa kumefanyika utafiti wa riwaya za Kiswahili hapo awali, utafiti huo ulichukulia kuwa riwaya imejitosheleza na inaweza kujisimamia. Utafiti huu unalenga kwingine, ambako ni kuonyesha kuwa baadhi ya riwaya zaweza kubainika na kueleweka zaidi kwa sifa za kimaigizo kuliko za kimasimulizi.

Walibora ni mwandishi chipukizi aliyeandika riwaya, hadithi fupi na vijiriwaya kadha. Kazi hizi zapaswa kuhakikiwa kwa jicho tofauti na kwa njia hiyo, tunasadiki zitapewa nafasi zinazostahili katika fasihi ya Kiswahili na kuendeleza taaluma hii kwa kuwapa waandishi na wahakiki fursa ya kuzishughulikia kazi za kifasihi kama zenye tanzu mseto.

### 1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia kazi mbili za Walibora; kijiriwaya cha *Ndoto ya Amerika* (2001) na riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003). Kazi zingine za mwandishi huyu zimeangaliwa katika kutoa mchango kwa utafiti huu. Hata hivyo, kutokana na usomaji wa awali, *Ndoto ya Amerika* (2001) na *Kufa Kuzikana* (2003) ni kazi zilizoonyesha mwelekeo wa kuibua data zilizofungamana na swala letu la utafiti. Riwaya hizi mbili zilichaguliwa pia kwa sababu zina sura za kuigizika zaidi na kwa sifa hizo kuwezesha maudhui yazo kuonekana na kueleweka kwa usahili zaidi.

Utafiti huu umechagua kuangalia kazi za Walibora kwa sababu kazi hizo ziliandikwa miaka michache iliyopita na zinagusia maudhui yanayopatikana katika mazingira yetu ya sasa.

Kazi za Walibora pia zimechaguliwa kwa sababu akiwa mmoja kati ya waandishi wenyeji wa Kenya, kuna uwezekano kuwa yanayopatikana katika kazi zake yanatokana na tajriba yake na kwa njia hii hadhira yake inaweza ikaelewa kwa urahisi.

Akiwa mmoja wa waandishi chipukizi na maarufu nchini, Walibora hajafanyiwa utafiti mwingi kama walivyofanyiwa waandishi wengine. Kwa sababu hii, utafiti huu umeangazia kazi zake ili kuongezea kwa ule mchache ambao umefanywa.

## **1.6 Misingi ya Nadharia**

Katika utafiti huu nadharia ya uhalisia imetumiwa pamoja na nadharia ya uigizaji. Hii ni kwa sababu nadharia hizi zinachukuana vizuri na swala la utafiti na lengo la utafiti.

### **1.6.1 Uhalisia Kama Nadharia ya Uhakiki**

Uhalisia ni mkondo unaosisitiza usanii wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Neno 'uhalisia' lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika mwaka wa 1850 ili kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa. Kama nadharia ya uhakiki, uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Jinsi ya kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika msingi huu, inawezekana kusema kuwa kila kizazi huwa na 'uhalisia' wake.

Kazi hii ya uhalisia iliwekewa msingi na mwana falsafa Hegel katika kitabu chake kilichojulikana kama '*Aesthetik*'. Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo. Uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hivi kwamba haiwezekani kuzungumzia riwaya bila ya kuyarejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia.

Nadharia hii husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake. Katika mtazamo wa uhalisia, yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi. Mwanasanaa katika misingi ya kihalisia anapaswa kuelewa ulimwengu wake kama kitu changamano na kinachobadilika. Mwandishi wa kiuhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na pia huyaakisi maisha katika ngazi za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Mchango mkubwa wa nadharia hii ni kuchora maisha kama yalivyo.

Larkin (1972:2), anasema kuwa wanauhalisia waliamini kuwa madhumuni ya mwandishi kwa jamii ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba ulimwengu atakaoumba mwandishi sharti uwe wa kweli au halisi.

Kulingana na Lukacs (1972:6) nadharia ya uhalisia ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi za sanaa na mtazamo wa msanii kuhusu mazingira aliyomo.

Lengo letu la kutumia nadharia hii ni kuihakiki kazi ya msanii ili kuona ni kwa kiasi gani anadhihirisha uhalisia na umuhimu wake katika fasihi ya Kiswahili.

Uhalisia ni njia ya uhakiki inayozingatia muundo na muwala na huchukua kazi ya fasihi kama zao linalojitosheleza. Njia hii huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Mhakiki humchambua mwandishi kwa namna mwandishi huyo anavyojibidiisha kuudhihirisha ukweli. Hapa mwandishi anapaswa kutoa picha ya jamii na hivyo kuwa kama kurunzi ya jamii. Jukumu la msanii linafaa kuwa la ukweli na linafaa kudhihirisha ukweli ili kujaribu kuufikia uhalisia. Msanii anafaa kutumia kipawa chake kuchora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake kwa sababu mazingira haya huwa na uhalisi unaoaminika.

### **1.6.2 Mihimili ya Uhalisia**

- (i) Msanii huandika kuhusu maisha yalivyo pasipo kuathiriwa. Kazi katika misingi ya kihalisia huangazia maisha katika ngazi zote, za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kijamii na kadhalika.
- (ii) Wahusika katika sanaa za kihalisia husawiriwa wakiwa wa kawaida na wakiwakilisha jamii zao. Ukweli unafaa uonekane katika kuwaamba wahusika wa kawaida katika mandhari ya kawaida. Msanii wa kihalisia huwapata wahusika wake katika jamii yake iliyo ya kawaida na inayojulikana.
- (iii) Lugha katika kazi za kihalisia huwa ni ya kawaida na wahusika huitumia kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu.

- (iv) Mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana. Maudhui na matukio kwa kiasi kikubwa yanatakiwa kulingana na yale ya jamii inayorejelewa.
- (v) Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Yeye huchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika kipindi fulani cha historia na namna ambavyo mabadiliko hayo husababisha hali mbalimbali. Hivyo basi, mwandishi wa kihalisia hutilia maanani mabadiliko ambayo yanatokea ili aweze kuwasawiri wahusika wake.

Utafiti huu umetumia uhalisia kuhakiki vitabu vya Walibora kama kazi zenye tanzu mseto.

### **1.6.3 Nadharia ya Uigizaji**

*Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia* (2003) inaeleza uigizaji kuwa ni ufundi na ujuzi wa kuiwasilisha au kutenda kazi za sanaa inayotegemea kuyaiga matendo fulani na kuyawasilisha kwenye jukwaa mbele ya hadhira fulani.

Kamusi hiyo pia inafasili maigizo kama dhana inayotumiwa kuelezea utanzu mmojawapo wa Fasihi Simulizi. Maigizo huhusisha uwasilishaji wa tungo mbele ya hadhira na huambatana na utendaji au uigizaji. Maigizo yana vipera vingine kama ngonjera, michezo ya jukwaani, majigambo, vichekesho au sarakasi.

Kwa mujibu wa Bauman (1992), maigizo ni hulka na pia ni tukio la mawasiliano au kuwasiliana. Anasema kuwa ingawa istilahi hii yaweza kutumiwa kwa njia ya kiuajumi kuelezea tukio halisi la mawasiliano na siyo uwezekano wa tendo la mawasiliano, maigizo aghalabu hurejelea hali ya kuwasiliana na hadhira kupitia jukwaa kwa njia inayovutia na kuiteka hisia hadhira hiyo. Anaongezea kuwa kupitia maigizo, tunaweza kugundua vitengo vya kijamii, kitamaduni na vya kiuajumi vya tukio la mawasiliano.

Katika sanaa za uigizaji, Bauman (1992), anasema kuwa tofauti kati ya uigizaji hali na uwezekano wa uigizaji huonekana tunapolinganisha miswada au miongozo inayoandaliwa kwa ajili ya uigizaji wa kisanaa kama vile miswada ya muziki ama mchezo wa kuigiza na uigizaji halisi wa kazi hizo mbele ya hadhira. Anasema hili huwezekana kwa kufasiri ujumbe kutoka njia moja ya mawasiliano hadi nyingine, mathalan, kugeuza uigizaji kuwa uandishi ama masimulizi kugeuzwa na kuwa maandishi.

Bauman (1992) anasema kuwa miongoni mwa mambo muhimu yanayoashiria uigizaji ni vitu kama jukwaa lililoinuliwa na mambo yanayotokea katika msimu au wakati fulani kama sherehe. Pia anaeleza kuwa maigizo yote hupatikana, hutokea na huthaminiwa kwa mujibu wa muktadha wa kijamii unaohusika.

Bauman anaeleza kuwa miongoni mwa maigizo yanayothaminiwa ni maigizo ya kitamaduni na haya huwa na sifa fulani mahsusi:

- (i) Matukio haya huandaliwa mapema kabla ya wakati wake wa kuigizwa.
- (ii) Huwa na mwanzo na mwisho maalumu au unaotambulika.
- (iii) Hutendwa katika sehemu maalum iliyotengwa mahsusi kwa shughuli hiyo. Sehemu hiyo inaweza kutengwa kwa muda mfupi au milele. Mifano ya sehemu hizo ni kama ukumbi wa maonyesho, uwanja wa sherehe au kijisitu kinachoheshimiwa.
- (iv) Maigizo ya kitamaduni huwa na ratiba maalumu inayoonyesha mfuatano wa matukio.
- (v) Huwa ni matukio ya hadhara yaliyopangwa na yanayotazamwa na hadhira pia hutoa fursa kwa washiriki kukutana na kudhihirisha vipawa vyao.

Bauman (1992) pia anaeleza kuwa hali ya mwigizaji hupenya katika hisia za hadhira yake. Haijifungi tu katika maigizo ya kitamaduni bali pia huonekana katika miktadha mingine ya kijamii kama vile mtu anapopigwa picha akitenda jambo la fadhila. Anahitimisha kwa kusema kuwa tutazamapo maigizo kisanii (na siyo kwa upana wa maisha yote kwa jumla kama maigizo), itabainika kuwa kaida za uigizaji zitakuwa zimefinyangwa pamoja ili kutumikia maana finyu ya kisanaa.

Kuigiza ni kumithilisha. Kwa kuwa umithilishaji huvihusu vitendo, maigizo ni aina ya sanaa-tendaji. Asili ya vitendo kulingana na Traore (1972:11) ni tajriba zinazojitokeza binadamu anapoyakabili maisha katika mazingira anamoishi. Kwa hivyo inambidi mwigizaji kufanya upekuzi wa hali anazomithilisha ili

kuwasilisha ukweli wa maisha kwa usahihi unaofaa kwa misingi ya umbuji wa sanaa ya uigizaji.

Ulazima huu hutakikana ili kumwezesha mtendaji kuzisawiri hali tofauti katika maisha ya binadamu na anavyobadilikabadilika kitabia katika mazingira na miktadha mbalimbali maishani. Ufinyanzi wa vitendo na mnasaba kati ya vitendo na sauti katika uigizaji hutegemea ubunifu wa mtendaji. Mwili pamoja na sauti ya mwigizaji hutumika kuujenga ujumbe na kusababisha hisia zinazodhamiriwa kuiathiri hadhira.

Aina ya uigizaji ulio maarufu aghalabu huambatanisha utendaji unaohusisha mwili na utoaji sauti. Kuna utendaji-bubu pia. Huu hutendwa bila kutolewa sauti. Aina ya kwanza ndiyo hutambuliwa zaidi kama utendaji. Robinson (1980:150) amedokeza kuwa hapana uigizaji ambao hauna nia ya kuwasiliana au kuishawishi hadhira kuuzingatia. Ufanisi wa uigizaji huangaliwa kwa jinsi ulivyofanikisha mawasiliano. Goodland (1971) anadokeza kuwa maigizo yanaweza kuihudumia jamii kwa kuuendeleza utamaduni wake, kudumisha mifumo ya kijamii na zaidi kuifahamisha jamii kuhusu maswala mbalimbali.

Akijadili dhana ya maigizo kabla ya ukoloni nchini Kenya, Ngugi anasema:

“Maigizo .... hayakuwa shughuli iliyojitenga, yalikuwa kiungo mojawapo cha maisha ya kila siku yaliyofuata mkondo wa majira katika jamii. Mbali na kuwa aina ya burudani, yalikuwa njia ya kufunzia na pia shughuli iliyochukuliwa kwa dhati kama njia mojawapo ya kuyaendeleza maisha ya jamii.”

(Ngugi 1986:37) (Tafsiri ya mtafiti).

#### **1.6.4 Mihimili ya Nadharia ya Uigizaji**

Kwa ufupi nadharia hii huwa na mihimili ifuatayo:

- (i) Uigizaji wafaa kueleza ukweli wa maisha kwa usahihi unaofaa. Mtendaji lazima azisawiri hali tofauti maishani mwa binadamu na jinsi anavyobadilika kitabia kutegemea mazingira na miktadha tofauti.
- (ii) Uigizaji unaomshirikisha mtendaji aliye hai huwa na ufanisi mkubwa kwa sababu mtendaji huyo anaweza kufaragua vitendo vyake ili kukidhi matakwa ya hadhira yake.
- (iii) Kila uigizaji sharti uishawishi hadhira kuuzingatia na ni kwa njia hiyo tu ambapo utafanikisha mawasiliano.
- (iv) Uigizaji wafaa kuihudumia jamii, kwa kuendeleza utamaduni wake, kuidumisha mifumo ya kijamii na kuifahamisha jamii kuhusu maswala ya aina mbalimbali.

Katika maandishi ya kinathari, ni wahakiki wachache waliotumia nadharia ya uigizaji kuzihakikia kazi zao. Walioitumia nadharia hii wameangazia zaidi tamthilia. Utafiti huu unalenga kutumia uigizaji kuhakikia riwaya kwa sababu tunaamini kuwa pana ombwe linalofaa kujazwa kwa kutumia mkabala tofauti wa kuangalia riwaya za Walibora.

#### **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Ingawa utafiti ulishafanywa kuhusu riwaya za Kiswahili hapo awali, utafiti huo ulilenga mambo tofauti. Miongoni mwa kazi zilizohakiki riwaya ni kama ile ya Kamau (1992) aliyechunguza ufundi katika riwaya za Mohamed S. Abdullah. Anaye (2004) alitafiti juu ya namna hadithi zilivyotumiwa kama

chombo cha maudhui katika riwaya za Mkangi na Magaju (2004) akatafitia uhalisiajabu katika riwaya *Babu Alipofufuka* (Mohamed, S. A. 2001) na *Binadamu* (Wamitila, 2002).

Utafiti huu unatofautiana na kazi hii kwa sababu kwanza, kazi hizo zilitafiti riwaya kama utanzu huru na unaojitosheleza ilhali huu umelenga kujaza pengo lililoachwa kwa kutafiti riwaya kama utanzu mseto unaoweza kuwa na sifa za kimaigizo au za kitamthilia.

Pili, utafiti huu unatofautiana na kazi hizo za awali kwa sababu baadhi ya kazi hizo ziliangalia namna maudhui yalivyojitokeza katika riwaya kwa njia ya masimulizi. Utafiti huu umenuia kuuajaza mwanya ulioachwa na kazi za awali kwa kuchunguza jinsi maudhui yanavyojitokeza katika riwaya kupitia maneno na vitendo na sio kwa maneno pekee.

Kazi zingine zinazokaribiana na utafiti huu ni ya Gituku (1990). Yeye alishughulikia maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya na dhima yake katika ufundishaji. Utafiti huu unakaribiana na wa Gituku kwa sababu kazi zote zinashughulikia maigizo. Tofauti ni kuwa kazi ya Gituku ilishughulikia maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya ilhali utafiti huu utashughulikia maigizo katika riwaya. Pili, utafiti wa Gituku haukuhusisha maigizo na kazi zozote maalumu jinsi ambavyo utafiti huu unatazamia kufanya.

Miongoni mwa walioshughulikia kazi zilizoigizwa moja kwa moja ni Mule (1991) aliyezungumzia swala la mwanamke katika tamthilia za Kiswahili

zilizandikwa na wanawake. Mwingine ni Mahero (1992) aliyetafitia swala la uongozi katika tamthilia za Chacha N. Chacha.

Utafiti unaokaribiana na huu zaidi ni ule wa Kairu (2005). Utafiti wake ulimulika uhalisi na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Vitabu alivyoshughulikia ni *Ndoto ya Amerika* (2001) *Mgomba Changaraweni* (2003) na *Mtu wa Mvua* (2003). Kairu (2005) aliangalia vitabu hivi kama vinavyoafiki mahitaji ya kusoma ya watoto na kwa kigezo cha ufupi wavyo aliviita fasihi ya watoto. Utafiti huu unakaribiana na wa Kairu kwa sababu kazi zote zinashughulikia maandishi ya Ken Walibora. Tofauti ni kuwa Kairu aliangalia uhalisi na mtindo wa Walibora katika vijiriyawa vitatu ilhali utafiti huu umeazimia kuchunguza maigizo katika kazi mbili za Ken Walibora.

Utafiti wa Kairu japo uliangalia vitabu vya Walibora, ulilenga mambo tofauti na yale yanayotafitiwa katika kazi hii, nayo ni jinsi Walibora alivyotumia uigizaji katika kuyaelezea maudhui kwa misingi ya uhalisia na uigizaji.

Mbughuni (1978) alionyesha jinsi masimulizi ya hadithi yalivyotumiwa kutoa maudhui. Alitoa mifano ya kazi za Shaaban Robert, *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1961), *Siku ya Watenzi Wote* (1968) na *Adili na Nduguze* (1951). Hizi ni kazi za fasihi andishi zilizojengeka katika fasihi simulizi. Utafiti wa Mbughuni unatoa changamoto ya kutazama mwandishi mwingine wa riwaya, naye ni Walibora.

Kathleen Greenfield katika Cantalupo C. (1995:38) alitumia hadithi ya talanta kuonyesha namna waliopewa vipawa tofauti walivyotumia kunyanyasa jamii. Hadithi hii ina msingi wake katika hadithi iliyotolewa na Yesu Kristo (Luka 19:11-26) kuhusu ugawaji wa vipawa katika *Agano Jipya*. Mwandishi anasema, 'Mfanyakazi aliyepewa shilingi laki moja alifukia zake chini kwa sababu pesa haziwezi kuongezeka bila kunyonya jasho la wafanyakazi'.

Utafiti huu unakaribiana na huu kwa vile unachunguza jinsi lugha na masimulizi yalivyotumika kutolea hadithi. Hata hivyo, unatofautiana na huu kwa sababu unatazamia kuangalia jinsi maigizo yaliyotumiwa na Walibora kuelezea maudhui yanavyokamilishana na uhalisia.

Kutokana na kupitia yale yaliyoandikwa juu ya mada hii, imeonekana kuwa hakuna utafiti au ni utafiti mchache uliofanywa kuhusu jinsi maigizo na masimulizi yanavyochangiana katika kuelezea uhalisia wa maudhui.

## **1.8 Mbinu za Utafiti**

Ukusanyaji wa data ulifanyika maktabani kwa kusoma kazi mbili za Walibora, *Ndoto ya Amerika* (2001) na *Kufa Kuzikana* (2003). Kazi zingine za Walibora zilisomwa ili kuona jinsi zilivyoweza kuchangia mada ya utafiti. Tasnifu na kazi zingine zinazohusiana na mada hii pia zilisomwa na yaliyo muhimu kunakiliwa. Makala ya kifasihi, majarida na magazeti ambayo yangesaidia katika utafiti huu kwa njia mbalimbali pia yalisomwa na yaliyo muhimu kunakiliwa.

### 1.8.1 Uchanganuzi wa Data

- (i) Kusoma kazi za mwandishi na za waandishi wengine juu ya kazi za Walibora ili kupata mwanga ufaao kwa utafiti.
- (ii) Data iliyokusanywa ikachanganuliwa kwa kuangalia yaliyo muhimu kutokana na usomaji wa vitabu, tasnifu, majarida na magazeti.
- (iii) Riwaya ya *Kufa Kuzikana* na kijiriwaya cha *Ndoto ya Amerika* zilisomwa kwa lengo la kuainisha na kudondoa sehemu zake za masimulizi yanayojidhihirisha kuwa maigizo.
- (iv) Sehemu hizo zilihakikiwa kwa kuzingatia nadharia ya uhalisia na nadharia ya uigizaji.
- (v) Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kupitia kwa maandishi ya nathari.

### 1.9 Kiishilio

Katika sura ya kwanza, mtafiti ametoa ufafanuzi wa maswala kadhaa. Maswala na malengo ya utafiti yameelezwa pamoja na sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na pia uchanganuzi wa data vyote vimefafanuliwa. Sura inayofuata ni ya pili. Sura hii inazungumzia historia, usuli na kazi za Ken Walibora.

## SURA YA PILI

### HISTORIA, USULI NA KAZI ZA KEN WALIBORA

#### 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia historia, usuli na kazi za Ken Walibora na namna zilivyochangia mada hii ambayo ni maigizo na uhalisia katika riwaya za Walibora na jinsi maigizo yalivyotumiwa na mwandishi kutolea maudhui yake.

Kazi hizo nyingine za Walibora zilijadiliwa kwa ufupi kwa sababu ya kutoa mwangaza zaidi juu ya kazi zinazotafitiwa katika tasnifu hii ambazo ni *Ndoto ya Amerika* (2001) na *Kufa Kuzikana* (2003).

Wellek na Warren (1979) wanasema kuwa sababu kuu ya kazi yoyote ya sanaa kuwapo ni msanifu au muumbaji wa kazi hiyo, mathalani mwandishi na kwa sababu hii, njia mojawapo ya tangu jadi na mwafaka zaidi ya kuhakiki kazi za kisanii ni kuanza kwa kueleza wasifu na historia ya mwandishi anayehusika.

Wasifu wa msanii wa kazi fulani ni muhimu kwa sababu hutuangazia zaidi kumhusu msanii kama huyo na tajiriba zake na kwa njia hii, huweza kurahisisha kazi ya kuhakiki kazi zake. Wanasema pia kuwa kuelewa historia na maisha ya msanii hurahisisha kueleza kazi zake kwa kiasi fulani.

Wellek na Warren (1979) wanasema pia kuwa iwapo wasifu wa msanii fulani utafanana kwa kiasi kikubwa na kazi za sanaa hiyo yake, basi kazi hiyo huwa

ni kama nakala halisi ya maisha yake. Hii ni kwa sababu sanaa mbalimbali anazobuni hutokana na tajiriba yake inayobadilika kila mara kutokana na mapisi ya wakati.

Wellek na Warren (1949) wanaeleza pia kuwa wakati mwingine, sanaa ya msanii fulani huweza kutumiwa kutoa picha tofauti kabisa na wasifu au maisha yake halisi. Wanatoa mfano kuwa kazi ya msanii na siyo maisha yake halisi; ndio inaweza ikatumiwa na msanii kama njia ya kusitiri wasifu wake halisi ama inaweza ikatupa picha halisi ya maisha ya msanii yasiyompendeza na ambayo angependa kuyaepuka.

Vile vile, Wellek na Warren (1949) wanasema kuwa msanii anaweza akaona maisha kwa njia tofauti kupitia kazi zake kwa sababu kazi kama hizo humfikia kupitia vigezo fulani na mambo yaliyowekwa na yanayofikiriwa kama ni kaida za fasihi zifaazo kuzingatiwa.

Wanahitimisha kwa kututahadharisha kuwa yafaa tuwe makini tunapochunguza wasifu wa msanii na kazi zake za sanaa kwa sababu wakati mwingine sanaa kama hizo haziwezi zikatumiwa kuandika wasifu wa msanii fulani. Pia wanasema kuwa hakuna ushahidi wowote wa wasifu wa msanii unaoweza ukaathiri namna kazi zake zinavyohakikiwa na kuwa ukweli katika maisha halisi ni tofauti na ukweli katika sanaa.

Hata hivyo, kutokana na umuhimuu wa historia na wasifu wa mwandishi katika fasihi kwa jumla na katika kutupa mwangaza wa kuelewa kazi za

wasanii, katika sura hii ya pili, utafiti huu umeeleza historia na wasifu wa Ken Walibora na pia kugusia baadhi ya kazi zake ili kupata taswira kamili ya kazi zake zilizohakikiwa katika utafiti huu.

## **2.1 Historia na Usuli wa Ken Walibora**

Ken Walibora ambaye jina lake halisi ni Kennedy Waliaula, alijibunia jina ‘Walibora’ kwa kuswahilisha jina lake la Kiluhya ‘Waliaula’. Alifanya hivyo kwa kulikata jina ‘Waliaula’ katika sehemu mbili, ‘Wali’ (mchele uliopikwa) na ‘Aula’ (kitu bora kabisa, adhimu) na akazua lakabu, ‘Walibora’.

Walibora alizaliwa katika mwaka wa 1965 wilayani Bungoma, mkoa wa Magharibi nchini Kenya na akakulia katika kijiji cha Sangura, tarafa ya Cherangani wilaya ya Trans Nzioa katika mkoa wa Bonde la Ufa. Yeye ni kitinda-mimba katika aila ya watoto watano, wavulana wanne na msichana mmoja.

Tajriba yake ya maisha alipokuwa mdogo ilichangia kwa kiasi kikubwa kazi ambazo alikuja akajiunga nazo baadaye maishani. Kwanza, akiwa mdogo, Walibora alikuwa na ndoto ya kuwa askari-polisi. Hii ilitokana na mambo aliyoyashuhudia akiwa mdogo. Mmoja kati ya jamaa zake wa familia yao pana alikuwa akimbughudhi na hata kuwakera wanakijiji wengine bila kujali wala kubali. Lakini siku moja, Walibora anasema kuwa polisi walifika kijijini na wakamtia mbaroni jamaa huyo. Siku hiyo, Walibora aliamua kuwa akiwa mtu mzima angekuwa askari-polisi. Alikuwa amevutiwa sana na kufurahishwa na kitendo cha polisi waliomshika mtu huyo msumbufu.

Lakini alipokuwa akipevuka, ndoto yake ya kudumisha sheria ilififia na badala yake akawa na hamu kubwa ya kuwa mtangazaji wa kandanda. Akiwa na umri wa miaka kumi, Walibora alitumia wakati wake mwingi akicheza kandanda ama akitazama vipindi vya runinga, katika ukumbi wa kijamii uliokuwa karibu. Vile vile alikuwa akisikiliza matangazo ya kandanda redioni ya wanahabari mashuhuri kama vile Leonard Mambo Mbotela, Abdul Ngalawa na Salim Mbonde. Hawa ni baadhi ya wahusika waliomvutia katika azma yake ya kuwa mwanahabari.

Akiwa kijana, Walibora alisafiri sehemu nyingi nchini Kenya katika harakati zake za kuridhisha kiu yake ya kupata elimu. Kwanza, alijiunga na shule ya msingi ya St. Joseph's mjini Kitale na baadaye akajiunga na shule ya upili ya Olkejuado wilayani Kajiado. Kutoka Olkejuado, Walibora alijiunga na shule ya upili ya Koelel, mjini Gilgil kwa masomo yake ya kidato cha tano na cha sita. Alipomaliza masomo ya kidato cha sita, Walibora alifundisha somo la Kiswahili katika shule ya upili ya Sitatunga katika wilaya ya Trans Nzoia na baadaye akajiunga na Taasisi ya Utawala ya Kenya (K.I.A) Kabete ambako alisomea masuala ya maendeleo ya kijamii. Akiwa mwanafunzi katika taasisi ya Kabete, Walibora alijaribu kwa mara ya kwanza umahiri wake katika utangazaji.

Wakati wa michezo ndiye aliyekuwa mtangazaji wa michezo mbalimbali ya Taasisi. Kwa sababu alikuwa pia mwana-michezo hodari, Walibora alihakikisha kwanza kuwa anakimbia na kuibuka mshindi katika riadha kabla ya kurukia jukwaa na kuendelea na utangazaji.

Walibora anasema kuwa hatamsahau daima mhadhiri wake mmoja katika taasisi ya Kabete kwa fadhila aliyomfanyia. Huyo alikuwa Bw. Philip Omoni, ambaye alihakikisha kuwa baada ya mafunzo yake, Walibora alitumwa kufanya kazi jijini Nairobi. Hili lilimpatia fursa ya kutimiza ndoto yake ya kuwa mtangazaji.

Kitaaluma, Walibora ni afisa wa kijamii anayehusika na urekebishaji wa tabia za wafungwa. Akiwa afisa wa kuchunguza mienendo ya wafungwa kwa miaka minane, Walibora alitumia wakati wake mwingi pamoja na wahalifu sugu katika baadhi ya magereza hatari nchini Kenya. Kwa wakati huo wote alijaribu kuelewa maisha ya wahalifu kama hao na wakati huo pia kujaribu kueleza mahakama picha halisi ya yale aliyogundua. Anasema kuwa kwa nyakati fulani, ripoti ambazo yeye na maafisa wengine walitoa kwa mahakama zilichangia katika hukumu ambayo ilitolewa. Alipokuwa katika Idara ya Magereza, masahibu wake walimkumbusha mara kwa mara kuwa nyota yake haikuwa katika idara hiyo, ila katika taaluma ya utangazaji.

Akiwa afisa wa magereza, Walibora alipata fursa ya kuandika kitabu chake cha kwanza, *Siku Njema* (1996) na mwaka wa 1997 kikateuliwa kuwa kimojawapo cha vitabu vya kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne nchini Kenya. Ushauri wa Walibora kwa yeyote ambaye angependa kujiunga na taaluma yoyote ni kuwa lazima uwe na bidii na uwe mvumilivu. Licha ya kuwa afisa wa kijamii ahusikaye na kazi ya kuchunguza tabia za wafungwa, Walibora anasema kuwa alijiunga na kazi ya utangazaji kwa sababu aliienzi sana.

Kuanzia mwaka wa 1987, na kwa miaka mitatu iliyofuata, Walibora alikuwa akilitumia Shirika la Utangazaji la Kenya (K.B.C) habari za michezo. Alifanya hivyo kupitia simu za umma na akilipia gharama hiyo kwa kipato chake kidogo wakati huo. Kati ya mwaka wa 1988 na 1996, Walibora alijaribu kujiunga kikamilifu na taaluma ya utangazaji, lakini juhudi zake hazikufua dafu. Kwa mfano, mwaka wa 1988, alijiunga na Shirika la Utangazaji la Kenya (K.B.C) kwa mafunzo yaliyohusiana na sauti ambapo aligundua changamoto nyingi zilizohusiana na utangazaji. Alifunzwa na watangazaji kama vile Willie Mwangi na Anderson Kalu na wakati wa mafunzo hayo, Walibora aliwapendeza walimu wake kwa sauti yake nzuri na kwa kipawa alichokuwa nacho. Lakini licha ya hayo yote, bado shirika la K.B.C halikumwajiri.

Mwaka wa 1990, Walibora aliomba ahamishwe kutoka jiji la Nairobi. Alikuwa amekata tamaa na alisadiki kuwa huenda pengine bahati yake haikuwa katika uwanja wa utangazaji. Kwa hivyo, alitaka awe mbali sana na ulimwengu ambao ulikuwa umemkataa. Mwaka huo wa 1990, aliamishiwa Nakuru alikofanya kazi kwa miaka minne kabla ya kuhamishiwa mjini Kitale. Akiwa bado katika Idara ya Magereza kama afisa wa kuchunguza na kutathmini tabia za wafungwa, Walibora aliendelea na uraibu wake wa kuandika miswada ya vitabu mbalimbali.

Ndoto ya Walibora kuwa mtangazaji kikamilifu ilikuja ikawa si ndoto tena bali ukweli halisi miaka sita baadaye katika mwaka wa 1996. Katika mwaka huo, Shirika la Utangazaji la Kenya (K.B.C) lilizindua stesheni ya redio

iliyoitwa 'Metro F.M. Radio'. Walibora alikata kauli ya kujaribu tena bahati yake katika taaluma ya utangazaji baada ya shirika la K.B.C. kunadi nafasi za wasomaji habari. Mkeke na dadake Walibora walimtia moyo wa kutuma maombi ya kuajiriwa na alipofanya hivyo, akabahatika kuwa miongoni mwa watu wachache walioajiriwa miongoni mwa maelfu ambao waliomba kazi hiyo.

Walibora anasema kuwa hakuwa mraibu wa muziki ila wa taarabu na hiyo ndiyo sababu kubwa iliyomfanya kujiunga na kitengo cha usomaji wa habari. Taarifa yake ya kwanza redioni ilikuwa katika mwezi wa Oktoba, mwaka wa 1996 ingawa baadaye alitafsiri makala mbalimbali na pia kutangaza mchezo wa kandanda moja kwa moja kutoka viwanjani. Ingawa alikuwa ameajiriwa, siku zake za kwanza katika Shirika la Utangazaji la K.B.C. hazikuwa za starehe. Mwanzoni, aliishi katika kijumba duni kilichokuwa eneo la Kabiria, katika mtaa wa Riruta Satelite jijini Nairobi na kwa sababu wakati huo zamu yake kazini ilikuwa ikianza saa tisa alfajiri, Walibora alikuwa akilazimika kuamka mapema zaidi. Hii ilitokana na sababu kuwa alikoishi, hakukuwa na barabara nzuri ambayo ingeliwezesha gari la shirika la K.B.C kwenda kumchukua. Kwa hivyo, alishurutika kurauka na kutembea hadi mahali salama ambapo gari lingempata. Aliondokewa tu na kazi hii ya ziada baadaye alipopewa nyumba ya Shirika la K.B.C katika barabara ya Jogoo.

Walibora anachukulia mwaka wa 1997 kama uliokuwa na umuhimu zaidi maishani mwake. Huu ndio mwaka ambao riwaya yake ya kwanza na maarufu sana, *Siku Njema* (1996) ilipochaguliwa kuwa mojawapo ya vitabu vya

kutahiniwa vya fasihi katika mtihani wa kidato cha nne (K.C.S.E). Huu pia ndio mwaka ambao bintiye anayeitwa Nasambu ama Zawadi alizaliwa na pia ndio mwaka ambao ndoto yake ya kujiunga kikamilifu na kazi ya utangazaji na Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) kama mhariri wa habari. Wakati mwingine Walibora angejiunga na watangazaji kama Leonard Mambo Mbotela katika kutangaza kandanda, ingawa anasema kuwa wadhifa wake kama mhariri wa habari haukumpatia fursa nzuri ya kusoma habari; kazi aliyohisi kuwa ilimwafiki zaidi, kando na ile kutangaza kandanda.

Walibora alipata fursa ya kusoma habari alipojiunga na shirika la utangazaji la 'Nation' mwaka wa 1999. Alipokuwa na shirika hili, Walibora anasema kuwa aliridhika mno. Ugwiji wake wa Kiswahili ulisaidia katika kuliimarisha na kulikuza shirika la utangazaji la runinga la 'Nation', kitengo cha Kiswahili. Walibora alikuwa akiongoza jopo la Kiswahili la shirika hilo katika kutafsiri habari kutoka Kiingereza hadi Kiswahili na wakati mwingine iliwabidi kufanya hivyo kwa muda mfupi sana. Akiwa na shirika la habari la 'Nation' Walibora alipata fursa ya kwenda kwa mafunzo zaidi katika Kituo cha Mafunzo ya Redio cha Deutsche Welle, Ujerumani. Walibora pia atakumbukwa kwa kubuni istilahi 'eneo-bunge' ambayo imekubalika na hutumiwa na vyombo vya habari nchini kwa maana ya sehemu ya nchi inayowakilishwa bungeni na mjumbe aliyechaguliwa na wananchi.

Licha ya harakati zake za kuajiriwa na za kubadilisha kazi moja na nyingine, Walibora ameweza kupata nafasi ya kuendeleza masomo yake. Alifuzu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi na shahada ya daraja la kwanza katika Kiswahili na

Fasihi na kwa sasa anaendeleza masomo yake ya Uzamifu katika Chuo Kikuu cha jimbo la Ohio-Columbus, nchini Marekani ambako anasomea masuala ya Fasihi ya Kiafrika na ya Wamerikani wenye asili ya Kiafrika. Mbali na shughuli za masomo, Walibora amepata nafasi ya kuandika vitabu kadhaa na kwa sasa anavyo vitabu vinane vilivyochapishwa. Hivi ni: *Siku Njema* (1996), *Ndoto ya Amerika* (2001), *Kufa Kuzikana* (2003), *Mgomba Changaraweni* (2003), *Mtu wa Mvua* (2004), *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza, Kitabu cha Wanafunzi* (2004), *Uhondo wa Kiswahili – Kidato cha Nne, Kitabu cha Mwalimu* (2005), na *Ndoto ya Almasi* (2006).

Walibora pia ameandika hadithi fupi na baadhi yazo zimo katika vitabu kama *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Vile vile, ameandika makala mbalimbali ya kitaalamu katika lugha ya Kiswahili. Walibora pia ameandika vitabu vingine ambavyo anatarajia vitatolewa hivi karibuni. Vitabu vinavyotarajiwa ni: *The American Dream* ambacho ni tafsiri ya Kiingereza ya *Ndoto ya Amerika*, *Kaka Tupu*, *Uhondo wa Kiswahili – Kidato cha Nne*, *Diwani ya Karne*, *Mwongozo wa Mwisho wa Kosa*, *Guilty but Innocent* na hadithi fupi kadhaa pamoja na makala ya kifasihi. Katika *Guilty but Innocent*, Walibora anatarajia kuanza kuwasiliana na hadhira yake kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Isisahaulike kuwa kitabu hiki *Ndoto ya Amerika* (2001) ndicho kilichoshinda tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta, mwaka wa 2003, nchini Kenya.

Kati ya vitabu sita vya Walibora ambavyo vinatarajiwa kutolewa hivi karibuni, mwenyewe anasema kuwa anakienzi zaidi kitabu *Guilty but*

*Innocent.* Hii ni hadithi inayosimulia masaibu anayopitia msichana aliyebakwa. Walibora anasema kuwa hadithi hii ina umuhimu zaidi kwake kwa sababu wakati wa kuiandika, hadithi ilijisimulia yenyewe licha ya kuwa ilikuwa ni mara yake ya kwanza kujaribu kuandika bunilizi akitumia Kiingereza.

Walibora amemwoa Anne Waliaula, ambaye ni mwalimu na wana mabinti wawili: Nasambu ama Sheila Zawadi na Katila Samba.

## **2.2 Kazi za Ken Walibora**

Walibora ameandika kazi mbalimbali za Kiswahili. Kazi hizo ni kama riwaya, vijirirwaya au fasihi ya watoto na pia hadithi fupi. Baadhi ya kazi zake ambazo zimechapishwa ni kama zifuatazo:

### **2.2.1 RIWAYA YA SIKU NJEMA (1996)**

Mhusika mkuu katika riwaya hii ni Kongowea Mswahili ama Msanifu Kombo. Kijana huyu alipitia shida nyingi na kutarajia kuwa siku moja, siku njema ingemfikia. Akiwa shuleni alitukanwa na kukejeliwa na wenzake. Mamake, Zainabu Makame, alipoaga dunia, alilazimika kwenda kuishi na mjombake. Huko, mkaza mjomba wake, Mwanasaumu alimtesa sana kwa kumnyima chakula na kumfanyisha kazi nyingi.

Kongowea alilazimika kuguria nchini Kenya ili kumsaka babake ambaye aliishi Kitale. Kutoka Tanga, safari yake ilimfikisha Mombasa kisha Eldoret na hatimaye Kitale. Kongowea aliugua alipokuwa mkahawani mjini Kitale

lakini aliuguzwa na kufadhiliwa na Bi. Mercy MacDonald aliyempeleka hadi kwake. Huko anamwajiri na pia kuishi na Kongowea akiwa katika shughuli za kumtafuta babake.

Siku moja alipokuwa akienda kutoa mhadhara shuleni Suwerwa, Kongowea alikutana kwa mara ya pili na Mzee Kazikwisha aliyemkazania kuwa aende kwake ama akikosa, angejuta. Walipofika kwake, Mzee alimwelezea maombi na matumaini yake ya siku nyingi. Pia alimwelezea mahali ambako alipendelea azikwe akifa; kisha akamruhusu kuendelea na safari yake ya kwenda shuleni.

Alipokuwa akihutubia, Mzee Kazikwisha alikuja nyuma ya ukumbi na kuanza kumsikiliza. Wanafunzi na walimu walitoroka walipomwona. Kazikwisha alimsifu Kongowea kwa hotuba yake nzuri na akamwagiza aende kwake siku ya pili.

Alipoitikia mwito huo baada ya siku kadhaa, Kongowea aliingia nyumbani mwa Kazikwisha na kupata barua iliyomfumbulia siri zote za maisha yake. Kumbe Mzee Kazikwisha ndiye aliyekuwa babake! Katika barua, pia alielezwa wapi pa kumzika babake na masharti ya kumzika.

Kutoka sebuleni, Kongowea aliingia chumbani ambamo aliikuta maiti ya baba yake iliyooza. Alimzika kama alivyoagizwa. Alipokuwa akichimba kaburi, aliupata wasia ulioonyesha kuwa yeye ndiye aliyekuwa mrithi wa mali ya Juma Mukosi. Kongowea akatajirika ghafla. Mwishowe alimwoa Vumilia

binti Abdala, rafikiye wa utotoni tangu walipokuwa shuleni, wakaishi katika mastakimu ya marehemu babake wakifurahia maisha. Kwa Kongowea, siku njema ilikuwa imefika.

### **2.2.2 NDOTO YA ALMASI (2006)**

Riwaya hii inarejelea maisha na masaibu ya kijana aliyeitwa Almasi. Kama anwani ya riwaya inavyotudokezea, Almasi alikuwa na ndoto nyingi maishani, lakini ndoto hizo hazikutimia kamwe. Kwanza, Almasi alitamani awe mwanakandanda maarufu na achezee timu ya taifa na ajulikane kama kina Mohamed Magogo na Joe Kadenge. Pili, Almasi alikuwa na ndoto ya kuwa mtangazaji wa redio na runinga na aliwahasudu watangazaji kama Mambo Mbotela, Khadija Ali, Anderson Kalu na Hassan Mazoa. Lakini ndoto hizi zilibaki kuwa ndoto kutokana na sababu kadhaa. Kwanza, familia ya Almasi ilikuwa maskini na pia Almasi mwenyewe japo alipata ufadhili wa masomo, hakusoma. Alifungwa jela kwa kuhusishwa na mgomo uliokuwa shuleni kwao. Alipotoka jela, hakuna aliyetaka kumkaribia. Alitengwa na babake pamoja na wanakijiji. Akaanzisha kazi ya ukulima aliyoifanya mchana kutwa.

Almasi pia alikuwa na ndoto ya kumwoa binti mmoja chotara aliyeitwa Chebosio. Binti huyu alikuwa amepata mimba na kumsingizia Almasi, akaozwa kwa lazima na wazee wa kijiji. Baadaye, Almasi aliambiwa kuwa Mzee Masasi, babake ndiye aliyekuwa amempatia Chebosio mimba. Hili lilimshtua sana Almasi.

Riwaya inaisha wakati Mzee Masasi alipogutuka kutoka usingizini na akakuta kuwa wakezwe wawili walikuwa wamemtoroka. Kwa hasira, alimwomba Almasi kamba ili ajinyonge, akaletewa, lakini akaokolewa na mkaza mwanawe, Chebosio, aliyempokonya kamba hiyo.

Baada ya kisa hiki, Mzee Masasi alizimia kufungua ukurasa mpya wa maisha yake na aila yake. Aliwaita wazee wa kijiji, na wakiwa mashahidi, akaitoa dhahabu aliyoileta kutoka Pokot Magharibi kama amana kwa mkewe, Paulina, na kumkabidhi mwanawe Almasi hadi mwenye amana atakaporudi. Alipania kufanya suluhu na mkewe na mwanawe Almasi na kuomba radhi kwa makuruhu aliyowafanyia. Ikiwa mkewe na mwanawe wangetumia dhahabu hiyo kuchangia kutimia kwa ndoto zao mbalimbali, yeye hakujali tena. Ilikuwa ni juu yao.

### **2.2.3 VIJIRIWAYA**

#### **(i) Mgomba Changaraweni (2004)**

Ni hadithi inayohusu vijana wawili; Chongameno na Alice Kesho. Chongameno alikuwa kijana maskini, lakini aliyekuwa na sura na tabia nzuri. Hili lilimfanya Alice kumtaka wawe marafiki japo Alice alitoka aila tajiri. Baada ya miaka sita ya kutofaulu, Alice alimwambia Chongameno amkubali wawe wapenzi ama angefanya jambo ambalo lingedhuru watu wengi. Alipokataliwa mara ya mwisho, Alice aliamua kuuchoma msitu ambamo Chongameno alikuwa akichungia ng'ombe. Juhudi za Chongameno kuuzima moto huo hazikufanikiwa; alizimia na kulazwa hospitalini alikolindwa na askari. Baada ya kupona, alifungwa jela kwa kuuchoma msitu. Chongameno

aliachiliwa baadaye baada ya ukweli kubainika. Ukweli ulikuwa katika barua ambayo Alice alikuwa ameandika kabla hajajiua.

“Kwa heri wazazi wangu. Sina uso wa kuukabili ulimwengu baada ya makosa yangu. Chongameno anaumia bure. Mimi ndiye niliyewasha moto. Tukutane ahera.”  
(Uk. 72).

**(ii) Mtu wa Mvua (2004)**

Kijiriwaya hiki kina hadithi tatu: (a) *Sungura Hasara*, (b) *Mtu wa Mvua* na (c) *Charo na Watoto Watoro*.

**(a) *Sungura Hasara* (Uk. 1 – 29).**

Hadithi hii inamhusu kijana kwa jina Fumbo. Fumbo alikuwa mjanja, mwizi na mwongo. Aliiba mchoro wa nduguye, Masika na kuupeleka shuleni alikosifiwa kwa ustadi wake katika uchoraji. Mwalimu Mkuu aliamua kumpatia kazi ya kuuchora mchoro kama huo kwenye ukuta wa shule, lakini Fumbo alishindwa. Alisingizia kuwa ni mgonjwa.

Uongo na ujanja wake uliisha pale Mwalimu Mkuu alipozuru kwao na kugundua mambo mengi. Shuleni, Fumbo aliadhibiwa na kulazimishwa kuungama hadharani kuwa yeye ni mwizi, mwongo na mjanja.

**(b) *Mtu wa Mvua* (Uk. 30 – 45)**

Hii ni hadithi ya pili katika kijiriwaya cha *Mtu wa Mvua* (2004) na pia ndiyo anwani ya kijiriwaya hiki. Wahusika katika hadithi hii ni Dora, wazazi wake na mchungaji ng’ombe wao kwa jina Okungu lakini ambaye wanakijiji cha Chebukaka walimbandika jina ‘Mtu wa Mvua’.

Mandhari ya hadithi hii ni kijijini Chebukaka. Okungu aliyetoka Kisumu alikaribishwa kwa kina Dora mvua ilipokuwa ikinyesha. Alikuwa akitafuta kazi ya kulima shamba au kuchunga ng'ombe.

Baada ya siku chache familia ya Dora iligundua kuwa Okungu alikuwa na miujiza fulani; kwa mfano, hakuweza kunyeshewa na mvua, aliamrisha mvua ianze au isite kunyeshwa na pia siku moja ng'ombe wa kina Dora walipoibwa, alifanya miujiza waliowaiba ng'ombe hao wakawarejesha na kujisalimisha.

Kutokana na vitimbi vyake vya kuianzisha ama kuisitisha mvua isinyeshe, wanakijiji walimpatia Okungu jina, 'Mtu wa Mvua', Okungu alifanya kazi kwa kina Dora kwa miaka saba. Alikuwa akiamuru mvua inyeshe au isinyeshe. Kupitia hadithi hii, Walibora anatuonyesha kuwa ukarimu na huruma ni maadili muhimu maishani mwa binadamu na vile vile akatutahadharisha dhidi ya kuwahukumu watu kutokana na maumbo yao ya nje. Kwa mtazamo wa kijuu juu, Okungu alionekana mtu asiye na maana, lakini kumbe alikuwa na maarifa yaliyoweza kuisaidia, si tu aila ya kina Dora, bali pia kijiji kizima cha Chebukaka.

***(c) Charo na Watoto Watoro***

Hadithi hii inamhusu kijana Charo ambaye licha ya kuwa na bidii na uerevu shuleni, alipenda uongo na kulala. Siku moja alipochelewa kufika shuleni, alifukuzwa ili aende akawalete wazazi wake. Akiwa njiani, aliamua kutoenda kwao na badala yake akajiunga na watoto wa mitaani.

Akiwa mitaani, alipitia shida nyingi. Kilele cha hadithi ni wakati tunampata Charo akiwa amelazwa hospitalini baada ya kuila nyama yenye sumu. Wazazi wake walimpata baada ya msako wa siku nyingi. Alipopata afueni, wazazi walimrudisha Charo kwao. Alijutia vitendo vyake, akabadilisha tabia na akaendelea na masomo yake.

#### 2.2.4 Hadithi Fupi

Licha ya riwaya na vijiriwaya, Walibora pia ameandika hadithi fupi. Katika diwani ya *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000), Walibora ametunga hadithi fupi mbili, *Kipara Ngoto* (Uk. 61-66) na *Songoro Leo Mimi* (Uk. 95 – 97). Katika hadithi ya *Kipara Ngoto*, Walibora anasimulia athari za malezi mabaya katika jamii. Hadithi inamhusu kijana anayeitwa Matata na ambaye ana jina la msimbo ‘Kipara Ngoto’. Baada ya kufukuzwa kutoka shule tatu za sekondari, kwa mwaka mmoja, Ami yake Matata aliamua kuwa Matata aende asomee kwake ili amtie adabu. Kwanza, alimnyoa nywele zote kichwani na hili ndilo lililofanya Matata akabandikwa jina ‘Kipara-Ngoto’.

Alipojiunga na Shule ya Upili ya Sitamani, Matata alipata maadui wengi kuliko marafiki. Alibandikwa jina ‘Kipara-Ngoto’. Hili lilimchukiza sana na akaamua kumfunza adabu aliyemandika jina hilo. Siku moja akarauka mapema na kuondoka pamoja na mizigo yake. Alikuwa ameazimia kulipiza kisasi. Kidudu-mtu aliyempatia jina hilo alikuwa Aggrey, mtoto wa sheha wa kijiji cha Sangura. Matata alimdunga kisu cha ubavuni na ilimbidi kulazwa hospitalini kwa mwezi mmoja kabla ya kupata afueni. Hadithi inapoisha, hatujui alikotokomea Matata. Tunaachwa na taharuki.

Hadithi fupi ya pili katika *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000) inaitwa ‘Songoro Leo-Mimi’ (Uk. 91 – 96). Katika hadithi hii, Walibora anagusia maisha ya Bwana Songoro Leo-Mimi ambaye alikuwa na vioja si haba. Songoro aliishi katika mtaa wa Laini Moja na maisha yake yalionyesha mkinzano kati ya imani ya dini au ya kiroho na uhalisi. Baada ya kuokolewa mwaka wa 1963, Songoro aliishi maisha ya Kikristo.

Masaibu yaliyompata Songoro ni ukosefu wa fedha za kulipia kodi ya nyumba, kuwaelimisha wanawe na vile vile kuwatunza kwa chakula na mavazi. Baada ya kupokea kitita cha shilingi elfu sabini, uwendawazimu wa Songoro uligeuka na ukawa kichaa. Aliitelekeza aila yake na kuyoyomea kusikojulikana ili kuyatafuta maisha ya anasa na uluwa aliyoyakosa kwa miaka hiyo yote. Hadithi inaishia pale Songoro alipopatikana amezuiliwa katika hoteli ya Kitalii ya ‘Park Villa’, kashindwa kulipia huduma. Inasemekana alikuwa ameingia huko an kipusa mmoja na kupangisha chumba. Alipoamka, alijikuta peke yake ilhali pesa zake zote zikiwa zimetoweka kama moshi hewani.

Katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), Walibora ameandika hadithi fupi moja kwa anwani ‘Tuzo’ (Uk. 57-62). Hadithi hii inasawiri masuala kadhaa yanayopatikana katika jamii zetu za sasa. Katika hadithi hii, Walibora amezungumzia ufisadi na maonevu yanayobainika katika mahali petu pa kazi na namna mapendeleo

yanayofungamana na uhusiano wa kidamu yanavyoathiri na kufifisha utendaji kazi wetu.

Hadithi inahusu wahusika watatu wakuu; Kibwana, Salome Dzero na Profesa Dzero. Kibwana alikuwa mtangazaji mashuhuri wa redio aliyependwa na wengi na alikuwa akifanya kazi na Salome. Siku moja Salome alimshtua kwa habari kuwa Kibwana alikuwa ameshinda tuzo ya mwaka ya utangazaji habari wa redio na kuwa Kibwana angepewa tuzo hiyo na Rais siku inayofuata. Salome alimpongeza kwa jambo hilo. Lakini kumbe alikuwa anachezwa shere. Siku ya tuzo ilipofika, Salome Dzero ndiye aliyekuwa mshindi. Jambo hili lilimshtua sana.

### **2.3 Kiishilio**

Katika sura hii, tumeangalia historia, asili na kazi za Ken Walibora. Kwanza tumetanguliza kwa kufafanua umuhimu wa kuelewa historia na maisha ya mwandishi kwa sababu jambo hili limechangia kwa njia moja au nyingine katika kuzielewa kazi za mwandishi kama huyo.

Pili, tumerejelea baadhi ya kazi za mwandishi, hasa zile ambazo tayari zimechapishwa. Kazi ambazo zimerejelewa kwa ufupi ni riwaya, vijiriwaya au fasihi ya watoto na vile vile hadithi fupi. Kazi hizo zimerejelewa kwa ufupi tu ili kutupa mwangaza wa kazi nyingine za mwandishi ambazo zitarejelewa katika sura zinazofuata. Kazi hizo pia hazikurejelewa kwa kina kwa sababu hazikuwa kiini cha utafiti huu. Kazi zilizorejelewa ni *Siku Njema* (1996), *Mgomba Changaraweni* (2004), *Mtu wa Mvua* (2004) na *Ndoto ya Almasi*

(2006). Tumerejelea pia hadithi fupi tatu za Walibora zinazopatikana katika diwani ya *Mwenda Wazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na ile ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Baada ya kuziangalia kwa ujumla kazi za Walibora, tumeweza kujenga msingi madhubuti wa kuzihakiki riwaya zake zinazohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti huu.

Katika sura ya tatu tutatoa maelezo ya jumla juu ya kijiriwaya cha *Ndoto ya Amerika* (2001). Pia tutajadili namna ambavyo mwandishi ametumia uhalisia na maigizo kama nyenzo za kukuza na kueleza maudhui katika kijiriwaya hicho.

## SURA YA TATU

### UIGIZAJI NA UHALISI KAMA NYENZO ZA MAUDHUI KATIKA

#### *NDOTO YA AMERIKA (2001)*

### 3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia maelezo ya kijumla kuhusu kijiriwaya cha *Ndoto ya Amerika*. Wahusika na matukio muhimu yamerejelewa kutoka mwanzo hadi mwisho wa kijiriwaya hicho. Sura pia imejadili namna maigizo yanavyobainika katika sehemu mbalimbali za kazi hii na jinsi maigizo hayo yalivyotumiwa na mwandishi kuonyesha maudhui mbalimbali.

Vipengele vya uigizaji ambavyo vimetumiwa katika kudhihirisha maudhui ni sifa za wahusika ama maelezo ya mwandishi kuhusu tabia zao; maneno na vitendo vya wahusika; lugha wanayotumia wahusika, mandhari ya matukio na mada au jambo linalosababisha mgogoro fulani. Mbinu za lugha kama vile taharuki, tashbihi na sadfa pia zimegusiwa kwa namna zinavyochangia katika suala na malengo ya utafiti.

Hayo yote yamejadiliwa kwa mujibu wa suala letu la utafiti ambalo ni kubainisha matumizi ya maigizo katika kazi teule za Ken Walibora na jinsi maigizo hayo yanavyotumiwa kuonyesha maudhui. Vile vile, imebainishwa jinsi maudhui mbalimbali yalivyo na uhalisi. Uhakiki umefanywa kwa kuzingatia nadharia za uigizaji na uhalisia.

### 3.1 Maelezo ya Jumla juu ya *Ndoto ya Amerika* (2001)

Kitabu hiki kina jumla ya kurasa arobaini na nane na sura sita. Kinazungumzia maisha ya vijana wawili, Madoa Namasake na Isaya Yano ama Isa. Vijana hawa waliishi na wazazi wa kike waliokuwa wakiwafanyisha kazi za sulubu kama kulima, na wakati mwingine walichapwa na wazazi wao. Shuleni, walimu walikuwa wakali. Ili kuepukana na shida hizo, waliamua kuacha shule na kukimbia nyumbani. Walishawishika kuacha shule kwa ahadi za uongo kuwa wangeenda Amerika. Namasake alimchukua mwenzake, Yano kutoka kwao kijijini Sangura ili wafanyiwe mpango wa kwenda Amerika na 'Rock Mwamba'.

Namasake alimwibia Mzee Zakayo Wekesa shilingi elfu mbili na mia tatu walizotumia kuwafikisha Nairobi kwa 'Rock Mwamba'. Baada ya siku mbili, Namasake na Mwamba walienda kuiba katika mtaa wa Buruburu, lakini mipango yao ikatibuka. Walishikwa na msako uliofanywa na askari nyumbani kwa 'Rock Mwamba' mtaani Kayole ambako bunduki, bastola, risasi na vitambulisho bandia vilinaswa.

Mahakamani, Zablon Okutoyi au 'Mwamba' alishtakiwa kwa kupatikana na bunduki kumi na nane, risasi arubaini na vitambulisho bandia kumi. Pia alishtakiwa kwa kujaribu kuiba kwa kutumia nguvu na kwa kuteka nyara watoto saba na kuwaua. Aidha alishtakiwa kwa kutoroka kutoka gereza la Kamiti mwaka uliotangulia alikokuwa amefungwa maisha. Okutoyi aliuliwa alipojaribu kumpokonya askari jela bunduki ili atoroke tena.

Madoa Namasake alifungwa kwa miaka mitatu, ilhali Isaya Yano aliachiliwa. Baadaye, Isaya Yano aligundua kuwa ile 'Ndoto yao ya Amerika' haikuwa kweli bali ulikuwa uhalifu ambao rafiki yake alitaka wautekeleze kwa pamoja. 'Ndoto ya Amerika' hatimaye iliwatumbukia nyongo.

### **3.2 Uigizaji na Uhalisi kama Nyenzo za Maudhui katika *Ndoto ya Amerika***

Kwa mujibu wa Bauman, (1992) maigizo ni tukio la mawasiliano au kuwasiliana. Pia anasema kuwa maigizo aghalabu hurejelea hali ya kuwasiliana na hadhira kupitia jukwaa kwa njia inayoiteka hisia hadhira hiyo. Ni kwa muktadha huo ambapo tumejadili namna maudhui ya *Ndoto ya Amerika* yamewasilishwa. Haya yamefanywa kwa mujibu wa nadharia za uigizaji na uhalisia.

#### **3.2.1 Sifa za Wahusika**

Maelezo ya Ken Walibora kuhusu sifa za wahusika yamejenga picha akilini mwa hadhira ambao wanaweza wakachukuliwa kama watazamaji katika ukumbi wa kuigiza au sinema. Mikabala ya nadharia ya uhalisia inasema kwamba, wahusika wanapaswa kusawiriwa wakiwa wa kawaida katika mandhari ya kawaida. Jambo hili huiwezesha hadhira kusadiki mambo yatakayokuwa yakiigizwa. Uhalisi wa wahusika ni sifa muhimu ya nadharia ya uhalisia. Vile vile nadharia hii inashikilia kuwa, mwandishi hana budi kuhusisha kazi yake na wahusika halisi ambao anawatoa kutoka mazingira yake.

Isaya Yano anasema kuwa rafiki yake, Madoa au kwa jina la kubandikwa

‘Ndiyo Alaa’ alikuwa na tabia hizi:

“Tulikuwa tukisoma naye katika darasa moja lakini hakuwa akihudhuria masomo kila siku. Alikuwa hapendi kusoma. Tena alikuwa haelewi chochote shuleni.” .... ukimwuliza,  
“Moja kuongeza moja utapata nini?” atakwambia  
“Tano”, mara nyingi alikuwa akitoroka shuleni na kwenda mahali pasipojulikana.” (Uk. 7).

Kupitia maelezo hayo, tunagundua kuwa madoa ni mjanja na pia zuzu.

Huenda haya yalichangia katika hali yake ya kujiingiza katika uhalifu. Isaya

Yano anaeleza zaidi, kuwa siku nyingi zingepita huku Madoa akiwa hajulikani aliko.

“Ndiyo Alaa, ulikuwa wapi?” nilikuwa nikimwuliza kila aliporudi Sangura.  
“Nilikuwa Nairobi”, alikuwa akijibu.  
“Ulikuwa Nairobi?”  
“Ndiyo Alaa!” alijibu (Uk. 7).

Isaya anaeleza kuwa mara nyingine Madoa angemwambia kuwa alikuwa ametoka Kisumu, Eldoret, Nakuru, Mombasa na miji mingine mikubwa nchini Kenya.

“Kuna wakati nitakwenda na sitarudi tena”, alimwambia Isaya siku moja walipokuwa wakitoka shuleni.  
“Kwani utakwenda wapi?” nikamwuliza.  
“Nitakwenda Amerika”, alijibu Madoa  
“Wataka kwenda Marekani?” nikashangaa.  
“Hapana, naenda Amerika, mbona husikii?”  
“Nimesikia bwana”, nikamwambia.  
Akasema kwa hasira, “Basi hujaelewa”.  
“Umesema utakwenda Marekani, sivyo?,  
“Nimesema Amerika”, akasema Madoa.  
“Amerika na Marekani ni sawa. Hukumbuki alivyosema mwalimu juzi?” nikamkumbusha.  
“Upuuzi huo!” akajibu tena kwa hasira.  
“Usiniambie mambo ya mwalimu. Ndiyo maana nimechoshwa. Nimechoshwa na huyo mwalimu. Nimechoshwa na maisha ya hapa Sangura. Nimechoshwa na masomo. Nimechoshwa na kwetu. Sitaki kuchapwa viboko kila siku. Sitaki kufanya kazi nyumbani kwetu. (Uk. 7-8).

Huu ni mfano mzuri wa maigizo. Wahusika wanaongea kwa kupeana zamu, hatua kwa hatua. Kupitia maigizo hayo, tunaona kuwa Madoa alikuwa mwenye hasira, mvivu, mwongo na pia aliyekengeuka. Hasira zake zadhihirika anavyojibizana na Isaya kwa sababu hataki kukosolewa. Ni mvivu kwa vile anasema kuwa hakutaka kufanya kazi, uongo wake unaonekana anapomdanganya Isaya kuwa alitembelea miji mingi nchini. Amekengeuka kwa sababu ni kama amechukia chochote chake na chao na anataka kukimbilia Marekani.

Kupitia maneno ya wahusika hawa, maudhui ya kunyanyaswa kwa watoto kwa kufanyishwa kazi na kuchapwa yamejitokeza. Kunayo maudhui ya umaskini. Madoa alifanyishwa kazi ili kukidhi mahitaji ya familia yake.

Hali nyingine ya uigizaji inabainika kupitia mhusika Dzombo katika *Walenisi* (1995). Alihukumiwa kifo kwa sababu ya hatia bandia ya kuwachochea wafanyakazi watiifu na kupinga dhuluma. Alikuwa afe kwa kupitia mtambo wa sayari. Anafikishwa kwenye kituo cha sayari akiwa tayari amevalishwa mavazi ya kifo. Umati wa watu ulikuwa umekuja kushuhudia namna Dzombo angepaishwa na mtambo wa sayari na hatimaye kuangamizwa. Kabla ya kuingizwa sayarini, alifunzwa na mnyongaji halali jinsi ya kuendesha mtambo huo. Taswira inayojitokeza ni ya uigizaji na pia inao uhalisi. Ni jambo la kawaida kwa watu wanaopenda ukweli na wanaotetea kazi zao na za wanyonge wengine kunyanyaswa na hata kuangamizwa na vyombo vya dola.

Wahusika hawa wawili wanaongea moja kwa moja. Kwa mujibu wa nadharia ya uigizaji, uigizaji unaomshirikisha mtendaji aliye hai huwa na ufanisi mkubwa kwa sababu huathiri hadhira moja kwa moja. Hili limebainika kupitia maongezi ya wahusika hawa. Madoa ametumia takriri katika kusisitiza azma yake ya kuepokana na matatizo.

Uzuzu wa Madoa unabainika katika mazungumzo haya;

“Sina pesa mfukoni. Siko tayari kwa safari hii ndefu.  
Lazima twende hadi Nairobi kwanza, umbali wa kilometa zaidi ya elfu nne kutoka hapa Cherang’ani”.  
“Ni kilometa mia nne, bwana”, nikamkosoa.  
“We’ ndiye umeenda Nairobi au mimi? Akajibu Madoa kwa hasira.

Maneno hayo yanabainisha kuwa Madoa alikuwa mkaidi na hakupenda kukosolewa. Pia hakuweza kukisia mwendo kati ya Cherang’ani na Nairobi. Madoa pia alikuwa mwizi na kupitia maneno na vitendo vyao na Isaya, maudhui ya uhalifu, hasa wizi yanabainishwa. Wote walikwenda kwa Mzee Zakayo Wekesa na wakamwibia pesa. Mzee alikuwa amesafiri. Isaya anaeleza:

“Akaniamuru nifuatane naye hadi nyumbani kwa Mzee Wekesa..... Tayari?” nikamwuliza.  
“Ndiyo Alaa!”  
“Umeiba bwana?”  
“Tumeiba sote”.  
“Nani aliyekufunza haya yote?”  
“Mwamba”, akajibu. “Rafiki yangu ‘Rock Mwamba.’  
“Tumefanya mengi pamoja.”

Kupitia kauli hizi, maudhui ya uhalifu na dhuluma za watoto yanabainika. ‘Rock Mwamba’ kama mtu mzima alikuwa akiwahusisha watoto katika uhalifu.

Mpango wa wizi wa Madoa na Rock Mwamba unatibuka na wanashikwa.

Isaya aliyekuwa ameachwa akilala anaamshwa na vurumai, Isaya anaeleza:

“Askari wote walikuwa na bunduki mikononi.  
“Nikaanza kutetemeka... kisha wakapindua kitanda  
nilichokuwa nimejificha chini.  
“Mamaa! Waaii!” Nikapiga kelele. (Uk. 37)

Maelezo mengine ya Isaya akiwa mahakamani,

“Wewe Isaya Yano umeshtakiwa kuwa mnamo tarehe 2 Novemba mwaka huu ulipatikana ukishirikiana na mtu anayeaminiwa kuwa jambazi hatari.  
Unakiri au unakataa shtaka?”  
“Ni Madoa aliyenidanganya kuwa ana rafiki atakayetupeleka Amerika. Ndiye aliyenileta hapa kwa rafiki yake huyo”.  
“Kwa hivyo unakubali makosa?” aliuliza tena hakimumu.  
“Naomba msamaha afande” (Uk. 43).  
“..... Afande ninaomba nisamehewe kwa sababu Madoa ndiye aliyenidanganya. Alinitorosha shuleni na nyumbani. Akaniambia tunakwenda Amerika kumbe ananipeleka kwa jambazi”.  
“... ninataka nirudi shuleni nimalize masomo yangu.  
Nikishakuwa mkubwa nigombe kiti cha ubunge niwe mbunge wa Cherang’ani.....”  
“Hutaki kwenda Amerika?” alisema hakimumu.  
“Sitaki”.

Kupitia maigizo haya, tunagundua kuwa Isaya alikuwa mwoga. Anapiga mayowe na kutetemeka anapowaona polisi. Yeye pia ni mkweli. Hili labainika kupitia maelezo yake kwa hakimumu. Isaya pia ana azma pevu na bidii. Anataka asome kisha baadaye awe mbunge. Maudhui yanayobainika ni kama uhalifu na kuonewa kwa watoto. Madoa alitaka kumshirikisha Isaya katika wizi, naye Rock Mwamba anumia watoto katika ujambazi.

Mhusika Zablon Okutoyi ama Rock Mwamba amejengwa kama mtu wa sifa zisizopendeza. Isaya anaeleza kuwa walipofika nyumbani kwa Mwamba katika mtaa wa Kayole, mlango ulifunguliwa kisha,

“... Nikamwona mwanamume mmoja mrefu mweusi .... mweusi kuliko makaa.

Alikuwa amevalia miwani ya jua, fulana nyekundu na suruali nyeusi.

Nywele zake zilikuwa zimesukwa rasta. Sauti yake ilikuwa nzito sana.

Nadhani alipoongea, kuta za nyumba zilitetemeka.

(Uk. 31).

Mwandishi ametumia taswira na chuku kututajia baadhi ya sifa za Rock

Mwamba. Mwamba pia ni mwizi na mhalifu kwa jumla. Haya yaonekana

kupitia maneno ya Isaya na Madoa:

“Humo ndani ya koti mna bunduki,” aliniambia madoa kwa sauti ya chini.

“Aah!” nilikodoa macho kwa mshangao.

“Usimchezee mwamba mwamba ni mwamba kweli kweli.”

“Kwani bunduki anafanyia nini?”, nikamwuliza

“Anafanyia ‘Kazi’. We’ Isa ni mshamba kweli”.

(Uk 32)

Uhalifu wa mwamba pia unabainika katika maelezo ya Isaya. Nyumbani

mwake, mlikuwa na vitambulisho vingi, lakini vyote vilikuwa na picha ya

Rock Mwamba lakini majina kwa kila kitambulisho yalikuwa tofauti. Baadhi

ya majina yalikuwa tofauti. Baadhi ya majina yalikuwa: Gideon Obiero, John

Kamau, Mwachofi, Mwandawiro, Katana Karisa na David Korir, Isaya

anauliza;

“Hivi vitambulisho vyote ni vya nini?”

“Vya kuwachenga polisi”, alisema Madoa

(Uk. 33).

Mwamba pia amesawiriwa kama mwaaji, mtoro na mkaidi. Sifa hizi zabainika

kortini.

“Wewe Zablon Okutoyi .... umeshtakiwa kwa makosa manne.

Kwanza, umeshtakiwa kwa kupatikana na bunduki kumi na

nane; risasi arobaini, na vitambulisho bandia kinyume cha

sheria. Pili, umeshtakiwa kwa kujaribu kuiba kwa kutumia

nguvu.... Tatu, wewe umeshtakiwa katika tarehe mbalimbli kati

ya mwezi Oktoba mwaka jana na juni mwaka huu, uliteka

nyara watoto saba na kuwaua. Nne, umeshtakiwa kwa kutoroka kutoka gereza la Kamiti mnamo Septemba mwaka jana ulikokuwa umefungwa maisha. (Uk. 40-41).

Karani anapomwuliza ikiwa anakubali au anakanusha mashtaka hayo; Okutoyi ananyosha mkono:

“Afande kwanza naomba hawa watoto waachiliwe maana hawaelewi kinachoendelea”.

“Huwezi kuiambia mahakama la kufanya. Wewe sema kama anakubali au unakataa mashtaka yako”.

“Nakataa”. (Uk. 41).

Ukaidi na kiburi cha Okutoyi au Mwamba vinaonekana kupitia majibu yake. Kupitia kwake, maudhui ya uhalifu kama vile wizi, mauaji na kughushi stakabadhi yamebainika. Suala la kuonewa kwa watoto pia limegusiwa kwa sababu tunaona kuwa Okutoyi ndiye anayesababisha Isaya na Madoa kushikwa na kushtakiwa. Sifa za wahusika hawa ambao ndio wametawala hadithi yote zina uyaikinifu unaoweza kupatikana katika maisha halisi. Akijadili dhana ya maigizo kabla ya ukoloni nchini Kenya, Ngugi anasema:

“Maigizo .... hayakuwa shughuli iliyojitenga. Mbali na kuwa aina ya burudani, yalikuwa njia ya kufunzia na pia shughuli iliyochukuliwa kwa dhati kama njia mojawapo ya kuyaendeleza maisha ya jamii”. (Ngugi 1986:37). (Tafsiri ya mtafiti).

Ukweli huu unabainika kupitia maigizo yanayotokea mahakamani. Hoja ya Okutoyi ya kutaka watoto waachiliwe ni ya kuburudisha hadhira licha ya kuwa suala linalohusika ni zito. Hali ya watoto na hata Okutoyi kushtakiwa ni funzo kwa hadhira inayoshuhudia kuwa uhalifu haufai.

### 3.2.2 Maneno na Vitendo vya Wahusika

Maneno na vitendo vya wahusika vimetumiwa kujenga hali ya uigizaji na papo hapo kuibua maudhui mbalimbali. Bauman, (1992) anasema kuwa kati ya sifa za maigizo ni kuwa matukio huandaliwa mapema kabla ya wakati wake wa kuigizwa.

Kabla ya Madoa na Isaya kwenda kumwibia Mzee Zakayo, wanapanga kwanza: Isaya anaeleza kuwa walipenya ndani ya msitu huku Madoa akiongoza njia. Kisha wakafika kwa Mzee Zakayo Wekesa.

“Hajarejea tangu alipokwenda matanga wilayani Bungoma”,  
alisema Madoa.  
“Kwa hivyo?”  
“Usiniulize maswali mengi, alaa!” Isaya anaeleza zaidi.  
“Akaniamuru nifuatane naye hadi nyumbani kwa Mzee Wekesa.  
Tukaenda pole pole hadi upande wa nyuma ya nyumba uliokuwa  
na dirisha moja dogo. Akaniambia kwa sauti ya chini nimbebe.  
Nikainama akanisimamia mabegani. Nikamnyanyua juu.  
Kisha akijinyoosha na kulifikia dirisha kwa mkono.  
Akalifungua. Akaniambia kwa sauti ya chini,  
“Usitoke hapa mpaka nirudi”. Akaingia ndani. Nikasikia akigusagusa  
vitu ndani ya nyumba.  
Akawa anafunga na kufungua sijui vitu gani.  
Punde si punde alirejea dirishani na kuniambia nisimame vizuri.  
Akashuka kwa kunikanyaga mabegani na kuniteremkia mgongoni.  
“Tayari?” nikamwuliza.  
“Ndiyo Alaa!”  
“Umeiba bwana?”  
“Madoa akajibu kwa hasira, “Wewe si ulitaka twende Amerika?”  
“Umemwibia Mzee Wekesa”, nikamwambia.  
“Si kitu bwana.”  
“Unasema kuiba si kitu”, Nikamwuliza.  
Madoa akajibu, “Tumeiba sote,”  
“Nani aliyekufunza haya yote?”  
“Mwamba”, akajibu. “Rafiki yangu Rock Mwamba.”  
“Tumefanya mengi pamoja.”  
(Uk. 26-27)

Katika maelezo haya, wahusika wamesema na kutenda mengi. Maneno na vitendo vyao vinatupa picha kamili ya mambo yanayotokea. Lugha

inayotumiwa ni ya kawaida. Hili laafikiana na uhalisia ambao hushikilia kuwa yafaa wahusika watumie lugha ya kawaida kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu.

Kupitia maneno, Madoa na Isaya wameulizana maswali, wameshangaa, wameagizana na kuhimizana. Pia wamekosoana kwa wizi wanaoutekeleza. Vitendo vyao vinavyoandamana na maneno na kuzua uigizaji ni kuwa; Madoa amesimama mabegani mwa Isaya, akanyanyuliwa akijinyoosha hadi katika dirisha, akalifungua, akaingia ndani. Baada ya muda anarudi, anashuka kwa kumkanyaga Isaya mabegani na kumteremkia mgongoni.

Mwandishi ametumia maigizo haya kubainisha maudhui ya uhalifu hasa wizi na matumizi mabaya ya watoto. Madoa anasema:

“Mwamba ... rafiki yangu Rock Mwamba.  
Tumefanya mengi pamoja.”  
(Uk. 27).

Maneno haya yaonyesha kuwa Mwamba ndiye aliyemfunza Madoa wizi.

Mfano mwingine unabainika katika maneno haya:

“Mwamba utatupeleka Amerika?” Madoa aliuliza kwa matarajio.  
“Hamna wasiwasi wowote”, alijibu Mwamba.  
“Mtakwenda popote mtakapo. Bora msibabaike na mkubali  
kufanya kazi.”  
(Uk. 33-34).

Maneno haya yaashiria kuwa Mwamba alikuwa akiwahusisha watoto katika uhalifu na kwa njia hiyo kukiuka haki zao. Baada ya Madoa na Isaya kukaa kwa Mwamba kwa siku mbili, mwenyeji wao alikuja jioni siku moja na kusema mambo ambayo Isaya hakuyaelewa vizuri.

“Leo usiku kuna kazi Buruburu ... umechoka au tutakwenda pamoja?”  
“Nimepumzika vya kutosha. Lazima twende”, alijibu Madoa.  
“Na huyu rafiki yako je?”  
“Isa bado mshamba hajui kazi”, alisema Madoa na kutikisa kichwa.  
(Uk. 34).

Haya pia yaonyesha kuwa Mwamba alikuwa akihusisha watoto katika uhalifu.

Madoa na Isaya wanagusia safari ya kwenda Amerika katika kauli hizi:

“... Basi Amerika utakwendaje, Madoa? Wajua huko ni mbali?”  
“Mimi ninajua namna nitakavyo kwenda”, alisema Madoa.  
“Penye nia pana njia. Kuna rafiki yangu ambaye atanipeleka”.  
“..... Na nikifika huko nitaitwa Michael Monday au Michael  
chochote na lotote”  
“Kwa nini ubadilishe majina tena?” Nikamwuliza.  
“Huko Makerani....”  
“Sema Ma-re-kanii,” nikamwambia.  
“Ndiyo Alaa!” Madoa akasema. “Lazima mimi pia nibadilishe jina.  
Huko kila mtu anaitwa Michael au kwa kifupi Mike.  
Rais wa huko ni Mike Tyson, Waziri wa Elimu anaitwa Michael  
Jordan, Waziri wa Afya anaitwa Michael Jackson, Makamu wa Rais ni  
Michael Johnson.”  
(Uk. 9-10).

Kupitia maneno haya, maudhui ya mkengeuko yanabainishwa hasa kupitia  
kwa Madoa. Anachukia kila chake cha asili na akifika Marekani anataka pia  
abadilishe jina lake. Hili ni tukio halisi ambapo watu wengi siku hizi hupania  
kwenda nchi za ng’ambo, na hasa Marekani kwa imani kuwa ni taifa  
lililostawi sana na lisilo na matatizo yoyote.

Kinaya ni kuwa Madoa anataka kuhamia nchi ambayo hata hawezi kutamka  
jina lake. Analitamka “Makerani”. Anapokosolewa na mwenzake, Isaya,  
anahamaki.

Larkin (1972:2) anasema kuwa wana uhalisia walisadiki kuwa lengo la  
mwandishi kwa jamii ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida

na kwamba ulimwengu atakaoumba mwandishi sharti uwe wa kweli au halisi.

Kupitia Isaya na Madoa, Walibora ametupa taswira kamili ya umaskini wao.

Isaya anasema;

“..... jina langu ni Isaya Yano. Mamangu huniita Isaya. .... nimekuwa nikiishi na mamangu tangu babu kufa. . sisi si matajiri.. nyumba yetu ina kuta za udongo. Imeezekwa kwa nyasi. ... ukiwa ndani ya nyumba yetu unaweza kuona mawingu yakikusanyika angani kupitia mashimo yaliyoko paani. ... mvua inyeshapo usiku mimi na mamangu hulazimika kuhamisha malazi hapa na pale nyumbani kutafuta pasipo vuja.  
(Uk. 5-6)

Isaya pia aeleza kuwa:

“Madoa pia alikuwa akichukia kwao. Alikuwa akiishi na mamaye .... Shamba lao lilikuwa kubwa kidogo kuliko letu. Hata hivyo, wao pia hawakuwa matajiri. Mamake alikuwa akiuza maandazi, chapati na sambusa katika soko la Sangura”.  
(Uk. 6-7).

Msanii wa kihalisia anafaa kuangazia maisha katika ngazi zote, za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kupitia maelezo haya, maisha ya kiuchumi ya Isaya, Madoa na familia zao yanatoa picha ya umaskini. Maudhui haya yamejitokeza kupitia kauli ya mhusika Isaya.

Msanii wa kihalisia huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Tatizo la umaskini katika *Ndoto ya Amerika* linabainika kupitia igizo hili. Isaya anasema kuwa siku moja asubuhi alipoamshwa na mamake kwenda shule alianza kulia:

“Unalia nini?”

“Sijaota juu ya Amerika.”

“Una wazimu?”

“Madoa aliniambia kuwa kila mtu anaota juu ya Amerika.”

“Mtoto wewe umerogwa?”

“... nilikwambia sitaki utembe na Madoa ana tabia mbaya.  
Nawe husikii. Umeanza kutembea naye tena. Eeh?”

Isaya anaendelea kueleza:

“Kisha mama alianza kunicharaza viboko kwa hasira ... nikaruka ghafla na kuelekea mlangoni. Mama akanifuata... alikuwa karibu kunichapa kingine, nikafikia mlango na kujitupa nje.”

“Isaya! Simama hapo! Aliniamuru. “Utakiona cha mtema kuni leo.”

Isaya anaendelea kueleza:

“Hakuna siku niliyowahi kumshinda mama mbio.

.... Nadhani kama si kuolewa mapema pengine mama angelikimbilia Kenya katika mashindano ya Olimpiki.

Nilitazama nyuma nikaona amenikaribia. ...

kisha nikasikia nyuma yangu kishindo kikubwa.”

Tifuu!” Nilipogeuka nilimwona

mama amelala chini.” (Uk. 14-15).

Kupitia igizo hili, tunagundua kuwa chanzo cha umaskini huenda kilichangiwa na mila ya ndoa za mapema. Anasema mamake aliolewa mapema. Hili linamaanisha hakuweza kusoma na kupata maarifa ambayo yangemsadia baadaye. Maudhui ambayo yamebainika hapa ni umaskini, ndoa za mapema na kunyanyaswa kwa watoto. Maudhui ya ushirikina na mkengeuko pia yamebainishwa pale mamake Isaya anapomwuliza iwapo amerogwa na pia wakati Isaya anasema kuwa kila mtu anaota juu ya Amerika.

Kupitia igizo hili, maneno na vitendo kadha vimebainika. Kwa maneno, mamake Isaya, amauliza, amemkemea amemwamuru, amemkanya. Kupitia vitendo, amemchapa, akamfuata, akamchapa tena, anamkimbiza, kisha anaanguka. Isaya naye amelia akaruka, akakimbia, akatazama nyuma na akamwona mamake ameanguka. Maneno na vitendo hivi vya wahusika ni

maigizo kamili yanayoweza kutazamwa kwenye jukwaa au filamu. Katika maigizo haya, mbinu ya taswira ama kuchora picha akilini mwa hadhira kwa maneno imetumiwa.

Mbinu ya chuku pia inabainika pale Isaya anaposema kuwa mamake angekimbia timu ya Olimpiki, anaaminisha mamake angeweza kukimbia sana; Isaya anasikia kishindo ‘Tifuu!’ mamake anapoanguka. Tanakali ya sauti imetumiwa katika maelezo hayo.

Maigizo kama haya pia yanajitokeza katika riwaya ya *Kiu* (1972) ya Mohamed S. Mohamed. Maneno na vitendo vya wahusika vinazua uigizaji ambao pia unaakisi uhalisi maishani. Ndoa ya Idi na Bahati haikuwa na furaha kwa sababu Idi alikuwa mlevi na pia alikuwa na jicho la nje. Kosa hili la pila linabainika baada ya Bahati kushauriwa na mjakazi wake, Mwajuma kufanya mpango ili amfumanie Idi.

Bahati anajificha kichakani karibu na nyumba yake akisubiri wakati ambapo Idi angewasili. Walipowasili, Bahati aliviona viwiliwili vya mke na mume vikitoka garini vimefungamana mikono viunoni. Muda si muda, akasikia sauti ya Idi, na mara akasikia kicheko cha mwanamke kikifuatia, kicheko kilichotiwa nakshi ya ulegevu wa kike, kilichochekwa kwa madhumuni.

Bahati anakasirika na kwenda kumkabili Idi. Alipomwita, Idi alikatiza starehe yake na kugeuka. “Kimekuleta nini huku?” alimkaripia, mkono wake mmoja ungali kiunoni mwa kile kisura. “Nani yule darl....?” kiliuliza kisura, sauti yake ikijikokota, yenye dharau, legevuni na nyororo.

“Huyu ndiye yule paka wangu niliyekuambia nafuga lakini ngojea ‘darl..... nitamwondoa sasa hivi’”.  
(Uk. 147-148).

Maneno na vitendo vya wahusika hawa ni mifano mizuri ya uigizaji unaorejelea mambo halisi katika jamii zetu.

### 3.2.3 Lugha ya Wahusika

Katika kazi za kihalisia, lugha huwa ni ya kawaida na hutumiwa na wahusika kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu. Wahusika katika *Ndoto ya Amerika* (2001) wametumia lugha inayozua hisia tofauti kwa wahusika wengine na kwa hadhira. Mifano hii yadhihirisha hayo:

“..... Huko Maakerani...”

“Sema Ma-rekanii”, nikwambia.

“Ndiyo Alaa! ... kila mtu anaitwa Michael. Rais wa huko ni Mike Tyson, waziri wa elimu anaitwa Michael Jordan...”

“Acha uongo, bwana.” (Uk. 10).

Isaya anapomkosoa Madoa, Madoa anakasirika na kudhani kuwa mwenzake amemdharau. Kauli zao nyingine zinazua hisia tofauti:

“... Hata liwe liwalo mimi nitakwenda Amerika.

Kwani wewe hujawahi kuota ndoto ya Amerika.?”

“Ipi?”

Hujawahi kuota umekwenda Amerika?”

“Bado”, nikamwambia Madoa.

“Ngoja tu utakapoota ndoto ya Amerika ndipo utaanza kutamani kwenda huko.” (Uk. 11).

Maneno ya Madoa yanazua taharuki na kumpa Isaya hamasa ya kujua maana ya ndoto ya Amerika. Anajiona kama mtu aliye na kasoro asipoota ndoto hiyo.

Maudhui ya mkengeuko yanabainika tunapoelezwa kuwa kila mtu nchini

alikuwa akiota juu ya Amerika. Maana ni kuwa watu wengi walikuwa na nafsi mbili, waliacha vitu vyao asili na kuthamini vya kigeni.

Isaya anapopigwa na mamake, anakimbilia msituni na huko anakutana na Madoa.

“Isa, hebu niambie kwa nini umekuja msituni?

Hata shuleni leo sikukuona”, akaniuliza.

“Ni mama amenichapa bila sababu”

“Hawa mama zetu nao wamezidi”, Madoa naye akaongezea.

“Na walimu nao ni *too much!*”

“Kwani kumetokea nini shuleni leo?” nikamwuliza Madoa.

“Leo mwalimu Njoroge aliniambia nisimame darasani niwaambie wanafunzi miji mikuu ya Tanzania, Uganda, Somalia, Ethiopia na Sudan”.

“Ukasema nini?”

“Nilimwambia Nakuru, Mombasa, Kitale, Naivasha, na Nyeri”.

(Uk. 22).

Maneno ya vijana hawa yanazua hisia tofauti kati yao na pia kwa hadhira.

Madoa anakasirika anapoambiwa kuwa Isaya alichapwa na mamake; Isaya naye anachekeshwa na majibu aliyotoa Madoa shuleni. Wote hawafurahii vitendo vya wazazi na walimu wao.

Hadhira nayo inapata mtazamo hasi kuhusu walimu na wazazi wa vijana hawa. Kupitia kauli za vijana hawa, maudhui ya maonevu na mateso ya watoto yamegusiwa. Mwandishi amechanganya ndimi na kutumia mbinu ya chuku kutubainishia maudhui. Kwa mfano, uzuzu wa Madoa umepigiwa chuku kupitia majibu anayoyotoa darasani. Hili pia laweza kuchekesha hadhira.

Isaya ama ‘Isa’ na Madoa wanatorokea Nairobi na kuelekea kwa Zablon Okutoyi ama ‘Rock Mwamba’.

Madoa anabisha mlango:

“Nani?” sauti ilinguruma ndani ya nyumba.

“Mimi ni Ninja”

“Ninja gani?” Ile sauti ya ndani ya nyumba ikanguruma tena.

“Ninja kutoka Cherangani”. (Uk. 30-31).

Maneno haya yanazua hali ya mshangao na taharuki. Isaya anagundua kuwa kumbe Madoa alikuwa na jina jingine. Anapoulizwa maana, anasema hilo lilikuwa jina lake la kazi. Hadhira inabaki ikijiuliza ni kazi ipi hiyo ambayo yahitaji kuwa na jina fiche. Maudhui ya uhalifu na matumizi yasiyofaa ya watoto yanaonekana hapa.

Msanii wa kihalisia huangazia maisha yalivyo pasipo kuathiriwa na huangazia maisha katika ngazi zote kama za kiuchumi na kijamii. Katika jamii ya *Ndoto ya Amerika*, inaonekana kuwa mfumo wa kijamii hauwathamini watoto ndipo wanaingizwa katika uhalifu. Jamii hii pia imeathiriwa na uhalifu.

Moja kati ya mihimili ya uigizaji ni kuwa mtendaji husawiri hali tofauti maishani mwa binadamu na namna anavyobadilika kitabia kutegema mazingira na miktadha tofauti. Hili labainika kupitia mhusika Madoa. Akiwa kwao Cherangani, tunamwona kama mtoto na pia mwanafunzi, lakini anapofika Nairobi, anabadilika kabisa. Anakuwa sasa si Madoa bali ni “Ninja”, yeye si mwanafunzi tena bali anafanya kazi; kazi ya wizi.

Lakabu anayojipatia inazua maswali mengi kuhusu tabia zake. Majibu ya Isaya anapokuwa kortini yanafurahisha na kuchekesha hadhira.

“Wewe Isaya Yano umeshtakiwa kuwa mnamo tarehe 2 Novemba mwaka huu ulipatikana ukishirikiana na mtu anayeaminiwa kuwa jambazi hatari. Unakiri au unakataa shtaka?”

“Ni Madoa aliyenidanganya kuwa ana rafiki atakayetupeleka Amerika. Ndiye aliyenileta hapa Nairobi kwa rafiki yake huyu.” (Uk 42-43)

Matamshi haya yanamfanya hakimu kutabasamu na wengine waliokuwa mahakamani kucheka. Ingawa jambo linalogusiwa ni zito, hadhira na wahusika wanalipokea kwa njia ya mzaha.

Siku ya kutolewa hukumu mahakamani, maneno yanayosemwa huko yazua hisia tofauti. Isaya anasema kuwa walipofika mahakamani, hawakumwona ‘Rock Mwamba’ au Okutoyi ambaye alikuwa amewekwa rumande katika gereza la Kamiti. Kisha akajaribu kumpokonya askari jela bunduki ili atoroke tena. Hakimu akamuuliza afisa huyo wa magereza.

“Kwa hivyo Okutoyi yuko wapi?”

“Alipigwa risasi na kuuawa na askari jela.” (Uk.46)

Isaya anasema kuwa alishtushwa sana na maneno hayo na alipomtazama Madoa akaona machozi yakimtoka machoni, huku akitetemeka. Suala la uhalifu ndilo linalogusiwa hapa na tunaona kuwa tamko la afisa wa magereza linazua hisia mbalimbali. Isaya anashtuka ilhali Madoa analia na kutetemeka. Hizi ni hisia za kawaida hasa mtu anaposikia habari za kugutusha.

Katika riwaya ya *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi, tunashuhudia wahusika wanaotumia lugha ambayo inazua hisia mbalimbali na pia kuzua hali ya uigizaji. Siku moja, Dzombo alikuwa amemwambia nduguye kuwa hali ya ufukara wao ilitokana na kunyanyaswa na tajiri wao. Kwa kuwa ndugu huyo

hakuwa akijua maana ya kunyanyaswa, basi yeye keshoye alimwendea tajiri wao na kumbwambia:

“Hebu nami nikunyonye.”

“Eti wasemaje?” tajiri akanwuliza kwa mshtuko.

“Nimeambiwa kwamba nikikunyonya, basi nami nitakuwa na hali ya kuvutia kama yako”, akajieleza.

“Nani mwenda wazimu gani ambaye amekwambia upuzi huo?”

“Ni ndugu yangu Dzombo”. Maneno haya yalimkasirisha sana tajiri wao. Baadaye Dzombo aliitwa na akaonywa asiendelee na uchochezi.

Siku iliyofuata, Dzombo alipata barua ya kumfuta kazi

(Uk. 14-16).

Katika *Mui Huwa Mwema*, (1978), Bw. Maarufu anaandaa karamu ya kumshukuru Kachero Senge ambaye alikuwa ameyanusuru maisha ya binti yake, Mashaka. Katika kuwahutubia waliohudhuria, anasema;

“..... Nimekualikeni karamu hii, ndugu zangu, kukuonyesheni mgeni wangu mhisani wangu ambaye amenitenda wema usio kifani kwa kuyanusuru maisha ya binti yangu, Mashaka, na kumrejesha kwangu. .... Tafadhali usinivunje, pokea hundi hii ni zawadi yako hundi ya shilingi 5,000. Pesa hizi zikakufaa huko uendako.”

Senge naye anaposimama anasema:

“Kuyanusuru maisha ya binti yako ni moja katika kazi zangu. .... Mbele ya wote kwa moyo mkunjufu na nia safi, nimeikubali zawadi ulionipa na mimi vile vile nakupa shukrani kuu kwa zawadi hiyo.” (Uk. 41).

Lugha inayotumiwa na wahusika hawa inatoa picha ya uigizaji na iliafikiana na mambo waliokuwa wakirejelea. Ni jambo la kawaida kwa mtu kumshukuru mwenzake anapotendewa wema. Majirani walioshuhudia haya wanaweza wakachukuliwa kama hadhira inayoshuhudia mchezo jukwaani.

### 3.2.4 Mandhari

Tukichukulia mandhari kuwa ni mazingira ya utendaji wa kazi ya fasihi, kuna mifano ambayo inabainika katika *Ndoto ya Amerika* na ambayo imetumiwa na waigizaji ili kudhihirisha maudhui kadha. Kwa mujibu wa Bauman, (1992) kati ya mambo muhimu yanayoashiria uigizaji ni vitu kama jukwaa lililoinuliwa. Kwa maana hii, mandhari yanaweza kuchukuliwa kama jukwaa linalotumiwa kwa kuigiza.

#### 3.2.4.1 Akilini

Isaya alikimbilia msituni baada ya kupigwa na mamake. Aliketi chini ya mti na kuanza kufikiria juu ya masaibu yake. Mara usingizi ulimshika na akaanza kuota ndoto.... Anaeleza:

“Nilikuwa ninaendesha gari kubwa. Gari kubwa kuliko la mbunge wetu.

Gari lenye rangi nyeusi. Madoa alikuwa ameketi karibu nami. Alikuwa ananionyesha njia. Kulikuwa na magari mengi sana barabarani kama zilivyo nyota angani wakati wa usiku”.

“Hapa ni wapi? Nikwamwuliza Madoa.

“Hapa ni Cairo”, akajibu.

“Nikamwambia, “sidhani ni Cairo. Kumbuka sasa tuko Amerika. Cairo ni mji mkuu wa Misri huko mbali barani Afrika”.

“Kila siku unapenda kujifanya unajua. Basi kwa nini unauliza kama wajua jawabu”, akasema Madoa kwa hasira.

Isaya anaeleza zaidi:

“Kisha tukaona mbele yetu jengo moja lililoandika ‘New York’. Nikaelewa kuwa tuko katika mji wa New York, nchini Amerika. Nikamwambia Madoa asome maandishi hayo”.

..... Madoa alikasirika zaidi na kusema kwa sauti kubwa,

“Hebu simamisha gari nishuke basi.

Sitaki kusafiri na mtu anayejifanya anajua sana!!

Isaya anaeleza zaidi:

“Akaanza kufungua mlango huku gari linakwenda mbio.  
Nikafunga breki ghafla. Gurudumu moja likatoka kwenye gari na  
kupaa angani kama ndege. Madoa akabofya kifaa fulani kwenye  
gari kisha gurudumu hilo lililochomoka likajirudisha lenyewe.  
(Uk 16-17).

Maelezo ya Isaya yanatuchorea picha akilini mwetu. Hapa akili ni kama  
jukwaa ambako matukio haya yanatendeka. Hali ya gurudumu kuchomoka  
kutoka kwenye gari na tena kujirudisha yaweza kuchukuliwa kama filamu za  
kifantasia au filamu sisimuzi. Maudhui ya mkengeuko yanabainika wakati  
vijana hawa wanapoacha bara lao na kwenda Marekani.

Isaya anasimulia zaidi,

“..... Tukashuka na kuingia katika hoteli moja kubwa. Ndani  
kulikuwa na mabomba ya soda, chai, kahawa na vinywaji  
vingine mbalimbali.  
Ukifungulia tu bomba hilo vinywaji hivyo vinabubujika kama  
maji katika mto.... Niliona chakula nacho kinajipika na kujileta  
mezani chenyewe. Nikaona sahani zinajiosha na kujikausha  
zenyewe.”

Wanaanza kuongea:

“Madoa! Hii ndiyo raha mstarehe!  
“Wewe usiniite Madoa.”  
“Kwani wewe si Namasake Madoa  
Michael Monday.”  
“Wewe ndiwe Michael Chochote au lolote, au sio?  
“Ndio Alaa!”

Isaya anasema kuwa alipomwambia Madoa kuwa alitaka kulala; Madoa  
alishauri akiite kitanda.

“Kitanda njoo,” akasema na punde si punde kitanda  
kikaja.....  
(Uk.17-18)

Ghafla Isaya aliamka. Ndoto ya Isaya kuhusu safari yao ya Amerika ni mfano wa maigizo yanayotoka akilini mwake. Maelezo yake hatua kwa hatua yanachora picha akilini mwa hadhira ambayo pia wanaweza kufuata mchezo unavyoigizwa kutokana na maneno na vitendo vya wahusika.

Maudhui ya mkengeuko yanabainishwa kupitia Madoa. Anakataa jina hilo ambalo anasema ni la Kenya na kutaka aitwe Michael Monday. Ugizaji kama nadharia hushikilia kuwa yafaa mwigizaji asawiri hali tofauti maishani mwake na kuonyesha anavyobadilika kutegemea mazingira. Kipengele hiki kimeonekana kupitia Madoa anayekataa jina lake la asili akidai ni la huku Kenya. Anataka aitwe Michael kwa sababu sasa yuko Amerika.

Kwa upande mwingine, maelezo ya Isaya kuhusu safari yao na namna wanavyoongea na Madoa yanaweza kuchukuliwa kama maelezo au maagizo ambayo aghalabu huandamana na filamu ama michezo ya kuigiza.

Maudhui ya starehe zinazodhaniwa kupatikana nchi za ng'ambo yamepigiwa chuku kupitia vinywaji, vyakula na vitanda vinavyojileta vyenyewe. Kupitia maelezo ya Isaya, Mwandishi pia ametumia maswali ya balagha, kinaya, kejeli, tashbihi na tashihisi katika kuendeleza maigizo haya na kufafanua maudhui ya mkengeuko.

Maigizo mengine yanayotokea akilini yanabainika Isaya alipoachwa nyumbani mwa Rock Mwamba. Mwamba na Madoa walikuwa wameenda

kuiba katika mtaa wa Buruburu. Isaya anasema kuwa alipoachwa, alianza kusinzia na kulala. Akaota juu ya Amerika tena .

Anaeleza kuwa ... “Niliota nimekuwa Rais wa Amerika. Watu wananishangilia huku nikipita katika barabara za New York kwa gari moja kubwa. Dereva wangu alikuwa mzungu. Nikawapungia watu mkono nikiwa nimesimama juu ya gari. Nikaingia katika uwanja wa michezo. Watu karibu “kupasuka kwa sababu ya kufurahi kuniona.”

Nikakaribishwa na kuanza kuhutubu: “Wananchi watukufu wa Marekani, kama mjuavyo hii ni nchi ya starehe. Hakuna umaskini. Hakuna mtu asiyekuwa na friji. Hakuna mtu asiyekuwa na gari. Hakuna mtu asiye na ndege pamoja na uwanja wa ndege. Hakuna mtoto anayecharazwa viboko na mwalimu ... . Wenye hekima wamesema kwamba:

“Ndoto ni mwana wa udanganyifu.” Lakini hali hapa Amerika au Marekani si ndoto bali ni kweli...  
(Uk.35).

Katika igizo hili, maudhui yanayogusiwa ni kama maendeleo yafikiriwayo yapatikana nchi za ng'ambo na haki za watoto. Mwandishi ametumia takriri na chuku kubainisha maudhui hayo.

Maigizo kama haya yanaonekana katika riwaya ya *Kiu* (1972). Idi alikuwa amemwalika Bahati wakutane kinarani ili wazungumzie mambo yaliyohusu urithi baada ya wao kutalikiana. Lakini, usiku wa kuamkia siku ya miadi, Bahati aliota ndoto inayohusu kufukuzwa na pini kubwa. Alikuwa awali

ameota ndoto kama hiyo; lakini safari hii, aliongezeka Mwajuma, mwenye mbawa mfano wa malaika, aliyeteremka na kuliangamiza lile pini.

“Haya!” akamwambia, lile pini lilikuwa limevunjika chini yao vipande kururi. “Sasa pumzika, nishakuondolea adui!” Lakini mara akamwona yule Mwajuma akumfukuza yeye. Alizindukana yumo mbioni. (Uk. 157-158).

Ndoto hii ni mfano wa mchezo unaotokea akilini mwa Bahati na iliashiria maangamizi yaliyomsubiri. Ingawa Mwajuma anajidai kuwa anamshauri Bahati, yeye ndiye aliyechangia kuvunjika kwa ndoa ya Bahati, Bi. Cheusi akimtafuta bintiye kwa kukosa kurudi nyumbani alipoenda kukutana na Idi. Mwandishi ametumia taashira na taharuki katika kisa hiki. Ni jambo la kawaida kwa watalaka kutotakiana mema maishani. Huenda Idi alimwangamiza Bahati ili asifiche siri juu ya utajiri walioupata kwa kumwambia Mzee Mwinyi.

#### **3.2.4.2 Nyumbani**

Maigizo mengine yanatokea nyumbani mwa Okutoyi ama “Rock Mamba.” Wizi wao unapokosa kufaulu, polisi wanawakamata na kuwaleta hadi kwa Mwamba ili kufanya msako. Isaya anaamshwa ghafla, kisha anaeleza; “chukua hivyo vitambulisho,” nilisikia sauti ya kike ikiamrisha. “Kagua hizo noti.” Nikasikia sauti nyingine ya kiume ikisema, “hawa ndio majambazi wanaohangaisha watu hapa Kenya.”

Isaya anasema, alikimbia na kujificha chini ya kitanda. Akasikia askari hao wakiingia chumbani humo na kuwasha taa ya umeme wakatafuta kila mahali kisha wakapindua kitanda alichokuwa amejificha chini yake.

“Mamaaa! Waaa! “Nikapiga makelele  
“Unafanya nini hapa ndani?” askari yule mwanamke akaniuliza.  
Isaya anaeleza jinsi mambo yalivyoendelea ... Alinikamata mguu,  
akanivuta na kunirusha kando kama karatasi.”.....  
“Eh! Ona jinsi bunduki zilivyojaa hapa.” Akashangaa .  
“Tumekutafuta siku nyingi Okutoyi. Leo umepatikana”,  
mwingine alisema.  
(Uk. 37-38).

Kupitia maigizo haya, maudhui ya uhalifu na mateso ya watoto yanabainika. Maneno na vitendo vya wahusika vinatoa picha kamili ya maigizo. Katika uhalisia, mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana. Maudhui na matukio kwa kiasi kikubwa yanatakiwa kulingana na yale ya jamii inayorejelewa. Suala la uhalifu ni la kawaida katika mazingira yetu.

### 3.2.4.3 Kortini

Baadhi ya sifa mahsusi za maigizo kwa mujibu wa Bauman (1992) ni kuwa:

- i. Matukio huandaliwa mapema kabla ya wakati wake wa kuigiza.
- ii. Huwa na mwanzo na mwisho maalum au unaotambulika.
- iii. Hutendwa katika sehemu maalum iliyotengwa mahsusi kwa shughuli hiyo.

Sifa hizi zinajitokeza katika maigizo yanayotokea kortini.

Katika korti, kila mmoja alipoitwa angeitikia kisha kuhukumikiwa kisha karani aliita”Zablon Okutoyi!”  
“Ndio Afande” “..... Umeshtakiwa kwa makosa manne....”  
“Afande kwanza naomba hawa watoto waachiliwe maana hawaelewi kinachoendelea.”  
“Huwezi kuiambia mahakama la kufanya wewe sema kama unakubali au unakataa mashtaka yako.”  
“Nakataa.” “Utapelekwa rumande hadi kesi yako itakaposikizwa tena baada ya wiki mbili.” (Uk.40-41).

Maigizo haya yanatokea katika korti baada ya maandalizi ya mapema. Kabla ya Okutoyi kusomewa mashtaka, lazima uchunguzi ulikuwa umefanywa na mashtaka kuandaliwa.

Kesi hiyo pia imekuwa na mwanzo maalum pale Okutoyi anaposomewa mashtaka na mwisho maalum ambapo Okutoyi anapelekwa rumande. Maigizo haya pia yametokea katika sehemu maalum iliyotengwa mahsusi kwa shughuli hiyo na sehemu hiyo ni kortini.

Katika uigizaji, mtendaji anafaa azisawiri hali tofauti maishani mwa binadamu na jinsi anavyobadilika kitabia kutegemea mazingira na miktadha tofauti. Akiwa, mahakamani, Rock Mwamba anaonyesha unyenyekevu. Anapoitwa, anaitika “Ndio Afande”. Jambo hili linatofautiana na maneno ambayo awali, Isaya alikuwa ameambiwa na Madoa.

“Usimchezee Mwamba. Mwamba ni Mwamba kweli.” (Uk. 32). Picha inayochorwa hapa kumhusu mwamba ni kuwa ni mtu asiyeogopa chochote na jasiri lakini afikapo kortini ananywea.

#### **3.2.4.4 Mada**

Katika *Ndoto ya Amerika* (2001) kuna masuala ambayo yamechangia kuwepo kwa migogoro kati ya wahusika na kwa njia hiyo kuzua maigizo

“Mimi nitakacho sasa ni kwenda Makerani.”

“ Unamaanisha Marekani”

Eeh! Uite utakavyo mimi ninakwenda huko.”

“ Basi tutakwenda pamoja.”

“Hapana ! siwezi kwenda huko na mtu anayependa kuniaibisha.”

(Uk 23).

Madoa anataka kwenda Marekani lakini hajui hata kutamka jina hilo, anapokosolewa, anahamaki. Maudhui ya mkengeuko na uzuzu yamegusiwa katika maigizo haya. Madoa na Isaya wanakorofishana tena wanapozungumzia suala la wizi. Baada ya Madoa kumwibia Mzee Zakayo Wekesa pesa zake:

“Umemwibia Mzee Wekesa,”  
“ Si kitu bwana”  
“Unasema kuiba si kitu?” nikamuuliza  
Madoa akajibu “ Tumeiba sote”  
“Nani alikufunza haya yote?”  
“Rafiki yangu Rock Mwamba. Tumefanya mengi pamoja”  
(Uk.27).

Kupitia maneno na vitendo vyao, maudhui ya wizi yanajitokeza. Inabainika pia kuwa Madoa ni mwizi wa siku nyingi. Anapokosolewa na Isaya kuhusu kitendo hicho, yeye anakiona kama ni kitu cha kawaida. Isaya anazua ukinzani kati yake na hakimu anapokuwa mahakamani kutokana na msamiati unaotumiwa na hakimu.

“Isaya Yano!”  
“Ndio afande!”  
“Wewe Isaya Yano umeshtakiwa kuwa mnamo tarehe 2 Novemba mwaka huu ulipatikana ukishirikiana na mtu anayeaminiwa kuwa jambazi hatari. Unakiri au unakataa shtaka?”  
“Ni Madoa aliyenidanganya kuwa ana rafiki atakayetupeleka Amerika. Ndiye aliyenileta hapa Nairobi kwa rafiki yake huyo.”  
“Kwa hiyo unakubali makosa?” aliuliza tena hakimu  
“Naomba msamaha afande.”  
“Una *Malilio* gani ? akauliza.

Isaya anasema kuwa hakupenda neno *malilio* na mpaka leo anaamini kuwa neno hilo si Kiswahili sanifu. Kwa vyovyote vile anasema alijikuta ameanza kulia.

“Wewe mtoto hatutaki kilio. Tunataka malilio!”  
Hakimu akaamrisha.  
(Uk. 42-43)

Katika maigizo haya, kuna shida ya mawasiliano kati ya Isaya na hakimu kutokana na matumizi ya neno “malilio.” Isaya anapoanza kulia mahakamani, hadhira inapata hisia tofauti. Wao wanacheka, lakini hakimu anakasirika. Maudhui ya haki za watoto yanajitokeza kwa sababu Isaya alipelekwa kortini kwa hatia ya kushirikiana na Mwamba ambaye ni mtu mzima. Mwamba anakiuka haki za Isaya kwa kumshirikisha katika uhalifu. Ni jambo halisi katika mazingira yetu kwa watu wazima kukiuka haki za watoto kwa kuwatumia kwa mambo kama uhalifu wa aina mbalimbali. Wengine pia huwaiba na kuwauza watoto. ‘Rock Mwamba’ ni mfano wa watu kama hao.

Katika riwaya ya *Kiu* (1972), suala la mapenzi linazua migorogoro kati ya wahusika na kwa njia hiyo kutoa picha ya uigizaji. Ingawa Bahati alimpenda Idi kwa dhati, Idi kwa upande wake alikuwa akimtumia kama chombo cha kupata utajiri kutoka kwa Mzee Mwinyi. Siku moja Bahati alimtumia Idi barua ya utani:

Idi,  
Usistaajabu nikikuambia ya kuwa hivi sasa niko kitandani kwa Mwinyi, tunapanga siku ya arusi yetu ya kikweli. Si ruhusa kutuingilia kwani tuna hiari yetu. Nakuonya kwa salama yako mwenyewe, kuwa mipango yako iwe imekoma bada ya kuipata barua hii. Nisalimie fulani.

Wa nafsi yangu,  
Bahati.

Tunaambiwa kuwa barua hiyo iliwasha moto moyoni mwa Idi na kumchemsha kwa hasira. Alianza kuhangaika chumbani huku akifikiri. Alikuwa amekunja ngumi na kumfokea mtu asiyemwona. Aliona bora kufa..... Lakini kwa nini afe yeye na hali mkosa abakie duniani akistarehe? Bora afe Bahati, wafe wote,

na Mwinyi pia naye afe! Alipiga kelele huku akishindilia risasi katika bastola yake ya magendo.....

Mlango ulikuwa wazi tangu mtoto aliyeleta barua kutoka. Basi wakati Idi alipokuwa akifoka, mara aliingia msichana akapita moja kwa moja hadi chumbani na kusimama mbele yake. Idi alishtuka na bastola yake mkononi. Alimtazama yule msichana, naye msichana akamkazia macho Idi. Kitambo kikapita. Wakaanza kusemezana kwa macho:

“Bahati wewe? .....Umekuja?” macho ya Idi yaliuliza.

“Naam, mimi Bahati, nimekuja”, macho ya yule msichana yalimjibu.

“Umekuja nikuue?”

“Nimekuja unipende”.

“Nikupende?” umeandika wewe ni wa nafsi yako, na Mwinyi....?

“Mimi na nafsi yangu ni wako. Wako, mali yako, milele!”

Kufikia hapo, Bahati hakuweza kuzuia kile kicheko kilichokuwa kikimsonga moyoni; kilipasuka ghafla, kikatawanyika na kuvuma chumbani mwa Idi. Idi alitupa macho chini kuitazama ile bastola aliyoshika, na vidole vyake vikaikataa, ikaanguka miguuni mwake..... sasa akajua kuwa yote yalikuwa ni mzaha tu (Uk. 58-60). Mbinu za kinaya, taharuki na tashihisi zimetumika hapa.

### 3.3 Kiishilio

Sura hii imetoa maelezo ya jumla kuhusu kijiriwaya cha *Ndoto ya Amerika* (2001). Matukio muhimu kutoka mwanzo hadi mwisho yamegusiwa.

Sura pia imeshughulikia uigizaji na uhalisi kama nyenzo za maudhui katika kijiriwaya hiki. Vipengele vya maigizo vilivyorejelewa ni sifa za wahusika, maneno na vitendo vya wahusika hao, lugha ambayo ilitumiwa na wahusika,

mandhari ya uigizaji na hatimaye mada zilizoshughulikiwa na wahusika katika uigizaji wao. Haya yalijadiliwa kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia na ya uigizaji. Isisahaulike pia kuwa matukio mengi ambayo yanaweza kuigizika aghalabu huwa na uhalisi fulani kwa sababu yote hutokea katika mazingira ya kawaida tuliyoyazoea.

Sura inayofuata ni sura ya nne. Katika sura hiyo, maelezo ya jumla kuhusu riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003) yametolewa. Sura pia imejadili namna Walibora alivyotumia maigizo kama njia kuu ya kueleza maudhui katika riwaya, na jinsi maudhui hayo yanavyoakisi uhalisi unaopatikana katika mazingira yetu.

## SURA YA NNE

### MAELEZO YA JUMLA JUU YA RIWAYA YA *KUFA KUZIKANA*

(2003)

#### 4.0 Utangulizi

Sura hii imetoa maelezo ya jumla kuhusu riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003) na kujadili namna Walibora alivyotumia maigizo kama njia kuu ya kufafanua maudhui yanayopatikana katika riwaya na jinsi maudhui hayo yanavyoakisi ukweli unaopatikana katika mazingira yetu.

Hii imefanyika kwa kuainisha vigezo mwafaka vya maigizo na uhalisia na kuonyesha jinsi ambavyo mwandishi amevitumia kufanya maudhui yake yaeleweke vyema kwa hadhira. Haya yamefanywa pia kwa kuzingatia swala pamoja na malengo ya utafiti. Hatimaye, kiishilio cha sura hii kimetolewa mwishoni mwa sura.

#### 4.1 Maelezo ya Jumla Kuhusu Riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003)

Riwaya hii ina jumla ya kurasa mia mbili na thelathini na moja na sura ishirini na tano. Matukio katika riwaya yameelezwa kwa kutumia nafsi ya kwanza katika hali ya umoja. Kwa kiasi fulani tunaweza kusema kuwa riwaya hii ni kama tawasifu kwa sababu ni kama Walibora anaelezea maisha yake. Riwaya hii pia inaweza kuwa mfano wa bunilizi ya kiushabihikweli kwa sababu inasimulia mambo yanayofanana na ukweli, ina maelezo ya kibinafsi na mambo yanayoelezwa ni kama yamechopolewa kutoka katika maisha halisi.

Katika riwaya hii, Walibora anaeleza maisha ya vijana wawili, Akida Sululu na Tim Mapisi ambao walikuwa na urafiki wa dhali, urafiki wa kina, urafiki wa kufa kuzikana licha ya tofauti walizokuwa nazo za kikabila. Akida alikuwa Mkanju ilhali Tim alitoka kabila la Wakorosho. Ingawa tofauti za kikabila zilisababisha vita na vifo katika wilaya ya Korosho, hayo hayakuathiri uhusiano wao. Kilele cha uhasama wa kikabila kilifikiwa wakati babake Tim, Bwana Zablon Mapisi alipomwua babake Akida, Bwana Sululu, ingawa walikuwa majirani. Kitendo hiki, kilimfadhisha Zablon na hatimaye akijitia kitanzi.

Tim na Akida walikuwa wakisaidiana kwa njia mbalimbali katika nyakati mbalimbali. Shuleni, Tim alikuwa akimhami Akida dhidi ya wanafunzi wachokozi. Baada ya kutia fora katika mtihani wa kitaifa, Tim pia alimpokea Akida jijini Tandika alikoenda kutuzwa na Waziri wa Elimu nchini. Vile vile alimtembeza sehemu muhimu mjini na kumfunza mengi yanayohusiana na mji.

Baada ya ndoto ya Akida ya kuendeleza masomo yake kutofaulu, aliamua kuishi na Tim na walipokuwa wakiishi pamoja, urafiki wao ulipitia mitihani mingi, lakini wakaishinda yote. Kwanza, Bwana Samson Tungu, mjombake Tim na pia mwajiri wake alimfuta kazi kwa sababu ya mpwa wake kuishi na Mkanju. Dadake Tim alimtusi Akida kwa sababu za kikabila na hata kudai kuwa Akida alitaka kumnajisi.

Baada ya kupoteza kazi, ilimbidi Tim kuhamia mtaa duni wa Falkland kutoka mtaa wa Shauri Moyo walikoenda kufanya kazi za sulubu na Akida ili kujitunza. Akida alitiwa korokoroni kwa kesi ya ‘mauaji’ na Tim aliendelea kumfadhili. Alipoachiliwa, waliendelea kuishi pamoja hadi wakati maisha ya Akida yalipoponzwa na genge la vijana wanne Wakorosho. Walitaka kumwua Akida kwa sababu yeye alikuwa Mkanju na pia kwa sababu Akida alikuwa amemjeruhi baba yao, Tito Tembo miaka mitatu iliyopita.

Kutokana na hali hii ya dharura, Tim na dadake Tamari walitumia ujanja na kuyaokoa maisha ya Akida. Akida aliamishwa usiku hadi mtaa wa Mama Nasambu, kisha mtaa wa Tiwani alikojificha kwa takribani wiki tatu. Wakati huo, Tim alikuwa akimtafutia cheti cha kusafiria hadi nchini Canada.

Awali, Akida pia alikuwa ameokoa maisha ya Mkanju mwingine aliyeitwa Tom. Babake Tom, Mzee Mangala alikuwa ameuliwa katika vita vya kikabila na Tom akaamua kwenda kumzika mashambani huko Baraki. Baada ya mazishi, kundi la Wakorosho lilimvamia Tom na kumpiga hadi akawa mahtuti na walidhani kuwa tayari alikuwa amekufa. Askari na watu wengine waliomsindikiza Tom kutoka jijini Tandika walitoroka maksudi na kumwacha Tom katika genge la wauaji. Akida ndiye aliyetumia ujanja hadi Tom alipofikishwa hospitalini na kutibiwa. Kutokana na kisa hiki, Tom aliamua kulipa hisani aliyofanyiwa na Akida. Baada ya kupona Tom aliuza vitu vyake vyote na akahamia Canada. Alipokuwa huko alimfanyia Akida mipango na kumfadhili ili aende akasomee huko na kuepukana na shida za nchi ya Kiwachema. Riwaya hii inafikia ukingoni wakati Akida anapopanda ndege

kuelekea Ontario, Canada baada ya kuagwa na Tim, dadake Tamari, na mchumba wake Tim, Pamela. Tunaachwa katika hali ya taharuki.

#### 4.2 Maigizo na Uhalisi kama Nyenzo za Maudhui katika Riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003)

Sehemu hii inahakiki namna Walibora alivyotumia maigizo kuwasilisha maudhui yanayoakisi uhalisi katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003). Hayo yanaelezwa kwa misingi ya nadharia za uigizaji na uhalisia.

Msanii yeyote anapoitunga kazi yake huwa ana lengo fulani kwa hadhira. Njogu na Chimera (1991:21) wamesema kuwa maudhui ni jumla ya mawazo mapana yanayoshirikishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelea. Ubunifu wa mwandishi na uwezo wake wa kuteua mbinu mwafaka za lugha, ndivyo vifaa vinavyomwongoza katika kuwasilisha ujumbe wake. Vile vile, mwandishi atungapo kazi yoyote ya fasihi huwa na lengo maalum. Ni katika lengo la mwandishi ambapo maudhui huingizwa. Mambo haya mawili hayana mpaka mkubwa kwa sababu, maudhui huchangia katika kuunda dhamira kuu ya kazi ya fasihi.

Maudhui katika utungo wowote wa fasihi hurejelea kitu, mtu, jambo au tukio. Pia hurejelea sifa, mahali au hali ya maisha inayozungumziwa. Syambo na Mazrui (1994) wanasema kuwa maudhui yanaweza yakawa ya kuonya, kukashifu, kutahadharisha, kuburudisha, kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo, miongoni mwa mambo mengine. Kwa hivyo, maudhui yanaweza kujitokeza kama lengo la mwandishi na ujumbe alionao kwa wasomaji wake. Nadharia

ya uhalisia na ya uigizaji zimeelezwa katika sura ya kwanza na ndizo zitakazozingatiwa katika uhakiki huu kwa mujibu wa Qusby (1988) na Bauman, (1992).

Vipengele vya maigizo ambavyo vimezingatiwa katika uhakiki huu ni tabia za wahusika au namna mwandishi alivyoeleza sifa zao; maneno na vitendo vya wahusika hao, lugha ambayo wahusika wanatumia katika mawasiliano yao na namna wanavyoitumia, mandhari ya matukio, muktadha ambamo matukio fulani yanatendeka, hadhira pamoja na mada au jambo linalosababisha mgogoro.

Ingawa kunavyo vipengele vingine, vipengele vilivyotajwa vimebainika zaidi katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003) na kuifanya riwaya hii kubainika zaidi kama maigizo kuliko masimulizi ya kinathari. Hili linaafikiana na swala pamoja na malengo ya utafiti huu.

#### **4.2.1 Tabia ya Wahusika**

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao hufanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa wahusika hutegemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia huwasawiri wahusika kwa namna inayokaribiana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida (Wamitila, 2003).

Katika *Kufa Kuzikana* (2003) kuna wahusika ambao kutokana na sifa ama maelezo ya mwandishi kuwahusu, kunajengeka taswira katika akili za hadhira.

Tunaweza kuchukulia wasomaji hao kama hadhira inayotazama mchezo wa kuigiza unaotokea akilini mwao huku akili ikiwa kama jukwaa la kuigizia.

Baadhi ya wahusika pia wamepewa majina yanayoafikiana na hulka zao na haya yanazua uyakinifu unaoweza kukubalika katika maisha ya kawaida. Baada ya kuwa miongoni mwa wanafunzi watatu bora katika mtihani wa darasa la saba nchini, Akida anaelekea jijini Tandika ili kutuzwa na waziri wa elimu. Kwanza anakaribishwa na rafikiye Tim na maongezi yao yanakuwa hivi:

“Hongera ‘shemeji’ kwa kushinda mtihani.”

“Nimehongera”

“Mimi nilijua lazima utautetemesha ulimwengu. Una rundo la vipawa.”

“Wapi bwana!”

“Wadhani ni jambo dogo kuwa miongoni mwa watatu bora taifa zima?”

Sasa taifa zima watu wanajua Akida Sululu ni nani. Utasoma uwe Profesa wa Maprofesa. Si kama mimi. Masomoni nilikuwa mbumbumbu nisokuwa na kumbukumbu.....”

(Uk. 15).

Kupitia dondoo hili, tunagundua kuwa Akida alikuwa mwerevu lakini asiyependa kujisifu. Ni mtu wa matao ya chini. Kwa upande mwingine, tunaona kuwa Tim hana kinyongo, ni mchangamfu, mkweli na pia hupenda kupiga chuku. Anasema pia kuwa shuleni hakuwa mwerevu.

Kawaida ya maisha ni kuwa mtu habarikiwi na vitu vyote. Ingawa Akida alikuwa mwerevu, hakuendeleza masomo yake kwa sababu ya umaskini wa wazazi wake. Alikuwa akafadhiliwa baadaye na Tom. Kwa upande mwingine tunaona kuwa japo Tim hakuwa mwerevu shuleni, alikuwa akaajiriwa kazi na ndiye anayeishi na Akida alipoenda jijini Tandika.

Katika dondoo hili, kupitia wahusika hawa Walibora ametueleza maudhui ya umaskini, ufisadi na kupotea kwa vipawa vya watu fulani kutokana na umaskini.

Mbali na kutuzwa, Akida pia alikuwa ametumwa na babake kwenda kumfuatilia mswada wake uliokuwa umekawia kuchapishwa na shirika moja. Shirika liliitwa, 'Hatubagui Publishers'. Kuhusu meneja wake tunaeleza kuwa "... alikuwa mwanamume mmoja wa makamo, mwembamba, aliyevalia miwani. Alikuwa hana ubaguzi hasa. Alitupokea kwa mawili-matatu hata kabla ya kutujua sisi nani. Hakuwa na vikwazo vya kumwona. Nilipojitambulisha kwake alionyesha msisimko mkubwa".

Akida na meneja huyo wanaendelea kuongea,

"Baba ataka ajue diwani yake itachapishwa lini?"

"..... Lo! Hajapokea kifurushi chetu bado?" aliniuliza meneja.

"Kipi?"

"Diwani ya Mzee Sululu tuliichapisha miezi sita iliyopita.

Tulimtumia nakala zake sita kwa njia ya posta."

"Nimetoka nyumbani siku chache zilizopita na alikuwa bado hajapata chochote."

"Basi wafanyikazi wa posta wamenyakua kifurushi hicho.

Wengi wao ni kama paka waliowekwa kulinda kitoweo.

Kawaida yao kudokoa mali za watu, na kuzichelewesha barua kufika."

(Uk. 51-52).

Baadaye meneja huyo anampatia Akida nakala sita za diwani ya babake, 'Kero za Mkiwa', ampelekee babake na pia anamkabidhi Akida nakala yake. Sifa za meneja huyu na jina la shirika lake vinaafikiana na vitendo vyake. Maongezi yao yanatonyesha maudhui ya uwajibikaji kwa upande mmoja, ilhali kwa upande mwingine tunaona ufisadi, wizi, mapuuza na miundo-msingi duni nchini.

Akida anakasirika baada ya kusingiziwa na Tamari, dadake Tim kwamba alitaka kumbaka. Anaondoka walikokuwa wakiishi wote watatu na safari yake inamfikisha katika klabu ya pombe. Anawakuta walevi wengi huko lakini mmoja anamkasirisha kutokana na maneno yake. Huyu ni Tito Tembo. Alikuwa mtu wa makamo, mfupi wa kimo na mwenye nywele tim tim kichwani. Tito anasema,

“Nakwambia tuliwafyeka wakanju.... korosho hawawezi kurudi tena... mwenyewe mimi usinione hivi nimeua Wakanju wengi sana” (Uk.132).

Maneno haya yalimkasirisha Akida ambaye alikuwa Mkanju. Tito alipoenda Maliwatoni, Akida alimvizia na kumpiga kwa ubao, akaanguka na kunyooka bila kufurukuta. Akida alidhani kuwa alikuwa amemwua; akatoroka jiji la Tandika.

Mwandishi amempatia Tito Tembo jina la kimajazi, yeye ni Tembo na anapenda tembo. Suala zito la ukabila limegusiwa na mwandishi kupitia wahusika hawa. Tunaweza pia tukakisia athari za ukabila kama vile kuchukiana, kushukiana, vita na mauaji.

Uigizaji unabainika katika tukio hili kwa njia hizi; kwanza, ukumbi wa kunywea tembo ni mfano wa mahali pa kuigizia. Akida anamkuta Bw. Tembo katika ukumbi huu. Kisha jukwaa hili linabadilika wakati hadhira inashuhudia Akida na Bw. Tembo wakiwa Maliwatoni. Huu ni mfano wa kubadilisha mandhari ya jukwaa wakati wa uigizaji.

“Kwani mjomba kuna nini?” aliuliza Tim.  
 “Wakanju?” aliendelea yule Mzee huku amenikazia macho.  
 “Hakuna watu wajinga kama wakanju. Mimi huwa nasema kwa jahara mambo haya, sifichi kitu”.  
 “Hebu niambie kijana”, aliendelea. “Babako ana wake wangapi?”  
 “Alikuwa na mmoja tu”.  
 “Kwani ni mkanju gani huyo?” Hakuna mkanju ana mke mmoja tu. Hakuna. *Number two*, wakanju wanapenda matanga sana. Ukimkuta mkanju safarini ujue anasafiri kwenda matanga; sijui matanga ya mjomba, sijui matanga ya binamu, sijui matanga ya shangazi... wataanza hata kwenda matanga ya mbwa na paka.....”  
 “Mjomba sasa twataka kuondoka”, alisema Tim.  
 “Nilikuwa sijiwezi kwa uchungu. Huenda Tim aling’amua hilo.  
 “Ah! Ngoja nikwambie Tim. Mkanju hana shukrani  
 (Uk. 25 – 26).

Maneno ya Akida na Bw. Tungu yanasababisha hali ya uigizaji. Akida anaposema, “Mimi ni Mkanju”, kauli hiyo inazua vitendo kadhaa tunavyoshuhudia kupitia Bw. Tungu. Aliukunja uso; akaweka glasi ya kinywaji mezani, akatikisa kichwa na kisha kuangua kicheko. Haya yanaweza yakashuhudiwa na hadhira. Huenda mjombake Tim, Bw. Tungu alipata mseto wa hisia kutokana na maneno ya Akida. Maneno hayo yanasababisha uigizaji tunaoutazama kama hadhira.

Kwa upande mwingine, Bw. Tungu anapotaka kujua kabila la Akida; Akida anajibu kuwa, ‘Mimi ni Mkanju’ kwa tabasamu. Kwa hivyo swali la Bw. Tungu; “Akida ni kabila gani?” linasababisha Akida kujibu kwa tabasamu. Kutabasamu ni ishara ya furaha na ishara hiyo hushuhudiwa na wanaomtazama mhusika.

Pia, maneno ya Bw. Tungu yanazua vitendo wanavyofanya Akida na Tim. Akida anakasirika anaposema, "... Nilikuwa sijiwezi kwa uchungu", ishara kuwa alikuwa amekasirika. Tim naye kwa kuhisi aibu na kuona hasira za Akida, anachukua hatua nyingine. Aliamua waondoke kwa mjombake. Hii yote ni mifano ya maigizo. Ni jambo halisi kwa mhusika kufurahi ama kukasirika kutegema maneno anayoyasikia. Haya yameshuhudiwa kupitia wahusika hawa watatu; Akida, Tim na Bw. Tungu.

Ingawa Tim na Akida hawana hisia za kikabila, tunamwona mjombake Tim kama mtu aliyelewa kasumba ya ukabila. Si mfano wa kuigwa na wengine. Kuongezea haya, alimfuta Tim kazi alipogundua kuwa aliishi na mtu wa kabila tofauti. Kupitia mdahalo huu, maudhui ya ukabila, ubinafsi na chuki yameelezwa na mwandishi kupitia wahusika. Mitindo ya takriri, kejeli na taswira imetumiwa na mwandishi kupitia wahusika hao.

Hali ya uigizaji kupitia sifa za wahusika pia inabainika katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* (1987). Monika amechorwa kama msichana aliyekengeuka, mwenye tamaa na anayependa sana anasa. Hali hii inamfanya kuhadaiwa na dereva wa waziri wa kilimo, Bw. Selemani. Aliyemdanganya aliitwa Juma na alidai kuwa alikuwa akifanya kazi katika wizara ya biashara. Baadaye alipoliona gari la waziri Selemani, alilikimbilia kwa lengo la kwenda kumgombeza Juma kwa kuchezea shere. Lakini alimkuta waziri mwenyewe na kumweleza yaliyomsibu. Hayo yalimchekesha sana waziri Selemani. Mazungumzo yao yalikuwa hivi;

"Lakini wewe nini?" Hili si gari la Juma Selemani?"  
"A-ah Juma! Unamjua?" yule mtu aliuliza.

“Ninamjua,” alijibu Monika, “na ndiyo maana nilitaka kusema naye”

“Ulikuwa na jambo muhimu unataka kumweleza Juma?”

“La, nilitaka kugombana naye, au anipe sababu ya kutenda kama vile”, Monika alijibu.

“Kwani alifanya nini?” Baada ya kueleza, mtu yule alicheka mpaka machozi yakamtoka.

Baadaye anamwambia, “Nasikitika amekudanganya nitamkaripia, nikirudi. Kwanza kwa sababu yako na pili kwa kutumia gari yangu bila ruhusa”.

(Uk. 102 – 105).

Mwandishi alitumia mbinu ya sadfa ili kubainisha uongo wa Juma na tamaa ya Monika. Ni jambo la kawaida kwa watu kutumia majina au vyeo vya wengine ili kujipatia sifa.

Hali hii ya uigizaji inaonekana pia katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* (1976) ya Mohamed, M. S. Pale ambapo Rehema anakutana na Sulubu ambapo maongezi yao yanasawiri uigizaji na uhalisi wa kiwango cha juu. Haya yanatokea baada ya Rehema na Sulubu kuondolewa kutoka ardhi walioishi sehemu ya Ramwe. Baadaye walipata kishamba katika eneo la Pakani. Maongezi yao yalienda hivi:

“Tumehamia katika jahanamu!” “Midudu kama hii na jua kali hili!”  
Sulubu anajibu, “Tutashinda tu, .... ngojaga,  
Tutashinda tu Pimdogo Reema” (Uk. 152 – 154).

#### 4.2.2 Maneno na Vitendo vya Wahusika

Walibora amefanya wahusika wake wanene na watende kiasi cha kuwaonyesha kama wanaoigiza zaidi ya wanavyosimuliwa. Maneno na vitendo hivyo vinazua mambo ya kusadikika na ambayo hupatikana katika jamii halisi. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, mambo yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi na

mwandishi wa kiuhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na huyaakisi maisha katika ngazi za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni (Qusby, 1988).

Kauli hii inaafikiana na ya Bauman, (1992) anayesema kuwa maigizo aghalabu hurejelea hali ya kuwasiliana na hadhira na kuwa kupitia maigizo, tunaweza kugundua vitengo vya kijamii na kitamaduni vya tukio la mawasiliano.

Alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara katika kituo cha biashara cha Baraki; mbunge wa Korosho, Johnstone Mabende alisema: “Hatutaki ‘madoadoa’ hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju”. Mbunge huyu alishangiliwa kwa hoihoi na nderemo na Wakorosho. Kujibu kauli hiyo, Mwalimu mmoja, Alex ambaye pia alikuwa mkorosho alisema, “Mheshimiwa sasa unanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. Wakanju ni ndugu zetu ati. Watu wa fikra kama zako ndio maharabu wa nchi.” Lakini baadhi ya Wakorosho walimwambaa na kumsibabi.

“Ni mkorosho aliyekimbia kisu cha ngariba, ...  
Yeye ni sawasawa na hao Wakanju anaowatetea,  
wasiotahiriwa.”  
(Uk. 2)

Hapa mwandishi amewahusisha wahusika hawa katika mazungumzo ya moja kwa moja na majibizano ya papo hapo. Hali hii inasaidia kuusukuma mbele mchezo wa kuigiza unaotokea. Hadhira pia inachangia katika hali hii. Kwa kutumia tashbihi, Mwalimu Alex anapinga mawazo ya kikabila ya mbunge. Hadhira pia inatumia tashbihi kumkebehi Alex. Mwandishi pia ametumia

sitiari na kinaya kutueleza maudhui ya ukabila, ubinafsi na nafasi ya baadhi ya mila katika jamii hii.

Mjombake Tim, Samson Tungu anapoambiwa kuwa Akida ni Mkanju, kando na maneno ya kejeli anayoyatoa, anafanya pia vitendo vingine ambavyo vilikuwa uigizaji wa moja kwa moja. “.... Alikunja uso, akaweka glasi yake ya kinywaji mezani, ..... akaangua kicheko kikavu...” (Uk. 25). Ni jambo la kawaida kwa mtu ambaye amekasirika, ameshangaa ama amefurahi kufanya vitendo kama hivi.

Mhazili katika kampuni ya mawakili ya Gembo hana mlahaka mzuri na wateja. Vitendo na maneno yanayofuata yanathibitisha haya na kuzua hali ya uigizaji. Mzee Yusuf Matuko anamsalimia:

“Ahlan wa Sahlan”, “Tapu! Tapu! Tapu!” Migongo ya taipureta iliendelea.

Mwanamke yule hakujibu wala kunyanyua uso kuona nani kamsalimu. Purukushani tele.

“Nimekuja tena”, yule Mzee alisema.

“Shida yako nini?” aliuliza mhazili, macho yameganda palepale kwenye taipureta.

“Umenisahau bibie?”

“Eeh! Waniita bibi nimekuzalia nani?” Tena wasema “Umenisahau?”

Kwani twaona watu wangapi hapa tena wa maana zaidi yako?”

Mhazili alijibu swali kwa maswali, katutazama kwa mara ya kwanza.

Aliponikazia macho kama anayetazama kinyaa, nilihisi niko tuputupu.

Moyo ulinidunda.

“Na we ‘chokora’ unataka nini?” aliniuliza kwa ukali huku akibenua mdomo, macho yetu yalipokutana. (Uk. 41).

Kupitia maneno, mhazili huyu amewakaripia, kuwakejeli na kuwatusi wateja.

Kupitia vitendo, kwanza amewapuza, anaendelea kupiga taipureta, hanyanyui

uso kuwaangalia wateja. Anaponyanyua uso, anamtazama Akida kama kinyaa na kubenua mdomo. Huu ni uigizaj, na kupitia uigizaji huu tunapata maudhui ya huduma duni maofisini, utaratibu mbovu wa kufanya kazi, unyanyasaji wa wanyonge na ubaguzi. Mwandishi ametumia tanakali za sauti, balagha, kejeli na sitiari katika uigizaji huu. Kwa mfano, mhazili anapomwuliza Akida alichotaka, tayari alikuwa anajua jibu la swali hilo. Watu huenda maofisini kutafuta huduma mbalimbali. Huu ni mfano wa balagha. Akida alitaka ahudumiwe na mhazili lakini ni mhazili huyo huyo aliyemwuliza alichotaka. Alikuwa ameenda kudai malipo ya bima ya hayati mamake, Bi. Joan Sululu aliyekuwa amekufa kwenye ajali ya basi.

Miongoni mwa mengine, uigizaji unafaa kueleza ukweli wa maisha kwa usahihi unaofaa. Mtendaji sharti azisawiri hali tofauti maishani mwa binadamu na jinsi anavyobadilika kutegemea mazingira. Vile vile, uigizaji unaowashirikisha watendaji walio hai huwa na ufanisi mkubwa kwa sababu watendaji hao wanaweza kuvifaragua vitendo vyao ili kukidhi matakwa ya hadhira zao.

Baada ya Akida kuachiliwa kutoka kifungoni, anaandamana na Tim hadi mtaa wa madongo poromoka wa Falkland alikoishi Tim. Punde si punde vijana wanne Wakorosho wanavamia ploti hiyo wakimtafuta Akida. Walitaka wamwue kwa sababu yeye ni Mkanju na pia vile hapo awali, alikuwa amemjeruhi vibaya baba yao, Bwana Tito Tembo.

Maneno na vitendo vya wahusika vinavyofuata vinakuwa ni maigizo kamili. Tamari, dadake Tim alipotoka shuleni na kumkuta Akida nyumbani mwa Tim, hakumsalimia. Alienda nyuma ya pazia kwa hasira.

“Kuna watu wamesimama katika lango la ploti hii,”  
alisema Tamari akiwa nyuma ya pazia alikokuwa”.  
“Wanataka nini?” Tim alimwuliza.  
“Sijui. Wamebeba silaha mikononi, ... wana panga na marungu”.  
“Basi wana nia gani?”

Tim alitoka nje ghafla. Nilipotaka kumfuata aliniamba nibaki ndani. Nikabaki kochini, huku Tamari yuko nyuma ya pazia. Sote tulikuwa tuli kama maji mtungini. Kimya chetu yamkini kilisababishwa na mambo mawili: kutoelewana baina yetu na hamu na ghamu ya kusikia yaliyokuwa yanaendelea huko nje.

“Kuna kijana Mkanju aliingia ploti hii”, sauti moja ilisikika ikisema.  
“Tunamtaka huyo Mkanju. Yule aliyeachiwa na mahakama leo”.  
“Basi hakuna Mkanju hapa. Hakuna mtu aliyeachiwa na mahakama hapa”,  
nilisika Tim akiwaghilibu.  
“Pigeni sachi mkimpata mchukueni,” alisema jirani mwingine.  
“Kwani amefanya nini?”  
Niliposikia vile nikanyapianyapia na kwenda nyuma ya pazia alikokuwa Tamari.  
Alikuwa amekaa kitandani.  
Alinikodolea macho. Nikaduwaa.  
“Wananitafuta”, nikanong’ona.  
“Wanakutafuta wewe kwani umefanya nini?” aliniuliza.  
“Sijafanya kitu,” nikajibu na kujaribu kuingia mvunguni mwa kitanda.  
“We’ nawe! Mbona watetemeka kama mwanamke”, akasema na kunizuia kuingia mvunguni.  
Akanivuta na kuniketisha kitandani. “Utakuwa mwanamume lini?”  
Nilishindwa kujibu. Tamari alitikisa kichwa na kuangua gauni yake ya manjano iliyokuwa ukutani. Akanipokeza gauni hiyo pamoja na kanga moja.  
“Vaa hizi,” alininong’onezea.  
“ We’ Tim ulikuwa na mgeni kijana leo”, nilisikia sauti yamkini ya jirani mmoja.  
“Lakini si Mkanju”, Tim alisisitiza.  
“Mtafuteni nyumba kwa nyumba”, nilisikia jirani mwingine akisema.  
“Vaa haraka”, alisema Tamari tena.  
“Nilianza kuvaa gauni juu ya mavazi niliyokuwa nayo”,

Tamari akaikamata gauni yake na kunizuia kuvaa.

“Mpuuzi wewe, vua hizi nguo ulizovaa kwanza”, alisema na kuanza kunivua shati haraka haraka. Nami nikajikuta nasalimu amri kama mwanajeshi kwa kamanda wake. Tamari alinitazama nikitapatapa kuvaa gauni.

Kisha alinitandia mtandio na kuniamuru nirudi kuketi kochini.

Akanifuatia hima kochini na kunipa viatu vyake vya mchuchumio vilivyokuwa havinitoshi, ni vidogo. Lakini katika hali iliyokuwa imejiri chochote kilifaa. Alichukua daftari lake moja na kunipokeza.

“Usizubae. Jifanye unasoma”, aliniambia.

Nilikamata daftari huku jasho lanitoka, mikono inatetemeka na macho yanaona kiwi. Milango ya madebe ilisikika ikifunguliwa na kufungwa. Mabishano na vurumai moto mmoja. Sauti hizo zilipokaribia nyumba ya

Tim moyo wangu ulikuwa unadunda kama ngoma inayokaribia kupasua kiwambo. “Hakuna Mkanju hapa”, alikuwa amepwelewa sauti kwa kukariri usemi huu tena na tena.

Alijitoma ghafla ndani ya chumba. Akanitazama. Kisha akamtazama dadake Tamari. Macho yake yalipokutana na ya Tamari, Tamari alimkonyezea jicho. Tim akashusha pumzi. Alielewa fika mpango. Alirejea mlangoni.

“Wako wapi hao wanaomtafuta Mkanju? Njoo mtazame hapa ndani”.

“Muda si muda vijana wanne wakajitoma ndani”.

“Mtafuteni Mkanju wenu”, Tim aliwaambia. Wakatazama nyuma ya pazia.

“Kwani amefanya nini?” Tamari aliuliza.

“Ni mahakama,” alisema mmoja wao.” Inamwachia bure mtu aliyemjeruhi vibaya baba yetu. Lazima tulipize kisasi wenyewe. Dawa ya moto ni moto”.

“Umeona wapi kisasi kimejenga nchi?” Tim aliuliza.

“Wakanju si watu wa kusamehewa bwana”, alisema mwingine

“Angalieni hata chini ya kitanda,” Tamari alisema. Wakatazama humo.

Hawa kumwona mkanju waliyemtaka.

“Lazima tumwue. Lazima tumpate tumwue.” Jitu moja likanikazia macho mekundu.

“Wewe kimwana watetemeka nini?” likauliza. Swali hili likaniua kabisa.

“Mbona tena mwamchokoza dadangu,” aliwazomea Tim.

“Hatumchokozi, twamwonea imani anavyotetemeka”.

“Mmetisha nyie! Tokeni mwende zenu!” aliongeza Tamari.

“Basi wacha twende zetu”.

Wakaanza kutoka mmoja mmoja.

“Na mwambie dadako asisome kitabu juu chini”.

Walipokamilisha msako wao, tuliwasikia wakiteta wao kwa wao na kwenda zao.

Hapa ndipo kicheko cha Tamari kilipotoka akachekeka karibu kufa.

(Uk. 203 – 205).

Kupitia dondoo hili, Walibora ametumia maneno na vitendo vya wahusika kugusia maudhui ya uhasama wa kikabila na kusambaratika kwa mfumo wa sheria katika jamii hii. Umaskini unabainika kupitia maskani duni ya wahusika. Ubinafsi unadhihirishwa na majirani wa Tim na Tamari na huruma na mapenzi ya dhati vinaoonyeshwa na Tim na Tamari katika kuyaokoa maisha ya Akida. Hasara za hasira na utovu wa umakinifu vinaonekana kupitia vijana hao wahuni kwa vile wanamwacha mtu wanayemtaka kwa sababu ya papara zao.

Mojawapo ya kaida za uigizaji unaoshirikisha waigizaji hai ni kuwa wanaweza kufaragua vitendo vyao ili vitosheleze matakwa ya hadhira zao. Hali hii inabainika katika igizo tulilorejelea. Ingawa Akida na Tamari walikuwa wamekosana, Tamari anasahau uhasama wao na kufanya lililostahili mtu yeyote kumtendea mwingine. Kwa muda mfupi sana, anamgeuza Akida kuwa 'msichana' kwa kumvisha mavazi yake.

Hadhira katika igizo hili haingependelea wale vijana wahuni wafanikiwe katika mipango yao miovu ya kumwua Akida. Tamari amekidhi matakwa ya hadhira hiyo kwa kutofanikisha mipango yao.

Katika tendo hili, wahusika kupitia maneno na vitendo vyao wameurefusha mchezo wenyewe. Kwa kutumia maneno, wameuliza, wamejibu, wameshangaa, wametisha, wametiana moyo, wamedanganya, wamekejeliana,

wamekarishana na kufurahishana. Vile vile wameamuru, wakaagiza na kuongoza. Haya yabainika hasa kati ya Tamari na Akida.

Wahusika pia wametumia vitendo kuendeleza igizo hili. Vijana wahuni Wakorosho wamebeba silaha, wamegonga milango, wametafuta mivunguni na nyuma ya mapazia, na kukodoa macho. Tamari ameangua nguo, amemvisha Akida amemfunga kanga, amempatia viatu vyake, amemvuta kutoka mvungu wa kitanda alikotaka kujificha. Kwa upande wake, Tim amefungua mlango, ameufunga, amemzuia Akida kumfuata nje, ameachama, akashusha pumzi; pia amewaita hao wahuni kuja kumtafuta Mkanju nyumbani mwake.

Kuongezea, katika kutueleza maudhui kwa vitendo na maneno, Walibora amewafanya wahusika wake watumie mitindo mbalimbali ya usemi. Kuna methali, tashbihi, takriri, tashihisi na kejeli katika mazungumzo yao. Maudhui ambayo mwandishi ameyashughulikia yanaweza kusadikika na kukubalika katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, mtu anapokabiliwa na hatari dhidi ya maisha yake; anaweza akafanya jambo lolote linalomwepusha na hatari kama hiyo. Tunamwona Akida akikubali kuvishwa mavazi ya kike ili anusuru maisha yake. Ni kawaida pia mtu anapoogopa, kutetemeka, kuwa na wasiwasi na kufanya vitendo vinavyomghafilisha zaidi. Akida anapoambiwa avae gauni la Tamari, anataka kulivalia juu ya mavazi yake ya kiume. Kitendo hiki kingeponza zaidi maisha yake.

Ni kawaida pia mtu anayejua anaficha jambo fulani kulithubika kwa maneno makali ama porojo. Haya tunayaona kupitia Tim na Tamari. Ili kuwazubaisha mahasimu wa Akida, Tim anasema:

“Mbona tena mwamchokoza dadangu”, naye Tamari anaongezea ...  
“Mmemtisha nyie! Tokeni mwende zenu!”  
(Uk. 205).

Katika riwaya ya *Doa la Mauti*, (1976), hali ya kuficha ukweli inabainika kupitia mhusika Moddy. Moddy alikuwa amemficha nyumbani mwake. Pili Shabani aliyekuwa mwanafunzi wa chuo cha Tabora. Alikuwa amempa mimba. Pili anajiua kwa kuchelea hasira za wazazi wake. Pili alipojiua, Moddy alikuwa kazini ilhali Aziza mjakazi wake alikuwa akidhani kuwa Pili alikuwa amelala mchana kutwa. Matukio yaliyofuatia yanazua uigizaji. Ili kuficha ukweli, Moddy aliamua kununua jeneza usiku na kuweka maiti ya Pili. Kisha alikodi tekisi iliyompeleka hadi karibu na msitu wa Mto Mara alikoitupa maiti. Lakini baadaye njama zake ziligunduliwa na akashtakiwa kwa kosa la kumficha mwanafunzi bila kuwaarifu wazazi wake, kumpatia mimba na kuitupa maiti yake. Riwaya inapoisha, Moddy anasubiri hukumu ya mahakama kuu.

Hali kama hii ya kuficha ukweli yabainika pia katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* (1987) ambapo dereva wa waziri Selemani anadai kuwa gari alilokuwa nao ni lake na kuwa alikuwa akifanya kazi na wizara ya biashara.

Mfano mwingine katika riwaya hii ni pale Asha bintiye Bi. Mariamu anamposingizia Bi. Keti kuwa alikuwa ameghushi vyombo vya madini

alivyokuwa ameazimwa na mamaye na kurejesha vya bandia. Bi. Keti anashikwa kwa mashtaka ya uongo.

“Salama”, wajibu askari. “Je, wewe ndiye Bibi Keti Rajabu?”

“Kuna nini Kwani?” askari walisema,

“Tumeambiwa tuje kukuchukua stesheni.”

Baadaye akiwa stesheni, anaambiwa na mkuu wa askari, Keti Rajabu, umeshitakiwa kwa kosa la kuiba vyombo vya dhahabu ulivyoazima kwa Bibi Mariamu Muhammed”.

“Mimi? Nimevirejesha! Naapa Yamini nimevirejesha vyombo hivyo kamili”. Tena alimgeukia Asha na kusema, “Na wewe Unajua”, Asha alifuna tu na kucheka, tena akamgeuzia uso”. (Uk. 18 - 19).

Katika maigizo haya, Asha alimsingizia Bi. Keti hatia ya uongo. Sababu ni kuwa tangu awali, Asha alimwonea wivu Bi. Keti kwa sababu alikuwa amependwa na mamake Bi. Mariamu. Vyombo vilivyodaiwa kuwa viliibwa vilikuwa vimechukuliwa na Asha na akampelekea mumewe ambaye alikuwa mcheza kamari. Asha alitaka kuficha maovu yake na ya mumewe kwa kumsingizia Bi. Keti.

#### **4.2.3 Lugha ya Wahusika**

Mojawapo ya mihimili ya uigizaji ni kuwa ni sharti uishawishi hadhira kuuzingatia na ni katika njia kama hiyo ambapo uigizaji huo utafanikisha, mawasiliano. Lakini mawasiliano hayawezi kufanikishwa bila matumizi ya lugha kwa sababu ndiyo njia kuu na muhimu ya kuwasiliana. Traore, (1972) anasema kwamba uigizaji ulio maarufu aghalabu huambatanisha utendaji unaohusisha mwili na utoaji sauti. Naye Robinson (1980:15) ameeleza kuwa hapana uigizaji ambao hauna nia ya kuwasiliana na kwamba ufanisi wa uigizaji huangaliwa kwa jinsi unavyofanikisha mawasiliano. Kwa misingi ya

uhalisia kipengele cha lugha ni muhimu pia kwa sababu lugha katika kazi za kihalisia huwa ni ya kawaida na wahusika huitumia kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu.

Licha ya kuwa wahusika katika *Kufa Kuzikana* (2003) wametumia lugha ya kawaida inayoweza kupatikana katika maisha halisi, lugha hiyo ni ya kushawishi, kuchochea, kuhamasisha na wakati mwingine pia ni ya kukebehi na kukasirisha hadhira. Kuna pia lugha ya kuchekecha. Lugha hiyo pia imeandamana na vitendo vya watumizi wanaopitisha maudhui mbalimbali.

Mbunge, Johnstone Mabende anatumia lugha ya kuwachochea Wakorosho dhidi ya Wakanju. Anasema, “Hatutaki, ‘madoadoa’ hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju”. (Uk. 2).

Ingawa Mwalimu Alex alikuwa Mkorosho, lakini Wakorosho walimwona kama msaliti na mhaini kwa kuwatetea Wakanju. Alipopatikana akiwa amekufa, tetesi zilienea kwamba lazima alikuwa ameuliwa na Wakanju. Akida anaokota karatasi katika kiambo chao kilichokuwa na maandishi ya kivoloya kama ya mtoto wa shule ya chekechea: “Wakanju mumechokosa nyuki kwa kumuuwaa mukoroso. Ama muondoke au mufe mzingani”.

Hii ilikuwa lugha ya uchochezi iliyojaa kasumba za kikabila. Wahusika pia wametumia lugha ya kushawishi. Akida anaposingiziwa na Tamari kwamba alitaka kumbaka, anakasirika na kwenda asikokujua. Anafika katika klabu ya

pombe, na hapo mwanamke mmoja mwenye umbo la kiboko anamjia na kumwuliza;

“Nikutilie moto au baridi *Sweetie?*”

..... “Unaogopa busaa na watu wa rika lako wanaikukumia kama maji kijana?”

(Uk. 132)

Maudhui ya ulevi yamejitokeza katika kauli hii. Vitendo vinavyohusika hapa ni kuwa, Akida alifika, akakaa kwenye fomu; naye mwanamke huyo akanjia.

Wahusika katika riwaya hii pia wametumia lugha ya kukebehi na kukashifu.

Majibizano kati ya mhazili katika kampuni ya mawakili ya Gembo na wateja wake ni mfano mzuri.

“..... Mzee faili yako haipatikani”, mhazili alimweleza mwanamume aliyekuwa hana mkono”.

“Teresia Mtoto Mwema”, aliita mhazili.

“Naam niko hapa”, mwanamke aliyekuwa na kikandiko mguuni aliitika.

“Ajali yako ni ya juzi tu, kwa nini umekimbilia kudai ‘process’ bado ni ndefu sana mama”.

“Basi nilipeni madai ya bima ya mume wangu.” alisema mwanamke huyo.

“Alikufa katika ajali kiwandani. Mwaka wa sita napelekwa huku na huku kama mpira uwanjani.”

“Tafadhali mama kama unafikiria unajua sana siasa, mbona usiwanie ubunge?” Mhazili alifoka.

“Hapa si ukumbi wa kisiasa.”

(Uk. 45).

Wateja hawa wote ni wanyonge wanaohitaji usaidizi, lakini badala ya kuupata, mhazili anatumia lugha ya kuwadhalilisha. Kupitia lugha ya wahusika hawa maudhui ya kiburi, ukatili, ufisadi, ubinafsi na kutowajibika yamejitokeza.

Taswira kama hizi ni mambo ya kawaida katika ofisi nyingi za umma.

Babake Tom, Mzee Mangala aliuliwa katika vita vya kikabila. Kwa sababu ya ukosefu wa usalama vijijini, aliwalipa polisi pesa ili wamsindikize kutoka jijini Tandika hadi kijijini amzike babake. Lakini kwa sababu ya hisia mbaya za kikabila, baada ya mazishi, askari na watu wengine waliomsindikiza Tom wanamwacha makusudi. Akida pia anaachwa kwa kumtetea Tom. Akida anaeleza ....

“Tulipokaribia barabara kuu nikamwambia dereva, ‘Simamisha gari nishuke”.

“Kwani kuna nini?” aliniuliza dereva.

“Wacha kashuke kashenzi aka”, askari mmoja akasema kwa hasira.

“Nakwambia hakuna watu zumbukuku kama Wakanju.

Wacha wauawe waishe wote”.

“Shida gani kijana?” dereva aliniuliza tena huku anapunguza mwendo wa basi dogo hilo.

“N’taka kumwona Tom”.

“Simamisha gari hicho kijibwa kishuke”, askari aliyekaa kiti cha mbele aliamuru.

“Kina mtindio wa ubongo hiki.”

(Uk. 104).

Askari wametumia lugha isiyofaa. Inabainika pia wao ni wakabila, wana ubinafsi, ni wakatili na hawawajibiki. Wanahitajika kulinda sheria lakini wanazivunja. Kundi la Wakorosho lilimvamia Tom na kumpiga hadi wakadhani kuwa alikuwa amekufa. Akida akiwa mafichoni aliwaona na pia akasikia kauli zao:

“Wenzake wamemwacha” ..... “Wacha alale hapo aoze au aliwe na mbwa, hakuna wa kumzika.

“Naam. Ati aje amzike babake kwetu Baraki?

Wakanju wana haki gani kumzika mtu Baraki.

Wao ni magugu sharti wang’olewe, zao linawiri”.

“Upumbavu wake umemtokea puani”.

“Pengine hajafa, nimpige mkuki kichwani sio?”

“Tumkate kichwa chake kilichosomea ng’ambo tukitundike mtini”.

“Mshale haujui msomi yakhe”.

Nilisikia vicheko, vicheko vyenye bezo na kujitutumua.

(UK. 106)

Maneno na vitendo vya watu hawa vinaonyesha kilele cha ujinga, ukatili, ubinafsi, uhasidi na ukasumba wa ukabila ambao ulikuwa umewajaa. Walifurahia kitendo cha kusitikisha na kujipongeza badala ya kujirudi. Walikuwa wamepofushwa na ukabila kwa kiasi kwamba walikuwa wanamkejeli mtu waliyedhani ni maiti.

Kauli hizi zao ni kinyume kabisa na imani na matarajio ambayo Tom alikuwa nayo kabla ya tukio hili.

“Nimefanya mpango na idara ya polisi”, alidokeza Tom.  
“Nimelipa kiasi fulani cha hela kwao. Wamekubali kutusindikiza hadi Baraki tugotoe shughuli za mazishi. Aidha nimekodi marafiki watakaonisaidia kwa shughuli ya kuchimba kaburi na kadhalika. Sharti nimzike babangu kwa heshima mstahiki ima fa ima” (Uk. 91).

Akida, Tim na Pamela walipokuwa jijini baada ya Akida kutuzwa na waziri, wanashuhudia kisa cha ajabu. Mwanamume mmoja alikuwa amefungwa ndi mkokoteni, ukiwa unasukumwa na wanaume wawili waliofuatwa na umati wa waume kwa wake. Lugha inayotumiwa wakati wa kisa hiki ni ya kukejeli.

..... Mwanamke mmoja alitoka umatini, kapu mkononi, akatukabili.  
“Toa kitu kidogo tumpeleke mtoto hospitalini”, alisema na kutunyoshea kapu (Uk. 54).  
na tena ..... “Haikosi wanampeleka hospitali ya wagonjwa wa akili”, ....  
“Mtu mzima kwenda tuputupu hivyo lazima awe na kichaa”.  
“Hata kidogo”, alidakia mwanamume mmoja aliyekuwa anapita karibu nasi.  
“Waliosema siku za mwizi ni arobaini... Huyu bwana tukibeba naye mizigo pale Soko Mjinga kwa miaka mingi. Tangu hapo hatujui mwenzetu kakimbia kisu cha ngariba... basi mwanamke mmoja waliyezaa naye watoto wawili lakini hawajaoana, ndiye aliyemsaliti kwetu. Sisi kumkagua leo, Lo! Kumbe mwenzetu bado ‘Mtoto’ ati. Basi tukaazimia tulifunge soko ili tuigotoe shughuli hii ya dharura kwanza. Wacha mtoto afanywe ‘mwanamume’ ndipo awe na akili. Toeni mchango wenu”.  
(Uk. 55)

Lugha iliyotumiwa na wahusika hapa ni ya kumkejeli huyo mwanamume ambaye alikuwa hajapashwa tohara. Suala la mila na athari zake limerejelewa hapa. Lugha ya kukasirisha pia imetumiwa na wahusika katika kuibua maudhui mbalimbali. Tamari, anatoroka vita kijijini na kukimbilia kwa nduguye mjini Tandika. Alikuwa amejeruhiwa. Akida anamkanda mguu na kumpikia chai lakini hayo yakiendelea, Tamari anasema:

“Nye Wakanju ni wajinga”.

“Ee! Tamari” Nilimaka.

“Nye ni wauaji”, aliendelea kufoka.

“Tamari usiseme hivyo tafadhali”, nilimtafadhaisha kwa matao ya chini.

“Nenda huko bwege wewe”, alinitupia tusi. “Mwanzo unafanya nini katika nyumba ya kakangu?” (Uk. 63).

Hisia mbaya za kikabila ndizo zinazomfanya Tamari kutumia lugha iliyomkarisha Akida. Analipa fadhila kwa mateke. Lugha ya mtangazaji wa redio ya ‘Sauti ya Kiwachema’ inamwudhi Tim na anaizima redio kwa hasira.

“..... Mkuu wa Wilaya ya Korosho Bwana Erastus Aduulo amevishutumumu vyombo vya habari vya kigeni kwa kupiga chuku hali ya usalama wilayani ....”  
(Uk. 61).

Ukweli ni kuwa vita vilikuwa vimechacha na kuwaangamiza watu wengi.

Malumbano kati ya mhazili katika kampuni ya mawakili ya Gembo na wateja yanawakasirisha wateja hao;

“Hata we’ Mzee wanitovukia adabu?” mhazili alimsaili Matuko huku anamtazama kwa jicho la hasama.

“We’ kijana”, alinigeukia. “Kampuni ya Bima ya Akiba haijaleta malipo ya mamako bado. Nenda uje siku nyingine”.

“Kila mtu akija mnamwambia ‘nenda uje, nenda uje’, alisema mwanamume mwenye mkono mmoja.

“Mnafikiri ‘nenda uje’, ni mshumbi wa wali mtu ataula ashibe?

Basi tumekula tukashiba ‘nenda uje’ hizo mpaka sasa tunazitapika”.

“Na hapa leo hatutoki mpaka tumemwona Bwana Gembo atulipe pesa zetu”, aliapa Mzee Matuko.  
“Nitakuitieni polisi, mhazili alitishia, mikono kaishika nyongani.  
“Waite na liwe liwalo,” wateja walimjibu (Uk. 46).

Tukio hili limehusisha wahusika katika maneno na vitendo na tunaona kuwa lugha wanayoitumia inawakasirisha wote. Kutojali, kiburi na ufiisadi ni hoja zinazogusiwa hapa. Akida alikuwa amepolekwa kwa shangaziye Pamela ili kuyaokoa maisha yake. Shangazi huyo anapomkuta Akida nyumbani mwake baada ya kutoka kazini alfajiri, anakasirika na pia kutoa kauli zilizomkasirisha Akida.

“Pamela!” nilisikia akiita kwa ukali.  
“Bee!”  
“Umegeuza nyumba yangu danguro?”  
“Nimekwambia huyo kijana ana shida shangazi”.  
“Lakini huwezi kumwingiza hapa mtu bila kibali changu.  
Video deck yangu imepotea juzi kutokana na watu kama hawa”.  
“Naomba radhi”.  
“Tena mtu ametoka jela kumleta kwangu?” mwambie atoke aende zake” (Uk. 214).

Hoja za uchoyo, ubinafsi, umaskini na huruma zimerejelewa hapa. Uchoyo na ubinafsi unaonekana kupitia shangazi yake Pamela anapojifikiria tu bila kujali shida za wengine. Anathamini sana mali kuliko uhai na utu; umaskini unashuhudiwa kupitia Akida. Ukosefu wa maskani ndio unaomfedhehesha. Pamela anaonyesha huruma kwa kumpatia Akida mahali pa kulala ingawa alijua kuwa shangazi yake alikuwa mkali.

Walibora pia amewashirikisha wahusika wake katika lugha ya kuchekesha hadhira. Kazi zozote za kihalisia huwapa wahusika fursa ya kuitumia lugha kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu.

Baada ya Akida kudhani ‘ameua’ mtu anaabiri basi kwenda kujificha Sangura, umbali wa kilomita mia nne kutoka Tandika jijini. Akiwa basini, mazungumzo yanayotokea baina ya utingo wa basi na abiria yalikuwa ya kuchangamsha na kuchekecha.

Kila abiria alijaribu kupiga bei ili apunguziwe nauli.

“Wewe huoni jinsi uchumi ulivyotuuma tangu wafadhili wamekatiza msaada kwa Kiwachema?” alilalamika abiria mmoja.

“Kosa si letu wenye mabasi”, alisema utingo. “Barabara zenyewe zimeharibika.....”

“Kosa si letu abiria, hatujaharibu barabara ya mtu”, alisema abiria mwingine.

“Kosa ni lenu wananchi maana nyie ndio mnaochagua marubani vipofu kuendesha ndege”, alisema utingo.

(Uk. 135).

Maongezi baina ya Jimmy na Rose, wanafunzi wa chuo kikuu ambao pia walikuwa katika basi yanachekecha.

“Wamjua Peter?”

“Peter yupi?”

“Yule wa kitivo cha sanaa, aliyewania uongozi wa chama cha wanafunzi

mwaka jana akashindwa”.

“Ooh! Namjua”.

“Basi babake ni hakimu”.

“Ala!”

“Basi alitueleza kuwa siku moja babake aliliweka ndani miaka kumi bila faini jizi moja lenye kutumia mabavu. Kisha jioni hiyo hiyo, alipokwenda baa kupiga mtindi, anakutana nalo limepiga oda ya bia meza nzima.

Likamwambia babake Peter, ‘Karibu Bwana Hakimu’. Basi baba mtu alitoka humo kwenye baa mbio ambazo hazina mfano...

(Uk. 139).

Maelezo haya yanachekecha yeyote atakayeyasikia. Japo mwandishi amezungumzia maudhui mazito ya ufnisadi, amefanya hivyo kwa lugha inayochangamsha hadhira yake. Wahusika wametumia maneno na vitendo

kuwasilisha maudhui ya ufisadi kwa hadhira. Hakimu alikuwa amehukumu, jioni amekwenda baa, amekutana na jizi, amegutuka, amekimbia. Hii ni taswira inayojengeka mawazoni mwetu. Jizi nalo pia limekwenda baa, limeagiza vinywaji, limemwalika hakimu.

Uigizaji mwingine wa kuchekesha kupitia lugha na vitendo kunaonekana katika mazungumzo kati ya Mzee Muyaka na mkewe Bi. Tina. Walikuwa wakiandaa mipango ya binti yao, Nana aliyekuwa aolewe.

“Baba Nana!” Bi. Tina alimwita mumewe.

“Nini?”

“Mbona hujawaita amu zake Nana?”

“Mtoto ni wa ukoo ama ni wangu na wewe?” alijibu Mzee Muyaka, “... unaweza kuwaita hao ndugu zangu kama ulizaa nao”.

“Wacha kunitukana”.

“Nawe wachacharika nini? Wewe ndiye unayeolewa au ni Nana?”

“Unasahau mume wangu kuwa kimila hakuna mtoto wa wazazi wawili tu”.

“Usiniambie mambo ya mila. Kwanza kihame hicho chama cha kupinga tohara ya wanawake, uwe mtetezi wa mila kamili. Utawezaje kupinga na kutetea mila wakati huo huo? Huo ni ukauleni kweli kweli!”

(Uk. 176-177).

Suala linaloleta utata hapa ni nafasi ya mila katika jamii zatu; je, kunazo mila zinazofaa na zisizofaa? Bi. Tina anamjibu mumewe.... kuwa; Kuna mila nzuri na kuna mila zilizopitwa na wakati”. (Uk. 177).

Katika kisa kingine, Mzee Muyaka anapokea barua kutoka kwa bintiye Nana. Kwa vile miwani yake ilikuwa haionekani, ilibidi kutafuta mtu amsomee. Bi. Tina akaja na Susana, kigoli aliyekatiza masomo kwenye darasa la sita ili aonje tamu na chungu ya ndoa. Susana aliifungua bahasha akaikunjua barua na

kubaki amesimama tutwe, ameitumbulia macho, na jasho kumchiririka kipajini.

“Soma mama”, alimhimiza Bi. Tina, huku Mzee Muyaka akiendelea na shughuli za kuiboresha bakora yake.

“Wajua kusoma?” Bi. Tina alisaili.

“Ndi .... ndiyo”.

“Basi soma”.

Kimya.

“Shida gani mama?” Bi. Tina alimwuliza, stahamala zimemwisha.

“Kwa kwe....li”, alidodosa msomaji, haya zimemjaa.

“Huyu ameandika kwa kukoroga sana mwandiko....”

“Enda ukanifatutie mtu ajuaye kusoma barua”, hatimaye alisema Mzee Muyaka, tena bila kunyanyua uso.

(Uk. 178-179).

Maneno ya Susana katika kisa hiki ni ya kuchekesha. Maudhui ya ndoa za mapema na kubaguliwa kwa wasichana katika jamii ndiyo yanayoonekana hapa. Mwandishi ameyagusia kwa lugha ya kawaida lakini ya kufurahisha.

Walibora pia amehusisha wahusika wake katika kutumia lugha ya staha.

Ilikuwa sadfa kuwa basi la ‘Salama’ lililopata ajali miaka kumi iliyopita na

kumwua mamake Akida, Joan Sululu, ndilo basi pia lililomjeruhi vibaya Mzee

Yusuf Matuko. Katika kuelezana yaliyotokea, lugha ya heshima inatumiwa.

“Kijana ulisema mamako alikufa ajalini miaka kumi iliyopita?” Mzee Matuko alinisaili.

“ Ndivyo”, nikajibu. “Alikuwa akisafiri kwenye basi la Salama kutoka jijini hapa....”

“Oooh! Pengine ni lilelile basi lililonibadilishia maisha. ... basi likayumbayumba, kisha puuu! Likakutana uso kwa uso na lori”.

“Wewe ulipoteza nini?” nilijasiria kumwuliza yule Mzee.

“Mimi .....nilikufa siku hiyo, nimekuwa marehemu tangu siku hiyo”.

“Hapo ndipo ulipokatika kidole siyo?”

“Kidole na .... ee! Chuma kilinipata .... Aaah!

“wewe mtoto mdogo pale ulipo, sasa nikwambie nini?”

“Wateja wengine waliposikia hivyo wakaangua kicheko wakacheka.

(Uk. 44).

Katika maongezi haya uhalisi wa maisha umegusiwa kupitia mambo kadhaa. Kwanza, siku hizi ni kawaida watu kusafiri na wanapofanya hivyo; wengi aghalabu hutumia magari hasa ikiwa safari ni ndefu. Pia ni jambo halisi kuwa siku hizi kuna ajali nyingi za barabarani zinazohusisha magari ya abiria. Zinapotokea, watu wengi hujeruhiwa ama hata kuaga dunia.

Pia ni tukio la kawaida katika mazingirira yetu kuwa manusura wa ajali kama hizo hupitia masaibu mengi hasa wanapojaribu kupata usaidizi kutoka kwa vyombo vya dola, mashirika ya bima ama wafadhili wowote. Tunayaona haya kupitia kisa cha Mzee Yusuf Matuko. Ingawa alikuwa amejeruhiwa vibaya, kampuni ya mawakili ya Gembo haikuwa tayari kumlipa. Suala la ufisadi pia lajitokeza hapa na ni jambo halisi katika maisha ya sasa.

Wanadamu hukasirika ama hufurahi kutegemea tukio la huzuni au la furaha. Lakini wakati mwingine kinyume cha haya hutokea na hili ni jambo halisi. Kwa mfano, ingawa matangani ni mahali pa huzuni; si ajabu kupata watu wakipiga gumzo na kucheka. Ingawa Yusuf Matuko alikuwa ameumia na alikuwa akizungumzia tukio la kusikitisha; maneno yake yanawachekesha waliokuwa wakimsikiliza. Huu ni uhalisi katika maisha.

Uigizaji pia umebainika kupitia maneno ya Matuko na Akida. Wanaongea mmoja, baada ya mwingine. Wako katika sehemu mahsusi, ofisini ambamo mnaweza kuchukuliwa kama jukwaa. Mzee Matuko anauliza swali; Akida anamjibu. Kisha anaeleza jinsi basi lilivyoyumbayumba na kukutana uso kwa

uso na lori na kuiga mlio, ‘Puuu!’ uliotokea magari hayo yalipogongana. Haya yote yanajenga taswira ya uigizaji akilini mwa hadhira inayosikiliza.

Suala linalogusiwa hapa ni zito na nyeti mno lakini Mzee Matuko ametumia lugha ya heshima ili kulifumba. Tamari anapoachwa nyumbani na Akida nduguye Tim alipokuwa ameenda kufanya kazi zamu ya usiku, anajaribu kumtaka Akida usuhuba.

“Wewe nani?” nikauliza kwa hofu.

“Usiseme kwa sauti”, nilisikia sauti ya kike.

“Aaa! Tamari!” niliuliza kwa mshangao.

“Usichacharike kama moto wa kifuu”, alinirai kwa mning’ono (Uk. 128).

Akida anapokataa vishawishi vyake, Tamari anamwacha na kusonya. Tena anamwambia,

“Nilifikiri wewe ni mwanaume” (Uk. 129).

Kauli hii ya mwisho ilikuwa na maana nyingine fiche. Mwandishi ameangazia suala la umaskini linalobainika kwa maskani duni yanayoweza kuchangia maovu. Mzee Muyaka anampa Akida masharti baada ya kumwajiri kazi ya kumchungia ng’ombe.

“Utakubali mshahara wa shilingi mia tatu kwa mwezi?”

“Bila shaka”

“Sasa sikia, hapa nina binti mmoja kenda shule asubuhi.

Tafadhali... tafadhali usimchezee”.

(Uk. 148 – 149).

Wazungumzaji wamehusishwa moja kwa moja katika kueleza maudhui ya umaskini na mila. Wanatumia lugha fiche lakini ambayo wote wanaielewa. Badala ya kusoma, Akida anachunga ng’ombe na hili linasababishwa na umaskini. Kimila, mambo mengine hayafai kutajwa waziwazi. Muyaka

anapomwambia Akida asicheze na bintiye, anaelewa anachomaanisha. Wahusika katika kazi za kihalisia huitumia lugha kama ilivyo katika hali halisi ya mazingira yao; hili limebainika katika mazungumzo haya.

Katika *Doa la Mauti* (1976), maneno ya askari wapelelezi yanazua uoga kwa Moddy. Maudhui yanayorejelewa ni uhalifu.

“Hodi”, Koplo Chacha alibisha mlango, kisha Moddy akafungua. “Karibuni ndani”, Moddy aliwakaribisha ukumbini. “... tumefika hapa ili kupata maelezo kadha wa kadha toka kwako”.

“Hapana neno Inspekta”, Moddy akaitikia kwa mashaka.

“Je, wamfahamu Pili walau kidogo?” Bila kuchelewa Moddy akaingilia,

“Pili yupi huyo?”

Pili yeyote yule unayemdhania”, Inspekta Willey alinena huku akamtazama Moddy.

“Kwa nafsi yangu itakuwa vigumu kubaini ni mhusika yupi mnayemhitaji ninyi. Pili ni jina tu sawa na bahari, labda kidogo mngegusia udibaji wa Pili mumtakaye nyinyi (Uk. 88 – 89).

Maneno ya wahusika hawa yanazua taswira ya uigizaji kwa namna wanavyojibizana kwa zamu. Pia ni jambo lililo na uhalisi kwa mtu aliyekosa kujaribu kuficha makosa yake. Haya yabainika kupitia Moddy anapoitupa maiti ya Pili msituni. Awali alikuwa ameishi naye kisiri na kumpatia mimba. Maneno ya askari yalimshtua na akabaini kuwa siri yake ilikuwa imefichuka.

Maigizo kupitia maneno ya wahusika pia yabainika katika riwaya ya *Kicha Maji* (1974) pale Tegemea na Moyokonde wanapozungumzia swala la ndoa

na ukosefu wa kulipa mahari. Haya ni mambo halisi yanayotokea maishani.

Tegemea anasema:

“Wewe ndiye umemwoa binti yangu?”

“Ndiyo”. Moyokonde alijibu kwa unyenyekevu.

“Ulifika nyumbani kuleta posa?”

“Hapana”

“Unafikiri Vumilia alianguka kutoka angani?”

“Hapana”.

“Basi, fahamu kwamba Vumilia alizaliwa. Ukifahamu hivyo, fahamu pia kwamba mama yake amekuja sasa kumchukua”.

Kisha baadaye wanaendelea,

“Kumchukua Vumilia sasa ni kuchukua maisha yangu.....”

“.... Na kwa nini mnaishi kwa nyumba kama hii? Sisi kwetu nyumba kama hii ni nyumba ya kuku. Siwezi kumwacha mtoto wangu humu”.

“Mimi ninakubali kwamba ni maskini. Lakini hata maskini pia hupenda”.

(Uk. 191 – 192).

Maneno ya Tegemea yanamdunisha Moyokonde.

#### **4.2.4 Mandhari**

Mandhari ni istilahi inayorejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vinavyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yaliyoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa, kwa mfano, nyumbani, njiani, au kwenye uwanja wa vita (Mbatiah, 2001).

Vile vile dhana hii hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia, yaani mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Katika maana pana, dhana hii huelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanamojikuta wahusika wa kifasihi. Aghalabu wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika lakini

hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia (Wamitila, 2003).

Fasili hizi mbili zinaafikiana na maelezo ya Bauman (1992) anayesema kuwa maigizo aghalabu hurejelea hali ya kuwasiliana na hadhira kupitia jukwaa kwa njia ya kuvutia na kuiteka hisia ya hadhira hiyo. Anaongeza kuwa miongoni mwa mambo muhimu yanayoashiria uigizaji ni vitu kama jukwaa lililoinuliwa, na pia kuwa maigizo yote hupatikana, hutokea na huthaminiwa kwa mujibu wa muktadha wa kijamii unaohusika.

Katika *Kufa Kuzikana* (2003) kuna mandhari mbalimbali yanayoweza kuchukuliwa kama majukwaa ya kuigizia na wakati huo huo ujumbe mbalimbali kuwasilishwa kwa hadhira. Majukwaa hayo ni kama ofisini, katika basi, mahakamani na bomani.

Ofisi ya mawakili ya Gembo jijini Tandika inaweza kuchukuliwa kama jukwaa ambapo uigizaji unatokea. Washiriki wanatumia maneno, vitendo na ishara kadha katika kuongea kwao ambako kumedhamiriwa kufikia hadhira.

“Nilikuuliza swali”, mhazili alinikemea.

“Mhudumie huyu Mzee kwanza, amenitangulia”.

“Usijifanye mjuaji, kazi sianzi leo. Hebu sema kilichokuleta”.

“Madai ya bima”... “Ndiyo malipo ya bima ya mamangu aliyekufa kwenye ajali ya basi”.

“Jina lake?”

“Joan Sululu”

“Namba ya faili yake?”

“12437 Mkwaju 84”.

“Nawe Mzee una shida gani.”

(Uk. 42).

Hapa mhazili hawasiliani na wateja kwa njia ifaayo. Maudhui ya kiburi, ubinafsi na kutowajibika yanagusiwa.

Katika ofisi ya waziri wa elimu, kabla ya kuzawadiwa, wanahabari waliwahoji waliofika kwa tuzo:

“Akida”, aliniuliza mwandishi mmoja mwanamke.

“Wataka kufanya kazi gani uhitimupo masomo?”

“Nataka kuwa msanifu ujenzi”, nikajibu.

“Kwa nini?”.

“Nimehuzunishwa mno na visa vingi vya majengo yaliyojengwa na kusanifiwa vibaya katika miji mingi nchini, yakiporomoka na kuwaua watu bure, bure bure bila kisa”. Ili kuondokana tatizo hilo, lazima wawepo wasanifu, ujenzi wengi waliobobea katika fani yao.”

“Nikidhani ufisadi ndio hupelekea kuwepo majengo yasiyofikia viwango

vitakiwavyo kujengwa mijini.”

“Mimi siwezi kubadili matamano yangu kwa sababu ya tatizo la ufisadi.

Ufisadi ungalikuwa mtu ungalimpiga risasi ukammaliza: Lakini ufisadi ni roho au pepo iliyomwingiea karibu kila mtu nchini. Utawaua watu wote ili kuondoa ufisadi?”

Mwanamke huyo alicheka sana kwa jibu langu. Mpiga picha mmoja akanifyatulia flashi.

(Uk. 48-49).

Katika dondoo hili, maudhui ya ufisadi na kutowajibika yamerejelewa na mwandishi kupitia maneno na vitendo vya wahusika. Kupitia maneno, mwanahabari amemhoji Akida; Akida naye amemjibu kwa kufafanua hoja zake. Vitendo vinavyotokea ‘ni kuuliza, kuandika, kupiga picha. Hadhira inayoshuhudia haya ni sisi wasomaji na pia watu wengine waliokuwa katika ofisi ya waziri wa elimu.

Jukwaa lingine lajitokeza katika basi alimokuwa Akida, akitoka Tandika kwenda Sangura. Kunatokea malumbano kati ya wahusika waliokuwemo.

Kulikuwako ilani kwenye basi, “Usivute sigara”, lakini mtu mmoja alikuwa akivuta sigara.

“Zima hiyo sigara”, utingo alitoa amri.

“Usiniletee uboza hapa”, alisema mvutaji sigara.

“Nakuona wewe kama sisimizi kwangu, hunitishi kwa vyovyote”.

“Tusitukanane bure, fanya heshima bwana”, utingo alimtafadhalisha.

“Mtupeni nje ya basi”, abiria mmoja alipendekeza.

“Anakataa bure huyo”, alisema mwingine.

Dereva alisimamisha basi ghafla, baada ya utingo kubofya kengele kwa hasira. Mabishano makali yakapamba moto baina ya mvutaji sigara kwa upande mmoja na utingo na abiria wengine kwa upande mwingine. Hatimaye mvutaji sigara alisalimu amri na kuizima sigara yake.

(Uk. 141).

Katika malumbano hayo, hali ya ukaidi, ubinafsi, na kutojali inajitokeza kupitia mvutaji sigara. Pia ametusi, kubeza na kudharau utingo. Abiria kwa upande wao wamemzomea, kumwaibisha na hatimaye kuusitisha uraibu wake. Kama hadhira, vitendo vinavyoshuhudiwa ni kama, kuvuta sigara, kubofya kengele, kusimamisha gari na kuzima sigara. Hatima ya maigizo haya inaafikiana na matarajio ya hadhira ambapo mvuta sigara anakomeshwa na wengi wanaochukizwa na kitendo hicho.

Baada ya kujificha Sangura, Akida anaeleza kuwa aliamua kurudi jijini Tandika na kujisalimisha kwa polisi;

“Na wewe kijana?” askari mwanamke aliniuliza.

“Nime... Nimemwua mtu”, nilisema kwa kusitasita.

“Ati umemwua mtu?” aliuliza tena kwa mshangao.

“Ndi... ndiyo”.

Kisha aliangua kicheko na kucheka kicheko cha kutisha. Alifungua kilango kilichokuwa pembeni mwa kaunta na kuniamrisha niingie ndani upande aliokuwa kisha akaniumrisha nivue viatu na kuketi kitako chini sakafuni karibu naye.

“Umemwua nani?”

“Zablon Mapisi”.

“Lini?”.

“Miaka mitatu iliyopita kisha nikakimbia.

Lakini nimeamua kujisalimisha kwenu ili mnifanye lolote”.

(Uk.186-187).

Hatimaye Akida anapelekwa kwenye seli.

Igizo hili limejaa kauli zinazoambatana na vitendo kadha. Maelezo ya Akida yanatuchorea taswira na kutuwezesha kama hadhira ‘kutazama’ yaliyokuwa yakitokea katika kituo cha polisi.

Akida na polisi wanaongea kwa kupeana nafasi, mmoja anaongea baada ya mwingine, hatua kwa hatua. Kuna kuhoji, kusesitiza, kuhoji tena, kucheka. Polisi pia anatenda haya: anauliza, anaangua kicheko, anafungua kilango, anaamrisha. Huu wote ni uigizaji. Maudhui yanayogusiwa hapa ni mifumo ya utendakazi, taratibu za sheria na shida zinazowapata wavunjao sheria.

Katika mahakama, Akida anasomewa mashtaka yake. Hapa mahakama ni kama jukwaa la kuigizia na waliokuwa mahakamani kushuhudia kesi hiyo ni hadhira. Mwendesha mashtaka aliombwa na hakimumu kutoa maelezo ya kesi ya Akida.

“Mheshimiwa hakimumu”, mwendesha mashtaka alianza kutoa maelezo”.

Mshtakiwa Akida Sululu au kwa jina la kupanga kipande madodo, alijisalimisha mwenyewe hivi karibuni katika kituo cha polisi cha kati jijini, akidai kuwa alimwua Zablon Mapisi kwa kumpigia kipande cha ubao katika mtaa wa Falkland. Kisha akatorokea eneo la Sangura alikokaa kwa miaka mitatu, huku anasumbuliwa na dhamiri. Tumefanya uchunguzi wetu tukagundua kuwa ni kweli Zablon Mapisi amekufa. Lakini uchunguzi huo umebainisha kuwa hayati Mapisi alikufa miezi minane iliyopita kwa kujitia kitanzi yeye mwenyewe. Hii hapa

hati ya uthibitisho wa kifo chake”, alimpa karani wa mahakama hati fulani, naye akamkabidhi hakimu.

“Mheshimiwa”, aliendelea mwendesha mashtaka.

“Aidha uchunguzi wetu umethibitisha kuwa mtu mmoja jina lake Tito Tembo, aliwahi kushambuliwa na mtu asiyejulikana katika klabu ya pombe ya busaa huko Falkland, miaka mitatu, iliyopita. Alipata majeraha mabaya. Lakini hakufa. Na maadamu mshtakiwa amekiri katika taarifa yake kwa polisi kuwa alimshambulia mtu, upande wa mashtaka umeamua kumbadilishia mashtaka”.

Kisha mwendesha mashtaka alimkabidhi karani wa mahakama karatasi nyingine naye akaanza kunisomea shtaka langu jipya.

“Wewe Akida Sululu, umeshtakiwa ya kwamba miaka mitatu iliyopita katika mtaa wa Falkland, ulimshambulia na kumjeruhi Tito Tembo, kinyume cha sheria ya jinai nchini Kiwachema sura ya 120, kifungu cha sita.

Je, unakiri au unakanusha mashtaka? .....

“Hebu sema kijana”, alifoka hakimu. “Unakubali au unakataa makosa?”

“Mimi nilimpiga kwa kipande cha ubao akaanguka”,

Nikajibu kidhalili. “Nilidhani amekufa, nikakimbilia .....”

“Kwa hiyo ulimshambulia”, hakimu alinihoji tena, macho kanitumbulia kwa makini.

“Ndiyo Afande”.

“Mheshimiwa hakimu”, alinyanyuka tena mwendesha mashtaka na kuanza kuhutubia mahakama.

“Kabla hujaamua kesi hii, naomba ifahamike kuwa hatuna kumbukumbu za kosa lolote jingine la mshtakiwa.

“Pili, mtuhumiwa amejipeleka kwenye kituo cha polisi kwa hiari yake mwenyewe, miaka mitatu baada ya kutenda kitendo alichokidhania ni kumwua mtu”.

“Mwisho napenda kutaja kuwa mwathiriwa mwenyewe Tito Tembo yuko hapa kortini. Amezungunza nami kimbele na kunitaka niombe korti itupilie mbali kesi hii. Ni hayo tu mheshimiwa”, mwendesha mashtaka alisema ana kuketi kitako kitini.

“Tito yuko wapi?” hakimu aliuliza.

“Niko hapa afande”, alijibu Mzee mmoja mfupi akisimama wima.

“Una lolote la kusema”, hakimu alinigeukia.

“Maisha yangu yamevurugika”, nilisema kwa haya.

“Nataka ... nataka nimtafute babangu. Sijui yuko hai au ... ..

Nataka niendeleo na masomo...”

“Kwa nini ulimshambulia Tito?” hakimu aliniuliza.

“Alituchukia sisi Wakanju.... nilimsikia akisema aliwaua wakanju wengi vitani huko wilayani Korosho. Nilikuwa na hasira. Naomba radhi”.

Hakimu aliandika kwenye faili kwa mkono wake wa kushoto huku kimya kimetawala mahakamani. Moyo wangu ulituturika karibu kukipasua kifua. “Umeachiliwa nenda, lakini usirudie”, alitoa kauli hakimu

(Uk. 191-193).

Maelezo haya ni maigizo kamili yaliyohusisha wahusika katika kunena na kutenda. Kwa mujibu wa Bauman, (1992), miongoni mwa sifa za maigizo ni kuwa huandaliwa mapema kabla ya wakati wake wa kuigizwa. Sifa hii inajitokeza katika mahakama kwa sababu kabla ya Akida kushtakiwa, kulikuwa na maandalizi ya mapema. Anapopelekwa mahakamani, alikuwa awali amewekwa seli, uchunguzi umefanywa, akasomewa mashtaka kabla hajaombwa kujitetea.

Maigizo pia huwa na mwanzo na mwisho maalumu au unaotambulika. Sifa hii pia inajitokeza mahakamani kwa sababu kwanza mwendesha mashtaka anayasoma, kisha baadaye Karani pia anafanya hivyo, hakimu anamwuliza Akida ikiwa anakiri ama kukataa, anaandika kisha anatoa uamuzi wake. Shughuli hizo zote zimefuata utaratibu mahsusi.

Maigizo pia hutendwa katika sehemu maalum iliyotengwa mahsusi kwa shughuli hiyo; kesi ya Akida inatokea mahali maalumu ambapo ni mahakamani. Haingetokea sokoni, barabarani ama hata uwanjani.

Maigizo vile vile ni matukio ya hadhara yanayoshuhudiwa na hadhira. Sifa hii pia imebainika vizuri katika maigizo yanayotokea kortini. Kulikuwamo

hadhira miongoni mwao, Bw. Tito Tembo anayechangia kuachiliwa kwa Akida.

Uigizaji pia wafaa kueleza ukweli wa maisha kwa usahihi unaofaa. Mtendaji lazima azisawiri hali tofauti maishani mwa binadamu katika miktadha tofauti.

Kitabia, Akida alikuwa mtu wa hasira. Lakini afikishwapo kortini, anabadili tabia hii na kuwa mnyenyekevu. Japo wakati mwingine alikuwa mwoga kortini anajipa moyo na kumjibu hakimumu kwa uthabiti.

Miongoni mwa mihimili ya uhalisia ni kuwa wahusika husawiriwa wakiwa wa kawaida na wao hupatikana katika mandhari ya kawaida. Haya yabainika katika mazingira ya kortini Akida anaposhtakiwa. Hakimumu, karani, mwendesha mashtaka na mashahidi pamoja na wanaoshuhudia kesi ni wahusika wa kawaida wanaotarajiwa kupatikana katika mandhari halisi ambayo ni mahakamani.

Vile vile, kazi za kihalisia hutumia lugha ya kawaida kupitia wahusika wake kutegemea muktadha waliomo. Mahakamani, mwendesha mashtaka na hakimumu wanatumia lugha inayoafikiana na shughuli zao katika kesi ya Akida. Baada ya kusikiliza upande wa mashtaka na pia wa utetezi, hakimumu anatoa kauli yake ambayo inaeleweka na Akida. Anasema, “Umeachiliwa, nenda, lakini usirudie” (Uk. 193).

Kazi za kihalisia pia hurejelea matukio yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana na maudhui kwa kiasi kikubwa hulingana na yale ya jamii inayorejelewa. Kabla ya kesi ya Akida, kulitokea mambo fulani ya uhalifu. Kwanza kulikuwa na mauaji katika vita vya kikabila, kisha kuna tukio la kutumia pombe na kauli ya Mzee Tito Tembo jinsi alivyowaua Wakanju. Maneno haya yanasababisha tukio la Akida kumpiga Mzee Tito; huu ulikuwa ni uhalifu. Mambo kama ulevi, vita na vifo ni matukio halisi katika mazingira yetu.

Matukio kama haya hatimaye yanatupeleka katika mandhari yanayojulikana na wahusika na hadhira ili yasuluhishwe; mandhari hayo ni mahakamani.

Maigizo mengine yanatokea katika boma la Mzee Muyaka. Siku moja, Akida alipokuwa amepeleka ng'ombe malishoni, Cynthia bintiye Muyaka alikuja kumwita:

“Madodo!”

“Nini Cynthia”

“Baba amekufa”.

Nikapiga mbio hadi kiamboni. Nikamkuta Mzee Muyaka kaanguka chali kwenye sakafu chumbani mwake, kiwiliwili kinatikisika na jasho jingi kumtoka. ....

Nikamvua koti lake na shati na kumpepea upepo.

... mwajiri wangu alianza kupata nafuu pole pole.

Cynthia akanisaidia tukamnyanyua na kumlaza kitandani.

“Na ... nani... ameiba bunduki yangu? Aliuliza Mzee Muyaka kwa kudodosa.

“Utaipata baba”

(Uk. 167-168).

Akida na Cynthia wameshiriki katika vitendo kadha ili kuokoa maisha ya Muyaka. Akida amekimbia, amemvua nguo Muyaka na kumpepea. Wamenyanyua na kumlaza. Maudhui ya huruma na uwajibikaji yamejitokeza.

Cynthia amemhurumia babake ndiposa akamsaidia ilhali, Akida anawajibika kwa kuitikia wito wa Cynthia.

Mandhari pia hurejelea mahali na wakati wa maigizo, na katika nadharia ya uigizaji, mhusika hubadilika kitabia kutegemea mazingira anamojipata. Hili labainishwa kupitia Akida. Akida alikuwa mwerevu shuleni na hata akatia fora katika mtihani wake wa darasa la saba. Alikuwa na tamaa ya kuendeleza masomo yake. Lakini baada ya kudhani alikuwa ameua, anatorokea Sangura na kujifanya kama mtu ambaye hajui kusoma. Pia anabadilisha jina na kabila lake. Anafanya haya ili kuafiki mazingira alimojikuta. Anasema:

“... Nitatafuta kazi ya shamba. Nikiipata kazi nijifanye zuzu wa kuzuzuliwa na kuifanya kazi hiyo kwa bidii.  
Naam nataka ‘nilale chini kibahasha’, nisiamshe tuhuma zozote dhidi yangu. Hata jina langu nitalibadilisha”.  
(Uk. 142)

Anapofika kwa Mzee Muyaka na kuandikwa kazi; Akida anakabidhiwa Bi.

Tina ambaye alimwuliza kabila lake:

“Mchungwachungwa”  
“Wachungwachungwa ni watu wazuri ila wanapenda ufuska”.  
Alikata kauli Bi. Tina.  
“Kila mtu ana tabia zake mama, .... huwezi kuhukumu kabila zima la watu kwa kosa la mtu mmoja au wawili.  
(Uk. 149).

Mara kwa mara, Bi. Tina alimpongeza Akida.

“Lo! Una bidii ya mchwa madodo, angemwambia.  
“Naam Madodo ndivyo nilivyojulikana sasa.  
Madodo Kipande. Jina la kupanga lililokuwa kinga yangu.  
Usiri ukawa ngao yangu. Unyamavu nao ukawa bunduki yangu.  
Niliamua kuufyata nisije nikajifunga kwa ulimi wangu mwenyewe...”.  
(Uk. 152)

Maudhui ya ukabila na umaskini yanaonekana hapa. Bi. Tina anamwuliza Akida kabila lake na papo hapo akasema kuwa watu wa kabila hilo hupenda ufuska. Umaskini ndio unaomfanya Akida kutoendelea na masomo na badala yake kuajiriwa kazi za shambani.

Mazingira, lugha, wahusika na matukio yanayotokea katika maigizo haya ni kawaida ni hili linaafikiana na nadharia ya uhalisia inayosisitiza hali ya kawaida katika maneno na vitendo vya wahusika. Ni kawaida kwa mwajiriwa kutii amri za mwajiri wake; hili linabainika Akida anapoitikia wito wa Cynthia na kuyaokoa maisha ya Mzee Muyaka.

Maongezi kati ya Akida na Bi. Tina ni ya kawaida. Maongezi hayo yamesheheni pongezi, kejeli, kinaya na hata chuku. Akida anadanganya kuwa yeye ni mchungwachungwa na jina lake ni 'Madodo Kipande', haya yalikuwa kinyume cha ukweli. Bi. Tina naye anatumia chuku kwa kuhukumu kabila lote la wachungwachungwa kuwa wanapenda maovu.

Pia ni jambo la kawaida kwa mtu kusitiri mambo fulani yanayomhusu, hasa akihisi kuwa hayapendezi ama maisha yake yanapokuwa hatarini. Tunashuhudia hayo kwa Akida. Msanii wa kihalisia huchunguza matatizo ya jamii na chanzo chake. Katika maigizo haya, Mzee Muyaka amepoteza bunduki yake na hili linamshtua hadi anazirai. Baadaye tunagundua kuwa alikuwa mmoja wa waliopigana katika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Baadaye, alipewa bunduki na serikali kuwa kama askari wa ziada na iwapo angeipoteza, angefungwa. Uhalisia huangalia namna matukio fulani

yalivyotokea katika kipindi mahsusi cha kihistoria na athari zake; tunayoana haya kupitia kwa Mzee Muyaka.

Regina, bintiye Mzee Uledi pia anaonyesha hali ya kubadilisha tabia zake kutegemea mazingira. Alipokuwa kwao kijijini Baraki, tunaambiwa:

“... Nilimjua sana Mzee Uledi. Regina bintiye tukisoma naye darasa moja huko Baraki. Sisi wanafunzi wenzake tukimwita Regina ‘mtawa’ kwa jinsi alivyojitenga kabisa na mambo ya kimapenzi. Alikuwa msichana msununu aliyekataa katakata kuwakaribia wavulana.”  
(Uk. 74).

Lakini baadaye, Akida anasema kuwa,

“Tamari ndiye aliyenibukulia kuwa Regina, bintiye Mzee Uledi alikuwa kahaba, anajichuuza kwa wanaume kwenye barabara za Tandika.”  
(Uk. 219).

Inaonekana Regina aliamua kubadilisha tabia zake na kujiingiza katika ufuska baada ya kukatishwa tamaa na vita vya kikabila vijijini vilivyosababisha maafa mengi. Maudhui ya vita vya kikabila, na maovu ya kijamii yamegusiwa kupitia vitendo vya Regina.

#### 4.2.5 Mada

Hili ni suala au jambo analolishughulikia mwandishi katika kazi yake (Wamitila, 2003). Katika muktadha wa maigizo au tamthilia, mada yaweza kuwa chanzo, kiini au asili ya mgogoro ambao unaweza ukakuzwa, ukafikishwa kilele na hatimaye kusuluhishwa kupitia maneno na vitendo vya wahusika.

Riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003) inazo sehemu zinazosababisha mikinzano na mitafaruku kati ya wahusika na wanajaribu kuisuluhisha kwa vitendo na maneno na, kwa njia hiyo, kusababisha uwezekano wa uigizaji.

#### 4.2.5.1 Ukabila

Suala hili linasababisha mitafaruku ya maoni kati ya wahusika kwa mfano; mbunge Johnstone Mabende anasema: “Hatutaki ‘madoadoa hapa’. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju”. Kauli hii inapingwa na Alex,”

“Mheshimiwa sasa unaanza kuzungumza kama mtu aliyefunguka skrubu za akili. Wakanju ni ndugu zetu ati. Watu wa fikra kama zako ndio maharabu wa nchi”.

(Uk. 2)

Mfano mwingine ni mjombake Tim, Bw. Samson Tungu:

“Akida ni kabila gani?” aliuliza mjombake Tim.

“Mimi ni Mkanju”, nikajibu kwa tabasamu. Kwanza mjomba wake rafiki yangu aliukunja uso na kuiweka glasi yake ya kinywaji mezani.

“Eti Mkanju?” alitikisa kichwa na kuangua kicheko.

“Kwani mjomba kuna nini?” aliuliza Tim.

“Wakanju?” .....

“Hakuna watu wajinga kama wakanju”

(Uk. 25).

Mkewe Mzee Muyaka, Bi. Tina anamwuliza Akida:

“Wewe ni kabila gani?”

“Mchungwachungwa” Akida akajibu, kisha Bi. Tina anasema”

“Wachungwachungwa ni watu wazuri ila wanapenda ufuska”.

“Kila mtu ana tabia zake mama, huwezi kuhukumu kabila zima la watu kwa kosa la mtu mmoja au wawili, akajibu Akida.

(Uk. 149).

Kupitia maongezi kati ya wahusika, tunaona kuwa suala la ukabila linachangia mvutano na majibizano kati yao kwa mtindo wa mchezo wa kuigiza; mmoja anatoa kauli baada ya mwingine anayepinga na kwa njia hiyo kuendeleza mchezo.

Katika jamii zetu, ni hali ya kawaida kwa watu kupongezana ama kukejeliana kwa misingi ya kikabila. Kazi za kihalisia huangalia mabadiliko ambayo hutokea katika kipindi fulani cha historia na jinsi mabadiliko hayo huzua hali mbalimbali. Kutokana na jinsi Wakanju na Wakorosho wanavyobaguana kikabila, tunagundua kuwa kihistoria, huenda walitawaliwa na wakoloni waliotumia mbinu ya ‘tenga-utawale’ ili kudumisha utawala wao. Baada ya uhuru hali hiyo ya uhasama wa kikabila ilibaki. Makabila tofauti yalitengwa kwa misingi ya elimu, ajira ama rasilmali nyingine za kitaifa. Hili lilizua uadui kati ya waliopendelewa na waliopuuzwa.

Jamii ‘ndogo’ pia zilipewa majina ya maeneo yaliyoakisi makabila yao na zilifanywa kuamini kuwa daima zilikuwa katika hatari ya kuangamizwa na jamii ‘kubwa’. Katika *Kufa Kuzikana* (2003), maeneo yamepewa majina ya makabila. Kuna eneo la Kanju, eneo la Korosho na eneo la Sangura. Tukio kama hili labainika katika mazingira yetu halisi.

#### **4.2.5.2 Ufisadi**

Mada hii pia yazua utata kati ya wahusika na kutoa taswira ya maigizo. Mandhari au jukwaa ni ofisi ya mawakili ya Gembo. Waigizaji ni mhazili

katika ofisi hiyo na wateja wake ni hadhira ‘wanaoshuhudia’ maigizo hayo kupitia taswira zinazotokea akilini mwao; mhazili anasema:

“We’ kijana”, ..... “Kampuni ya Bima ya Akiba haijaleta malipo ya mamako bado. Nenda uje siku nyingine”.  
“nenda uje, nenda uje”, alisema mwanamume mwenye mkono mmoja.  
“Mnafikiri ‘nenda uje’, ni mshumbi wa wali mtu ataula ashibe?  
Basi tumekula tukashiba ‘nenda uje’ hizo mpaka sasa tunazitapika”.  
“Na hapa leo hatutoki mpaka tumemwona Bwana Gembo atulipe pesa zetu”. (Uk. 46).

Kampuni hii ya mawakili haikuwa imefidia wateja wake athari mbalimbali walizopata kutokana na ajali. Hili lasababisha ubishi na malumbano kati ya wateja na mhazili.

Katika kazi za kihalisia, mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana. Maudhui na matukio kwa kiasi kikubwa yanatakiwa kulingana na yale ya jamii inayorejelewa. Mhimili huu unajitokeza katika mifano iliyorejelewa hapo juu; suala la ukabila na ufisadi ni mambo yaliyokita katika jamii zetu.

#### 4.2.5.3 Mila na Athari Zake

Mazungumzo kati ya Akida, rafikiye Tom na mkewe Jenelle yaonyesha misimamo waliyo nayo kuhusu baadhi ya mila.

“Huyu ni Akida”, alijulisha Tom. “Rafiki yangu kutoka Baraki”.  
“Anaitwa ....” Tom alijaribu kudakia.  
“Ah! Jina langu si muhimu ....

Tangu nifike Kiwachema miaka mitatu iliyopita, nimeona watoto na wanawake. Wakinasibishwa tu na baba na waume zao.  
Mathalan kule Baraki Tom si Tom, ni mtoto wa Mangala, nami si Jenelle, ni mke wa mtoto wa Mangala, na kadhalika”. Sote tukaangua kicheko.

“Lazima nizingatie mila ya watu wa Tom”.

“Lakini sasa tayari umevunja miko”, alisema Tom kwa ucheshi.

“Kwa njia gani?”

“Umeliita jina la baba mkwe”.

“Samahani nimeghafilika”. Tunacheka tena.

“Baadhi ya mila zimepitwa na wakati, bora zitupwe kwenye kapu la sahu”, alisema Tom.

“Pengine ni kweli. Maana kwa mfano sielewi kwa nini baba mkwe wangu hawezi kuishi nasi hapa katika nyumba hii...”

“Na akifa?” aliongeza, “Hupaswi kuiona maiti yake. Unaruhusiwa kwenda matangani baada ya yeye kuzikwa”. (Uk. 82-83).

Mfano mwingine ni mazungumzo kati ya Cynthia, bintiye Muyaka na Akida,

Akida aeleza:

“Jioni hiyo Cynthia alininong’onezea, nyanya anataka nitahiriwe safari hii”.

“Hujatahiriwa?”

“Bado”

“Na Susana?”

“Susana alitahiriwa kabla hujaja janibu hizi. Ningetahiriwa pamoja naye lakini mama akasema ningali mdogo. Imepita miaka kadha mama akitoa kisingizio hiki na kile”.

“Na baba”.

“Anamwunga mkono bibi”.

“Na wewe?”

“Dada zangu wote wakubwa wametahiriwa. ... zamani nilifikiria ni sawa.

Lakini sasa sitaki.”

“Kwa nini?”

“Nasikia kuna madhara. Wasichana wengi hufa. Rafiki zangu wawili walifariki mwaka jana pale ng’ambo”.

(Uk. 170).

Kupitia dondoo hili, baba na nyanyake Cynthia wanaunga mkono tohara ya wasichana ilhali Cynthia na mamake wanapinga mila hiyo. Maongezi kati yao yanazua hali ya uigizaji.

Kazi za kihalisia huangalia maisha katika ngazi zote kama za kijamii na kitamaduni. Hili labainika katika kauli za wahusika wa riwaya hii. Masuala ya

kijamii yanayorejelewa ni adabu, na tohara. Maudhui haya ya mila na matokeo yake yanazua mikinzano kati ya wahusika na hili hutokea katika maisha halisi.

Mkewe Tom; Jenelle analalamika kuwa ameona watoto na wanawake wakihusishwa tu na majina ya wanaume. Hili ni tatizo la ubaguzi wa kijinsia ambalo hushuhudiwa pia katika maisha ya kawaida ya jamii zetu.

Pia Jenelle haelewi ni kwa nini hawawezi kuishi na baba mkwe wake katika nyumba moja. Jambo hili pia lazua swali iwapo inafaa tuendelee kufuata tu mila zote kipofu ama nyingine zisizofaa ziachwe.

Wahusika wa kihalisia pia hujengwa wakiwa wa kawaida na wakiwakilisha jamii zao na kupitia kwao, ukweli unafaa uonekane. Jenelle na Tom ingawa wameoana wote wanawakilisha jamii tofauti. Jenelle anawakilisha wageni, naye Tom anawakilisha wenyeji. Jenelle amesawiriwa kama mhusika aliyejikomboa kimawazo na haya yanaonekana kupitia kauli zake za ukweli anazotoa kuhusu maana ya kuendelea kufuata baadhi ya mila. Tom naye ingawa amepata elimu ya kisasa, bado ni mhafidhina anayezingatia mila za kiasili bila pingamizi.

Suala la tohara linazua mikinzano katika aila ya Mzee Muyaka. Yeye analiunga mkono ilhali Cynthia na Bi. Tina walipinga. Cynthia akiwa mfano wa mhusika wa kihalisia, anasema ukweli kuwa ingawa dada zake wakubwa walikuwa wametahiriwa na kuwa awali alidhani hili ni sawa, sasa alikuwa anapinga mila hiyo. Anasema husababisha madhara na hata vifo.

Mikinzano inayotokana na mila vile vile inabainika katika riwaya ya *Mali ya Maskini* (1981) ya Zainabu Burhani. Kadiri anamweleza bintiye Zahara kuhusu posa ya waziri Selemani ya kutaka kumwoa Zahara. Ni jambo la kawaida kwa posa kupitia kwa wazazi wa binti na pia kwa wazazi hao kumshauri binti yao. Mazungumzo kati ya Zahara na babake, Kadiri yanatoa taswira ya uigizaji.

“Unamjua Selemani, yule waziri ..... amekuja kukuposa, anataka kukuo, ikiwa utakubali”

“... sina haja ya kufikiri baba, mimi simtaki”.

“Ina maana kuwa hutaki bado kuolewa kwa sasa, au humtaki huyo Selemani tu?”

“Huyo Selemani simtaki”.

“Unaweza kuniambia kwa nini?” aliuliza Kadiri

“Kwanza ni mtu mzima”, alijibu Zahara.

“Kwa hivyo unataka mume kijana”, aliitikia Kadiri na Zahara alicheka kwa mara ya kwanza katika muda mrefu.

“Pili?” aliuliza Kadiri.

“Simpendi hata kidogo”, alisema Zahara huku akikunja pua.

Kadiri alicheka na kusema, “Ah, nafikiri unasoma hadithi nyingi. Ukikaa na mumeo na kumzoea utaweza kumpenda baadaye”.

(Uk. 94 – 95).

Huu ni mfano mzuri wa maigizo yanayorejelea suala la kawaida maishani.

### **4.3 Kiishilio**

Sura hii imetoa maelezo ya jumla kuhusu riwaya ya *Kufa Kuzikana* (2003).

Mtiririko wa riwaya hii umerejelewa kutoka mwanzo hadi mwisho, wake huku wahusika na vitendo vyao muhimu vikigusiwa.

Sura hii pia imeshughulikia uigizaji na uhalisia na kudhihirisha namna nyenzo hizo zilivyotumiwa kubainisha maudhui ya mwandishi. Vipengele muhimu vya maigizo vilivyorejelewa ni: tabia ya wahusika, lugha ya wahusika,

mandhari ya matukio na mada zilizosababisha matukio fulani. Vipengele hivi vimejadiliwa kwa mujibu wa nadharia za uhalisia na uigizaji huku maudhui muhimu yaliyojitokeza kwa kila maigizo yakibainishwa.

Maudhui yaliyojitokeza ni kwa mfano, ukabila, ufisadi, ubinafsi, huduma duni katika maofisi, kutowajibika, unyanyasaji na suala la mila na athari zake. Haya yamebainishwa kupitia maneno na vitendo vya wahusika; vipengele vilivyochangia kubainika vyema kwa maudhui ya riwaya hii.

Sura inayofuata ni ya tano na ndiyo sura ya mwisho. Katika sura hiyo, hitimisho la utafiti limetolewa. Matokeo ya utafiti yameelezwa na matatizo yaliyomkabili mtafiti kutajwa. Hatimaye, mchango wa utafiti huu umemulikwa pamoja na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## SURA YA TANO

### HITIMISHO LA UTAFITI

#### 5.0 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho la utafiti huu na inashughulikia, kati ya mambo mengine, muhtasari, na pia matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti. Matatizo yaliyokabili utafiti huu yameelezwa pia. Aidha, sura hii imetoa mchango wa utafiti na hali kadhalika mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili katika uga wa riwaya.

#### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Mada ya utafiti huu ni maigizo kama mbinu ya maudhui katika riwaya za Walibora. Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna Walibora alivyotumia mtindo wa kitamthilia au maigizo katika kueleza maudhui ya riwaya zake. Utafiti huu pia ulilenga kudhihirisha namna uhalisi unavyojitokeza katika vitabu vya mwandishi huyu kupitia mandhari, vitendo na maneno ya wahusika. Aidha, utafiti ulilenga kuonyesha ya kwamba riwaya za Walibora ni mifano mahsusi ya mwingiliano kati ya sifa za riwaya na sifa za tamthilia. Utafiti pia ulilenga kuonyesha ikiwa maudhui ya riwaya za mwandishi huyu yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuyafanya masimulizi yake yawe kama maigizo.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti, suala la utafiti, nadharia tete na malengo ya utafiti. Sababu za kuchagua mada hii na misingi ya nadharia pia yameelezwa katika sura hii.

Aidha, sura imerejelea yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo na mipaka ya utafiti, zikiwemo pia mbinu zilizotumika kuendeleza utafiti huu.

Sura ya pili imerejelea mwandishi wa kazi zilizotafitiwa. Sura hii imefafanua historia, usuli na kazi za Walibora. Kazi zilizorejelewa ni riwaya, vijiriwaya na hadithi fupi. Baadhi ya kazi zake ambazo hazijachapishwa pia zimepitiwa kwa ufupi.

Sura ya tatu imetoa maelezo juu ya kijiriwaya ya cha *Ndoto ya Amerika*. Sura hii pia imechunguza namna uigizaji ulivyotumiwa kubainisha maudhui katika *Ndoto ya Amerika*. Vipengele vya maigizo vilivyoshughulikiwa ni sifa za wahusika, maneno na vitendo vyao, lugha ya wahusika, mandhari na mada husika. Hivi vimetumiwa kubainisha maudhui katika kijiriwaya hiki kulingana na malengo ya utafiti. Riwaya nyingine za Kiswahili ambazo pia zina sifa za uigizaji zimerejelewa kwa ufupi.

Sura ya nne imejadili riwaya, *Kufa Kuzikana* kwa kutoa maelezo ya jumla ya riwaya hiyo. Aidha, sura hii pia imechunguza namna uigizaji na uhalisia vilivyotumiwa kama njia ya kubainisha maudhui katika *Kufa Kuzikana*. Miongoni mwa maudhui yaliyofafanuliwa ni uhalifu, ukabila, umaskini, mila na athari zake na ubinafsi. Maudhui haya yamefafanuliwa kwa kuzingatia vipengele vya uigizaji. Vipengele vilivyozingatiwa ni tabia za wahusika, maneno na vitendo vyao, lugha wanayoitumia, mandhari ya matukio pamoja na mada zilizohusika. Haya yameshughulikiwa kwa mujibu wa mada na

malengo ya utafiti. Aidha, kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili, hasa riwaya na ambazo zina mifano ya maigizo zimepitiwa kwa ufupi.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu. Hitimisho hili limetoa utangulizi na muhtasari wa utafiti. Aidha, limetoa muhtasari wa kila sura. Maelezo ya matokeo ya utafiti yamefafanuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye, sura hii imetaja matatizo, mchango wa utafiti na mapendekezo ya tafiti ambazo zinaweza kufanywa siku za baadaye katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili katika kitengo cha riwaya.

Matumizi ya nadharia zilizoteuliwa yalitokana na sababu kwamba zote mbili zilitarajiwa kuhimili kazi hii. Wataalamu ambao walitumia nadharia ya uigizaji, waliitumia kuchunguza tamthilia na siyo riwaya kama ilivyobainika katika utafiti huu.

Nadharia ya uhalisia hushughulika na mambo ya ushabihikweli yanayoweza kupatikana katika jamii. Katika utafiti huu pamekuwa na azma ya kuona ni kwa kiasi gani vitabu vya Walibora vimejikita katika uhalisi wa maisha.

Kupitia nadharia ya uigizaji, utafiti huu ulilenga kuainisha sifa zinazozifanya riwaya za Walibora kubainika zaidi kama maigizo kuliko kama masimulizi ya kinathari. Vile vile ulinua kuchunguza ikiwa maudhui ya riwaya za Walibora yalichangia kwa kuyafanya masimulizi yake yawe kama maigizo.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti kuhusu Kazi za Walibora

Kutokana na utafiti huu, imebainika kwamba fasihi ya Kiswahili, na hasa uandishi wa riwaya, haukuwa ukizingatiwa sana na waandishi wa Kenya baada ya uhuru, lakini utanzu huu umeendelea kuwa maarufu jinsi miaka ilivyozidi kuendelea. Kwa wakati huu, waandishi wa riwaya za Kiswahili wameongezeka na maudhui wanavyoyashughulikia yamekuwa yakibadilika kutegemea wakati unaohusika.

Mbinu wanazotumia katika kuandika kazi zao zimekuwa zikibadilika kutegemea mapisi ya wakati. Kutokana na hadhira mseto na masuala mapya yanayoibuka katika mazingira yetu na vile vile mabadilko ya kiteknolojia, imewalazimu baadhi ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili kutunga kazi zilizo na sifa mseto. Maana hapa ni kuwa utanzu kama wa riwaya unaweza kuwa na sifa za kitamthilia. Sifa kama hizi zimebainika katika kazi za Walibora zilizo changanuliwa.

Ingawa Walibora ameandika kazi za kinathari au riwaya, kazi hizo zina sifa zinazoweza kuzifanya zikaigizika. Mifano ya riwaya hizo ni *Kufa Kuzikana* (2003) na *Ndoto ya Amerika* (2001). Katika kazi hizi, Walibora amewahusisha wahusika katika mazungumzo ya ana kwa ana na vitendo mbalimbali ambavyo vinazifanya riwaya hizi kubainika zaidi kama tamthilia ama maigizo ya jukwaani kuliko riwaya.

Baadhi ya vipengele vya maigizo ambavyo Walibora ametumia ili kufanya kazi zake ziweze kuigizika ni kama sifa za wahusika, lugha wanayoitumia

wahusika hao na vitendo wanavyojihusisha navyo. Vipengele hivi vimesaidia kubainisha kwa uwazi zaidi maudhui ambayo mwandishi angependa yaifikie hadhira yake.

Kupitia utafiti huu, majibu ya masuala ya utafiti yamebainika kupitia kazi za Walibora zilizotafitiwa. Ingawa kazi hizo zilikuwa za kinathari; kupitia utafiti huu, masimulizi hayo yamebainika zaidi kama tanzu za kuigizwa kuliko za kuelezwa moja kwa moja. Sababu ni kwamba mwandishi ametumia mbinu mbalimbali katika kuyafanya masimulizi yake yabainike kama maigizo kuliko maelezo.

Kwanza, utafiti umebainisha kwamba mwandishi ametumia wakati uliopo katika sehemu nyingi za kazi zake na kwa njia hiyo kuyafanya matukio katika kazi hizo kuonekana kama yaliyokuwa yakitokea jukwaani moja kwa moja na kushuhudiwa na hadhira. Jambo hili pia liliyapa uhai zaidi maudhui yaliyokuwa yakipitishwa. Mifano ya maudhui hayo ni ukabila, ubinafsi na athari za uhalifu pamoja na ukatili kwa watoto.

Kupitia utafiti, imebainika pia kuwa mwandishi amewahusisha wahusika wake zaidi katika vitendo vilivyoandamana na matamshi ama kauli zao ambazo zilitolewa moja kwa moja na wahusika wenyewe. Hali kama hii inaweza kuziteka hisia za hadhira ili kuyazingatia yanayowasilishwa kwao. Jambo hili pia hujenga taharuki miongoni mwa hadhira.

Imebainika pia kwamba, Walibora amewashirikisha wahusika wa kazi zake katika mazungumzo ya moja kwa moja. Wahusika wanaonekana wakiongea kwa zamu, mfano ni Isaya na Madoa; wanahojiana na kujibizana kwa mfano; Akida na mwanahabari, wanakasirikiana kwa mfano, Mhazili wa Gembo na wateja wake. Wengine wanagombana na kupatana kama Akida na Tamari. Mbali na kuleta uhai katika kazi za mwandishi; jambo hili pia linawafanya wahusika waonekane kama wanaoigiza zaidi kuliko kusimuliwa.

Kupitia utafiti, imebainika vile vile kuwa Walibora ametumia binadamu halisi kama wahusika wake. Binadamu hao pia ni wa aina zote. Kuna watoto na watu wazima, wanawake na wanaume, wema na waovu. Hili ni jambo linalopatikana katika maisha halisi.

Kupitia utafiti, imebainika pia kuwa mwandishi ametumia mandhari halisi na ya aina mbalimbali yanayolingana na maudhui anayoyashughulikia. Kuna mandhari ya shuleni, kortini na sokoni yanayoakisi shughuli za elimu, udumishaji sheria na biashara. Isaya na Madoa wamekutwa shuleni wakisoma, lakini baadaye tunamwona kortini kama wahalifu. Kwa nyakati tofauti Akida anakuwa mwanafunzi, mfanyikazi, msafiri, na mfungwa kutegemea mandhari aliyomo Bw. Samson Tungu naye ni mwajiri na pia mzazi kutegemea mazingira yake. Mandhari kama haya hupatikana katika maisha halisi.

Kupitia utafiti, imebainika kuwa baadhi ya maudhui ya riwaya za Walibora yamechangia kuzifanya riwaya hizo zionekane kama maigizo zaidi kuliko masimulizi. Baadhi ya maudhui ambayo yamebainika ni ubinafsi, ufisadi,

ukatili, ukabila na umaskini. Isaya na Madoa waliadhibiwa na kufanyishwa kazi kila mara na wazazi wao; shuleni, walichapwa na walimu. Maudhui ya ukatili katika *Ndoto ya Amerika* (2001) yanaonyesha wahusika wakitekeleza vitendo vyao vya kikatili.

Katika *Kufa Kuzikana* (2003), ukatili unabainika kupitia vita vya kikabila vinavyoshirikisha wengi katika vitendo kama kuua, kukata, kupiga na kutupa. Wanatumia pia maneno ya uchochezi, kejeli, kinaya na chuku. Wakanju na Wakorosho wanauana kupitia uchochezi wa watu kama Johnstone Mabende.

Ubinafsi wa 'Rock Mwamba' katika *Ndoto ya Amerika* (2001) unamfanya awashirikishe Isaya na Madoa katika uhalifu. Hili linazua mfululizo wa vitendo mbalimbali vinavyoonekana kama maigizo. Katika *Kufa Kuzikana* (2003), ubinafsi unadhihirika kupitia malumbano kati ya Mhazili wa Gembo na wateja. Mhazili hataki kuwahudumia; badala yake anawabeza na kuwatisha. Ubishi unaotokea baina yao ni mfano wa maigizo.

Umaskini umebainika kupitia wahusika kama Mzee Uledi, Akida, Tim na Tamari. Mzee Uledi anaonekana akiwa kando ya barabara jijini Tandika. Anamwiita na kumnyoshea mkono yeyote anayepita ili amsaidie. Akida, Tim na Tamari wanaishi katika chumba kimoja kidogo. Wavamizi wanapotaka kumwua Akida, kunatokea sarakasi katika chumba hicho na maisha ya Akida yanaokolewa. Maudhui haya na mengine ni mambo halisi yanayopatikana katika ulimwengu wa kweli.

Utafiti umeweza kubainisha ya kwamba riwaya za Walibora ni mifano mahsusi ya mwingiliano kati ya utanzu wa riwaya na wa tamthilia kwa sababu kazi zilizohakikiwa zimebeba sifa za tanzu hizo mbili.

Mwandishi ametumia maelezo pamoja na vitendo na maneno ya wahusika kuendeleza maudhui mbalimbali. 'Rock Mwamba' amechorwa kama mhusika jasiri jinsi Madoa anavyomwelezea Isaya. Lakini anapofika mahakamani, anakuwa mtiifu. Anapoitwa na hakimu, anasimama na kuitikia kwa heshima. Hili linamgutusha sana Isaya.

Tunaelezwa pia namna Akida na Tamari wanavyokosana na Akida kuelekea katika klabu ya pombe. Huko, anakasirishwa na Mzee Mapisi. Anaamua kumpiga na kisha anaabiri basi hadi eneo la Sangura ambako anabadilisha jina pamoja na kabila lake. Mandhari haya tofauti yanajenga picha ya maigizo.

### **5.3 Matatizo ya Utafiti**

Utafiti huu ulikabiliwa na matatizo fulani. Mojawapo ya matatizo hayo ni tafsiri. Ili kuweza kupata maana ya dhana mbalimbali zilizotumiwa, mtafiti alilazimika kusoma vitabu vya Kiingereza na baadaye kutafsiri dhana hizo. Jambo hili halikuwa rahisi kutekeleza.

Tatizo jingine ni kuwa, maelezo mengi kuhusu nadharia zilizotumiwa yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Halikuwa jambo sahali kutafsiri zile dhana zilizotumiwa katika nadharia na ujumbe muhimu kwa jumla. Licha ya

hayo, kulikuwa na tahakiki chache zilizoandikwa kuhusu uigizaji katika riwaya. Tahakiki nyingi zilizoandikwa ziliegemea upande wa tamthilia.

Mwandishi ambaye kazi zake zilitafitiwa hakuwa nchini wakati utafiti huu ulipokuwa ukifanywa. Juhudi za mtafiti kuwasiliana naye kupitia barua pepe hazikufaulu. Kwa hivyo, mtafiti alilazimika kurejelea makala tofauti katika vitabu, majarida na magazeti ili kupata habari zilizohitajika.

#### **5.4 Mchango**

Kupitia utafiti huu, imebainika kuwa inawezekana tukawa na mtazamo mwingine tofauti wa kuhakiki riwaya kuliko mitazamo iliyo zoeleka.

Utafiti pia umeonyesha kuwa kazi za Walibora na hasa riwaya, zina sifa na miundo ya kitamthilia inayoweza kuigizika na kwa namna hiyo kumwezesha kuwasiliana na hadhira yake moja kwa moja na kurahisisha ujumbe ambao huenda angetaka uifikie hadhira kama hiyo. Mifano ya kazi hizo ni kama hizi zilizohakikiwa.

Mchango mwingine wa utafiti huu ni kuwa awali hakukuwako na kazi kumhusu Walibora na iwapo zimekuwako basi zilikuwa chache. Utafiti huu kwa hivyo ni miongoni wa kazi za kwanza zilizohakiki baadhi ya kazi za Walibora kwa kina na utakuwa wa manufaa kwa watakaopenda kuzungumzia kazi nyingine za mwandishi huyu.

Utafiti pia umeshirikisha nadharia mbili za uhalisia na uigizaji na kubainisha namna zinavyoweza kutumiwa katika kuhakiki utanzu wa riwaya.

### 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia uhalisia na uigizaji katika riwaya teule za Walibora. Vitabu vilivyotafitiwa vilikuwa riwaya moja na kijiriwaya kimoja. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanyiwe vitabu vingine vya mwandishi huyu hasa kwa upande wa uhusika na namna sifa za wahusika zinavyofanana katika kazi tofauti za mwandishi huyu. Hili ni jambo ambalo halijashughulikiwa kwa kina. Aidha, mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu mandhari ya matukio na jinsi ambavyo mandhari hayo huchangia katika kujenga na kuendeleza masuala yanayoshughulikiwa na mwandishi. Pia inapendekezwa kuwa utafiti zaidi ufanyiwe kazi za mwandishi hasa kwa namna anavyoangazia masuala nyeti na masuala ibukizi katika jamii.

## MAREJELEO

- Achebe, C. (1979): *Shujaa Okonkwo*: Nairobi, EAPH.
- Aktivaga, S. na E. Gachukia (1975): *Teaching of Literature in African Schools*: Nairobi, K.L.B.
- Alembi, E.B. (2000): *Appreciating Drama*: Nairobi, Acacia Stantex Publishers.
- Allen, J. (1979): *Drama in Schools: It's Theory and Practice*: London, Heinemann Educational Books.
- Alington, A.F. (1970): *Drama and Education*: Oxford, Basil Blackwell
- Anaye, J. V. (2004): "Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi: Uchanganuzi wa Riwaya za Mkangi, G. K. Mafuta (1984) na Walenisi (1995)" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Austen, J. (1966): *Emma*: Harmondsworth, Penguin.
- Baldrick, C. (1990): *The Concise Oxford Dictionary of Literary Terms*: England, Clays Ltd.
- Bauman, R. (1986): *Story, Performance and Event*: New York, Cambridge University Press.
- Bauman, R. (Ed.) (1992): *Folklore, Cultural Performances and Popular Entertainment*: New York, O.U.P.
- Bibilia Takatifu (1989): Nairobi, Evangel Publishing House.
- Burhani, Z. (1981): *Mali ya Maskini*: Nairobi, Longhorn (K) Ltd.
- \_\_\_\_\_ (1987): *Mwisho wa Kosa*: Nairobi, Longhorn (K) Ltd.
- Cass, J. E. (1967): *Literature and the Young Child*: London, Longman Group Ltd.
- Coombes, H. (1953): *Literature and Criticism*: London, Penguin Books.
- Cuddon, J. A. (1979): *A Dictionary of Literary Terms*: London, Deutsch.
- Eagleton, T. (1983): *Literary Theories: An Introduction*: Oxford, Basil Blackwell Publishers.
- Etherton, M. (1982): *The Development of African Drama*: London, Hutchinson, and Company.

- Eyo, H. N. (1987): "Theatre, Televisions and Development: A Case Study for the Third World" Katika Jarida la Africa Media Review: Toleo 1 Nambari 3. Nairobi: African Council for Communication Education.
- Foster, E. M. (1960): *Aspects of the Novel*: Harmondsworth, Penguin.
- Geranija, P.C. & Muwanga, A.S (1976): *Doa la Mauti*: Nairobi, EAEP.
- Gikandi, S. (1987): *Reading the African Novel*: Nairobi, Heinemann.
- Gituku, N. (1990): "Maigizo ya Kienyeji ya watoto nchini Kenya" Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Goodland S. R. (1971): *The Sociology of Popular Drama*: London, Heinemann Educational Books.
- Hardy, T. (1974): *Far from the Madding Crowd*: London, Macmillan.
- Hegel, G. W. F. (1979): *Introduction to Aesthetics*: Oxford, Clarendon.
- Hilton, J. (1987) *Performance*: London, The Macmillan Press Ltd.
- Jamaadar, A. (1978): *Mui huwa Mwema*: Nairobi, Longman (K) Ltd.
- Kairu, W.M. (2005): "Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Kamau, M. (1992): "Ufundi katika Riwaya za Mohamed S. Abdullah" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Kezilahabi, E. (1971): *Rosa Mistika*: Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_ (1974): *Kichwamaji*: Nairobi, East Africa Publishing House.
- \_\_\_\_\_ (1978): *Gamba la Nyoka*: Arusha, East Africa Publications.
- Larkin, M. (1977): *Man and Society in the Nineteenth Century Realism*: London, Macmillan.
- Leech G. & Short M. (1981): *Style in Fiction*: Essex, Longman Group Ltd.
- Leger, L. (1990): *Creating Unforgettable Characteristics*: New York, Henry Holt and Company.
- Levitt, P.M. (1971): *Structural Approach to Analysis of Drama*: The Hague, Mouton.
- Lukacs, G. (1963): *The Meaning of Contemporary Realism*: London, Merlin Press.

- \_\_\_\_\_ (1972): *Studies in European Realism: A Sociological Survey of Writings of Balzac, Stendhal, Zola, Tolstoy, Gorki and Others*; London, Marlin Press.
- Lutwack, L. (1984): *The Role of Place in Literature*; Syracuse, Syracuse University Press.
- Macherey, P. (1978): *A Theory of Literary Production*; London, Routledge.
- Magaju, J. (2004): "Uhaliajabu katika *Babu Alipofufuka na Binaadamu*": Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Mahero, J. A. (1992): "Maoa ya Jamii katika Tamthilia za Chacha N. Chacha; Swala la Uongozi" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Masinde, E. (2003): "Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui" Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Mwangi, M. (1974): *Carcase for Hounds*; Nairobi, Heinemann.
- Mazrui, A. M. na B. K. Syambo, (1992): *Uchambuzi wa Fasihi*: E.A.E.P.
- Mbaabu I. (1985): *New Horizons in Kiswahili: Asynthesis in Developments, Research and Literature*: Nairobi, K.L.B.
- Mbatiah, M. (2001): *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi, Standard Textbooks, Graphics and Publishing.
- Mbele, M. (1980): *View Points: Essays on Literature and Drama*: Nairobi, K.L.B.
- Mbughuni, P. M. (1978): *From Oral to Written – The Politicization of Kiswahili Literature*,. Michigan University Microfilms.
- Mead, H.M. (1938): *The Philosophy of the Act*: Chicago University Press.
- Mkangi, G. K. (1995): *Walenisi*: Nairobi, EAEP Ltd.
- Mohamed, S. A. (1995): *Kunga na Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*: Nairobi, E.A.E.P.
- Mohamed, S. M. (1972): *Kiu*: Longhorn (K) Ltd.
- \_\_\_\_\_ (1976): *Nyota ya Rehema*: Nairobi, OUP Ltd.
- Momanyi, C. (1991): "Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

- Msokile, M. (1992): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi, E.A.E.P, Ltd.
- Mugambi, P.M.J. (1982): "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Muhando, P. na N. Balisidya, (1976): *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*: Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.
- Mukobwa, J. M. (1985): "Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia Tano za E. Hussein". M.A. Thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mule, K. (1991): "Swala la Mwanamke katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa Kike katika Njia Panda": Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Ngara, E. (1982): *Stylistic Criticism and the African Novel*: London, Heinemann.
- Ngure, A. (2003): *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*: Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.
- Ng'weno, H. Et al (2005): *Usiniharakishe*: Nairobi, Mvule, Africa Ltd.
- Njogu, K. na R. Chimerah, (1999): *Ufundishaji wa Fasihi-Nadharia na Mbinu*: Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.
- Njue, J. G. (1994): "Language Choice and the Young Kenyan Playwright" in Forum, Nairobi, Writers Association of Kenya.
- Packard, W. (1997): *The Art of the Playwright*: New York, Thuna Mouth Press.
- Robinson, K. (ed) (1980): *Exploring Theatre in Education*: London, H.E.B.
- Saturday Nation (18/8/2001): Katika "Nation Profiles – Know your Broadcasters" Yakirejelea Wasifu wa Ken Walibora, Nairobi. Nation Media Group Ltd.
- Senkoro, F.E.M. K. (1982): *Fasihi*: Dar es Salaam, Press and Publicity Centre.
- Scher, A. na C. Verall, (1975): *100 Ideas for Drama*: London, H.E.B.
- Sunday Nation (29/2/2004): Katika 'Lifestyle' yakirejelea wasifu wa Ken Walibora, Nairobi, Nation Media Group Ltd.
- Ngugi T. (1972) *Home Coming: Essays on African and Carribean Literature, Culture and Politics*: Nairobi., Heineman.

- \_\_\_\_\_ (1986): *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*: Nairobi, Heineman.
- Tolstoy, L. (1949): *What is Art?* Oxford, Oxford University Press.
- Traore, B (1972): *The Black Africa Theatre and its Social Functions*: Ibadan, Ibadan University Press.
- TUKI (2000): *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*: Toleo la Pili, Dar es Salaam.
- TUKI (2001): *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*: Toleo la Pili, Dar es Salaam.
- TUKI na OUP (2004): *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Nairobi.
- Wafula, R. M. (1999): *Uhakiki wa Tamthilia-Historia na Maendeleo Yake*: Nairobi, J.K.F.
- Walibora, K. (1996): *Siku Njema*: Nairobi, Longhorn.
- \_\_\_\_\_ (2001): *Ndoto ya Amerika*: Nairobi, Sasa Sema Publications.
- \_\_\_\_\_ (2003): *Mgomba Changaraweni*: Nairobi, Phoenix Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003): *Mtu wa Mvua*: Nairobi, Phoenix Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003): *Kufa Kuzikana*: Nairobi, Longhorn Publishers.
- Walibora, K. et al (2004): *Uhondo wa Kiswahili*: Kidato cha Kwanza, Nairobi, Macmillan Kenya.
- Walibora, K. & H. Mogambi, (2005): *Uhondo wa Kiswahili*: Kidato cha Nne, Nairobi, Macmillan Kenya.
- Walibora, K. (2005): *Mwongozo wa Mwisho wa Kosa*: Nairobi, Sasa Sema Publications.
- Walibora, K. (2006): *Ndoto ya Almasi*: Nairobi, Macmillan Kenya.
- Wamitila, K. W. (2002): *Uhakiki wa Fasihi-Misingi na Vipengele Vyake*: Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003): *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*: Nairobi, Focus Publishers Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003): *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*: Nairobi, Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (Mh.) (2004): *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*: Nairobi, Focus Publishers Ltd.

Warritay, B. (1988): "Communication Development and Theatre use in Africa", *Katika Africa Media Review*" Toleo 2. Nambari 3 Nairobi, African Council for Communication Education.

Webster, B. (1975): *Working with Theatre in Schools*: London, Sir William and Sons Ltd.

Wellek, R. (1965): *A History of Modern Criticism: 1750-1950*, Vol. 3, Cambridge, Cambridge University Press.

Wellek & Warren (1949): *Theory of Literature*: Harmondsworth, Penguin.